ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Sita - Tarehe 17 Mei, 2017

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

KIAPO CHA UAMINIFU CHA MHE. MJUMBE WA BARAZA

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil

(Mheshimiwa aliyetajwa hapo juu aliapa kiapo cha uaminifu na kukaa katika sehemu yake ndani ya Baraza la Wawakilishi.)

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa mujibu wa marekebisho wa kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi tulizofanya mwishoni mwa mwaka 2016, kanuni ya 40(4) kinahitaji maswali ya nyongeza yanayojibiwa kwa maandishi, yawasilishwe mbele ya Baraza kwa kupitia taarifa ya Spika.

Madhumuni ya kanuni hii ni kuwawezesha wananchi kufahamu majibu ya maswali hayo yanayoulizwa kwa niaba ya wananchi wanaowakilishwa kwenye chombo hiki.

Waheshimiwa Wajumbe, mwanzoni mwa mkutano huu wa bajeti Mhe. Masoud Abrahman Masoud Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Bububu, aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi akitaka kujua thamani ya fedha iliyotumika kwa ununuzi wa dawa ya *ansonil*. Katika kutimiza masharti ya kanuni hiyo ya 40(4) ya kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2016, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeleta jibu lifuatalo ambalo napenda kulisoma mbele yenu Waheshimiwa Wajumbe na kwa wananchi kwa ujumla.

Waheshimiwa Wajumbe, ni kweli Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ilinunua dawa hiyo ya *ansonil* kwa ajili ya kuulia magugu ya mpunga katika msimu wa kilimo wa mwaka 2015/2016. Kwa mujibu wa mkataba wa manunuzi, MANR/PMU/GO2/2015/2016 uliosainiwa tarehe 13 Januari, 2016 na thamani ya dawa hiyo ni shilingi milioni 504. Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuruni sana. *(Makofi)*

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaendelea kuwataja waheshimiwa kuendelea kuichangia hii hoja, naomba kwanza kuwasomea wageni ambao wamefika mbele yetu. Wageni hao ni wa Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais. *(Makofi)*

Wageni hao ni wanafamilia wa Mhe. Ahmada Yahya na ni kama wafuatao. Kwanza Mama Fatma Amour mama watoto wake naomba asimame. Karibu sana. Pili ni ndugu Sada Ahmada ambaye ni mwanawe na yeye naomba asimame na wa tatu ni ndugu Yunus Ahmada ambaye pia ni mwanawe karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya taarifa hiyo ya wageni nadhani mtaona kwamba kwa siku ya leo tumeondosha maswali na ni kwa sababu waheshimiwa ambao mmeomba kuchangia hoja hii ambayo tunajaribu sana kuihitimisha leo hii ni wengi. Kwa hivyo, tumeondosha maswali ili kuwapeni nafasi watu wengi zaidi kuweza kuchangia hii hoja, ili hatimae leo kabla ya salat Ishai tuweze kuikamilisha hii hoja. Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumwita Mhe. Mnadhimu wetu ambaye alikuwa ameanza kuchangia jana, ili aweze kumalizia sehemu ya mchango wake. Karibu sana mheshimiwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nikushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi hii kuweza kuichangia hoja hii. Mhe. Spika, ningependa niendelee tu kwa sababu kama nilivyoanza jana kama ulivyotamka na hoja zangu hizi.

Mhe. Spika, naomba nimuombe Mhe. Waziri kwa muda mrefu sana tumekuwa tunapiga kelele juu ya makazi bora ya vikosi vyetu. Mhe. Spika, mimi naomba nimuombe Mhe. Waziri kwa dhati kabisa, sote tunayafahamu makazi ya askari wetu hawa na hali yetu ya kiserikali ya kifedha kila mtu anaielewa, lakini ninachotaka kumuomba ni kutafuta njia mbadala ya kuweza kulisaidia suala hili ili tuweze kuwajengea makaazi mazuri askari wetu katika vikosi mbali mbali.

Mhe. Spika, chengine ambacho nataka nilizungumzie ni suala la mitaro iliyozunguka Manispaa ya Zanzibar. Mhe. Spika, Wazanzibari tumekuwa na utamaduni wa maradhi, tunajua kutengeneza lakini hatujui kukienzi tulichokitengeneza. Mhe. Spika, kama kuna jimbo ambalo limezungukwa na mitaro basi ni Jimbo la Kwahani. Kuna mtaro ulioanzia Mwembenjugu mpaka uwanja wa farasi, kuna mtaro wa Kibandahatari mpaka uwanja wa farasi, kuna mtaro wa Kassim Ali mpaka Muungano Msikitini, kuna mtaro nimeongezewa tena juzi Mhe. Spika, kutoka viwanja vya mpira kuelekea Sebleni kupitia mradi wetu wa *ZUSP*.

Sasa Mhe. Spika, ninachomuomba Mhe. Waziri aisimamie Taasisi ya Manispaa ili kuona kwamba mitaro iliyojengwa kwa gharama kubwa na serikali basi haiwachwi ikafikia pahala mpaka ikawa inaharibika na pasipo na ujenzi. Lakini cha kusikitisha kabisa ambapo Mhe. Waziri nataka nimuombe, tulipopata mradi wa *CAFEW* wa Ujerumani Uwanja wa Farasi kabla ya mradi ule tulikuwa na mtaro wa asili, mtaro ule Mhe. Spika, baada ya kujengwa mtaro mpya basi umedharauliwa na umeachwa na haufanyi kazi na inasemekana kwamba ujenzi wa Kariakoo ndio umesababisha mtaro ule usifanye kazi kabisa. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri apeleke timu ya wataalamu, kwa sababu mtaro uliojengwa wa ziada ulikuwa ni kusaidia kuondosha maji katika eneo la uwanja wa farasi, lakini tulipopata mtaro mpya mtaro wa mwanzo umeachwa. Waswahili wanasema na hata washairi walisema kwamba 'ukipata chungu kipya usitupe cha zamani'.

Mhe. Spika, sasa mtaro wa asili wa uwanja wa farasi umeziba, nimuombe Mhe. Waziri apeleke timu yake ya wataalamu wakaangalie njia mbadala ya kuweza kuunganisha mtaro wa zamani na mtaro mpya, tutafute njia ya kuunganisha kwa pamoja ili tuweze kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Kwahani katika kuondosha masuala ya maji na kuondosha maafa katika eneo lile. Sio vyema kwamba serikali inatumia pesa nyingi na gharama kubwa lakini baada ya kupata mradi wa *CAFEW* mradi wa mwanzo umeachwa na mtaro haufanyi kazi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mimi nataka nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Wakuu wa Mikoa, wenzangu walikuwa wakiwataja wa Mjini, Magharibi na wengine. Lakini mimi nataka nizungumze kwa jumla, Wakuu wa Mkoa wote wa Unguja na Pemba. Mhe. Spika, katika kipindi hiki tumeona namna Wakuu wetu wa Mkoa wanavyofanyakazi kwa nguvu kubwa na wamejitahidi kuleta mabadiliko katika maeneo mbali mbali, katika mikoa yao lakini pia na Wakuu wa Wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, mimi niwaombe tu kasi na *speed* waliyokuwa nayo wajitahidi kuiongeza, ili tuweze kuwaletea maendeleo wananchi wetu katika maeneo tofauti. Mhe. Spika, wenzangu walisema sana hapa, wengine walifika pahala kutetea, lakini kila mtu na uoni wake katika kuchangia. Walipiga kelele juu ya masuala ya madisko kuzuiliwa. Mhe. Spika, ni lazima tukiri katika kipindi cha karibuni nchi yetu ilikuwa tunafika pahala tunaelekea kubaya, utamaduni uhalisia wa Zanzibar ulikuwa unaanza kutoweka. Ulikuwa unaona tabu usije ukapata mgonjwa kuanzia saa 7 za usiku, ni aibu na fedheha kwa Wazanzibari. Kasi ya kuzuwia masuala haya ambayo yalikuwa hayastahiki katika nchi yetu, mimi naomba iendelee na tuwazuwie vijana wetu.

Mhe. Spika, kama kuna mtu ambaye alikuwa hapendi madisko haya basi mimi ni mmoja sipendi kabisa, kwa sababu nilikuwa napata tabu. Mhe. Spika, mim ni Rais wa Timu ya *Negro Sports Club*. Timu yangu kama ilikuwa ikicheza siku za Jumatatu au Jumanne nilikuwa napata tabu, kwa sababu vijana wangu walikuwa wanakwenda kufanya mambo ambayo hayastahiki, siku ya pili wanashindwa kucheza hata mechi taabani, inabidi nitumie muda wa kuwalaza sehemu kuwadhibiti ili kuondokana na masuala yale. Mapombe yalikuwa yanauzwa ovyo bila ya utaratibu. Sasa niwaombe Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wajitahidi kudhibiti suala hili, isipokuwa kwa wale ambao wamepata vibali, lakini pia pamoja na vibali vyao waendelee kufuata taratibu na kusikiliza silka na utamaduni wa Wazanzibari.

Mhe. Spika, mimi nina ombi kwa Mhe. Waziri, na ombi langu ni kwamba tumeshazowea sasa hivi kuwa masika hadi masika njia ya Mwanakwerekwe haipitiki. Sasa kwa kuwa serikali ilifanya jitihada ya kutengeneza *feederl road* kutoka Mwanakwerekwe kuendea Kwa Mchina, na imekuwa inasaidia sana wakati wa masika njia ile. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri katika mipango watakayoipanga halmashauri kuna njia imetoka Mwanakwerekwe inatokezea Magogoni, njia ile katika kipindi hiki wananchi walikuwa wanataka kuitumia lakini ilikuwa ikileta ugumu kabisa katika matumizi yake kutokana na hali halisi ya njia ile ilivyo.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri atowe kipaumbele kwa njia ile ili tuwe tuna njia mbili mbadala, tuwe na njia ambayo imeelekea Kwa Mchina, lakini tuwe na njia ya kutoka Mwanakwerekwe Makaburini kuelekea maeneo ya Magogoni, ili kuondosha mtafaruku katika njia zetu zile. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nichangie ni katika suala zima la mapato katika maeneo tofauti ya Manispaa yetu ya Zanzibar. Najua tunapiga kelele tunahitaji kutengenezewa maeneo yetu *feeder road*, *drainage* katika maeneo

yetu, lakini yote haya hayatoweza kutekelezeka kwa haraka pasipo na umakini katika masuala mazima ya ukusanyaji wa kodi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri ukusanyaji wa kodi katika manispaa zetu hauko makini, na tunapoteza fedha nyingi sana katika manispaa. Mhe. Spika, sisi ndio tunaotumia manispaa hizi katika maeneo mbali mbali, sisi ndio tunaokwenda masokoni, sisi ndio tunaegesha magari. Watu wengi hawapendi kuchukua risiti katika *parking*. Ukishatoa shilingi 1,000 unamwambia mtu basi mimi niachie niende zangu, sasa makusanyo hayapo, tuondoke katika uhalisia tuliokuwa nao, kwa sababu tumewaambia *ZRB* kwa kupitia kamati ya fedha, biashara na kilimo. Niombe waandae mikakati ya kuweka *electronic ticket*, nalo hili Mhe. Waziri liangalie linaweza likakusaidia, unaweza kuongeza mapato na ukaondosha yale maneno na makero ambayo tunakupigia kelele kila siku katika maeneo yetu tofauti. Manispaa ina fedha nyingi lakini bado umakini katika ukusanyaji wa kodi hauko vizuri.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, nimeangalia kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri, nimeangalia kitabu cha bajeti cha Wizara ya Fedha kitabu kikubwa, nimeona limegusiwa suala la michezo. Mhe. Spika, nchi yetu imebahatika, na nimshukuru sana Mhe. Rashid Ali Juma Waziri wa Habari, Utalii na Michezo, katika uongozi wake ni muda mfupi sana imehakikisha Zanzibar tumepata uwanachama wa *CAF*, na tunaelewa sasa hivi wizara yake inakwenda mbio ili kuhakikisha tunapata uanachama wa *FIFA*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri sana vikosi vyetu vyote hivi vina timu ambazo ziko *premier* timu ambazo zimekuwa tishio na timu ambazo zimekuwa ni kivutio kwa wanamichezo wa Zanzibar. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri tuandae mikakati ya kutosha mikakati madhubuti, tuandae mipango mizuri katika kuimarisha vilabu vyetu hivi, tulikuwa tunahangaika na vilabu hivi wakati hatupati kitu. Wizara ilikuwa inahangaika kutafuta fedha za kuendesha vilabu hivi lakini tunakoelekea tunategemea huenda tukaanza kupata ruzuku kupitia mashirikisho haya ya michezo duniani, sasa wakati tunaelekea huko ni vyema basi na sisi tukaandaa mikakati iliyokuwa mizuri kwa vijana wetu.

Lakini pia kumekuwa kuna tatizo kwa vilabu hivi Mhe. Waziri, matatizo ya masuala mazima ya kuendesha masuala mazima ya kuwapa nafasi katika uajiri wanamichezo hawa, mimi nakuomba uandae mipango mizuri vijana wanapochukuliwa katika vilabu ujue nani tunamuajiri nani tunampa mkataba wa muda. Kwa sababu unapomjengea matumaini mazuri mchezaji unamfanya atulie katika klabu lakini usipompa matumaini mazuri unamfanya akimbie katika klabu aende klabu nyengine na lengo ni kuviimarisha vikosi, sasa hivi nashukuru kwamba wanamichezo wengi wameanza kujitokeza timu za asili

zimeanza kuimarika na timu za asili zina uwezo na wameanza kupora wachezaji kupitia vikosi vyako Mhe. Waziri, sasa usipoandaa mikakati mizuri tutakuwa tunashiriki tu baada ya washindani na lengo letu vikosi vyetu Mhe. Waziri vishindane.

Lakini pia Mhe. Waziri basi niwaombe wakuu wa vikosi vinapocheza vilabu vyao wende wakawape moyo wanamichezo si vyema kamanda wa kikosi hujui hata ukiulizwa mchezaji wako namba sita nani humuelewi, timu yako leo imecheza matokeo yako vipi hujui. Nimpongeze sana kwa dhati kabisa Kamanda wa Polisi wa Traffic Kamanda Hassan Nassir haondoki Amani kutoa motisha wa timu zake, sasa niwaombe basi na makamanda wengine nao wafike Amani ili kuweza kutoa motisha kwa vijana wao, vijana wanapoona wakuu wao pale wamekaa wanapata ari ya kiuchezaji na kutoa ushindani uliokuwa wa hali ya juu.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa naomba sasa nimuite Mhe. Mwanaasha Khamis Mwenyekiti wetu, atafuatiwa na Mhe. Zulfa Mmaka Omar na Mhe. Miraji Khamis Mussa ajiandae. Mhe. Mwanaasha karibu.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache katika hotuba ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwanza kabisa na mimi niungane na wachangiaji wote kwa kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wote katika Wizara hii katika kuwasilisha hotuba hii nawapongeza sana.

Lakini mimi nije moja kwa moja katika mchango wangu Mhe. Spika, katika ukurasa wa 12 program ya usimamizi wa utumishi wa Idara Maalum za SMZ kifungu cha 26, nimeona katika program hii kuna Tume ya Utumishi ambayo inashughulikia mambo ya utumishi katika program hiyo, kwa hivyo mimi nilikuwa na suali tu nilikuwa nataka kujua ni Watumishi wangapi ambao wamepandishwa vyeo katika Idara hii au katika program hii. Lakini la pili pia nilitaka kujua Mhe. Spika, ni wanawake wangapi na wanaume wangapi ambao wamepandishwa cheo.

Lakini niendelee na ukurasa wa 14 Mhe. Spika, katika program za idara maalum za SMZ kwenye jeshi la Kujenga Uchumi, kwanza niipongeze sana

Idara hii kwa kuona kuwa kwa kuanzisha *program* hii ya kuwachukua vijana katika kuwafundisha kazi za amali, kutoa mafunzo kwa kuwajengea uwezo vijana hao ili waweze kujitegemea katika mambo mbali mbali ya kiuchumi waondokane na utegemezi. Lakini Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja anipe majibu katika *program* hii ya kuwajengea vijana uwezo nimeona katika viashiria vya matokeo ni vijana 400 ambao wamejengewa uwezo na nina imani watakuwa wako vizuri. Swali langu lipo hapa nilitaka kujua baada ya kuwajengea ule uwezo Mhe. Spika, vijana wale tayari wameshajengewa uwezo nilitaka nijue tu kuna utaratibu gani wa kuwapatia nyenzo baada ya kumaliza mafunzo yale.

Mhe. Spika, nije ukurasa wa 18 katika *Program* ya Chuo cha Mafunzo niwapongeze sana, nawapongeza sana Mhe. Waziri kwa kutoa mafunzo ya wapiganaji wetu na katika program hii imezingatia katika kuwapa mafunzo ya stashahada pamoja na shahada na uzamili, lakini nilitaka nijue katika hizi shahada zilizotolewa katika program hii ni shahada ama ni katika fani gani ambazo wamewapatia mafunzo wapiganaji hawa. Lakini vile vile nataka nijue katika fani hizo hizo wanawake wangapi na wanaume wangapi ambao wamepatiwa mafunzo hayo, lakini katika hesabu niliyoifanya hapa wamesema katika hiki kitabu kuna wafanyakazi wawili wanasoma shahada za uzamili, 9 wanasoma shahada ya kwanza, na stashahada 17 na Cheti 31.

Mhe. Spika, nilitaka kujua katika hisabu niliyoifanya hawa watakuwa karibu wafanyakazi 58 kama sikosei je katika utendaji ni nzuri niwapongeze ni nzuri kwa maendeleo lakini katika utendaji kwa mwaka mzima kuwaondosha wafanyakazi hawa haijaathiri utendaji wa kazi katika vitengo hivyo ambavyo amewatoa hao wapiganaji. Lakini pia nilitaka kujua ni kiasi gani cha fedha kilichotumika kuwapatia wafanyakazi hawa katika mafunzo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nilikuwa nataka kujua katika *program* za mikoa dhana ya utekelezaji wa madaraka kwa wananchi, kifungu cha 63. Mhe. Spika, niwapongeze sana najua kwa matokeo ambayo katika kifungu hichi kimeeleza kuna matokeo yanayotarajiwa katika kupatikana katika kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji, kuanzia namba moja (i) hadi (v) maelezo hayo yapo, lakini nilitaka nijue Mhe. Spika, kupitia Waziri ni mikakati gani tayari tuna matarajio ya kupatikana katika miaka mitatu. Lakini ni mpango gani mikakati ambayo wameipanga kabla ya matokeo yanayotarajiwa, katika kitabu hichi sijaona ile mipango mikakati ambayo wameipanga kuhusiana na matokeo yanayotarajiwa.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nina hayo lakini pia nilikuwa nataka nizungumze suala la maslahi kwa wafanyakazi au watendaji wa idara hiyo, kwanza nimshukuru sana Mhe. Rais katika kuwapatia watumishi wote wa kima cha chini kwa ongezeko la mshahara nina imani na watendaji hawa au wafanyakazi wa vikosi na wao wamefaidika na hili. Lakini hapa nilitaka kujua kidogo kuhusiana na suala zima la maposho ya likizo kwa wafanyakazi hawa, kwa sababu nahisi bado kuna malalamiko kidogo kwa watendaji au wafanyakazi hawa kuhusiana na maposho ya likizo. Kwa hivyo nilitaka nijue hili liko je katika kuwapatia maslahi wafanyakazi hao.

Mhe. Spika, kwa hayo machache ambayo na mimi nimeona niyachangie namshukuru sana Mhe. Waziri, lakini pia najua sigusi kwenye barabara kwa sababu najua watashirikiana na Mhe, Gavu katika kuitengeneza ile barabara ya Chukwani ambayo juzi niliizungumza. Kwa hivyo naunga mkono hoja kwa asilimia mia Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Asante sana Mhe. Mwanaasha waheshimiwa Wajumbe nilimtaja Mhe. Zulfa lakini nilisahau jana alishachangia kwa hivyo ninakwenda moja kwa moja kwa Mhe. Miraji Khamis Mussa, naona nae simuoni naomba sasa nimwite Mhe. Viwe Khamis atafuatiwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) ajiandae.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii ya leo kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ,

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii ya Wizara yake, nichukue nafasi hii nimpongeze Naibu Waziri, nichukue nafasi hii niwape pole wananchi wote wa Zanzibar ambao wamepata maafa katika kipindi hichi cha mvua za masika, pia niwape pole wananchi wa Nyarugusu, Kinuni pamoja na Pangawe ambao walipata kimbunga kikali juzi na kuweza kuharibu maeneo mengi katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, nianze na mchango wangu kwenye ukurasa wa 9 kuna wafanyakazi ambao wamepatiwa mafunzo wafanyakazi 11 wanaendelea na masomo yao katika fani za usimamizi wa rasilimali watu, uhasibu, utunzaji wa kumbukumbu, ununuzi na ugavi. Nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja anipatie maelezo ni wanawake wangapi katika wafanyakazi hawa 11 ambao wamepatiwa masomo hayo au wanaoendelea na masomo hayo ya fani mbali mbali.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa 12 kuna vijana ambao wameandikishwa katika kujiendeleza na JKU kwenye mwaka huu wa 2017. Ni kweli vijana wetu huwa wanajiandikisha na JKU kwa kila mwaka, lakini vijana hawa wanapokuwepo JKU wanajituma kwenye fani mbali mbali. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje aniambie ni sababu gani ambazo zinapelekea vijana hawa zinapotokea nafasi za ajira wakawa hawachukuliwi na wanachukuliwa vijana ambao wapo nje na kambi hizi za JKU. Kuna vijana wetu wanatulalamikia wapo JKU wanafika miaka mitatu mpaka mitano zinapotokea nafasi za ajira vijana hawa huwa hawachukuliwi wanaambiwa eti miaka yao imeshakuwa mingi. Je ile miaka ambayo walikuwa wanaitumikia kule JKU ilikuwa inasaidia nini au ilikuwa dhamira yao ni kitu gani namuomba Mhe. Waziri atakapo kuja aje kunipa maelezo ya kina kuhusu suala hili la vijana wetu ambao wanapoteza nguvu kazi zao miaka mitatu mpaka mitano, zinapotokea nafasi za ajira wanasahauliwa kabisa.

Mhe. Spika, niende kwenye kurasa wa 26 vita dhidi ya dawa za kulevya, kuna watu 24 ambao wamekamatwa na madawa haya ya kulevya katika Unguja na Pemba na hasa Mkoa wa Mjini Magharibi, lakini tumeambiwa wamekamatwa na kesi zao ziko kwenye Afisi ya DPP. Lakini cha kusikitisha kwa vijana hawa au watuhumiwa hawa ambao wamekamatwa wasiorodheshwe na majina yao, kila siku tunasikia watu kesi hizi zimekamatwa kwa madawa ya kulevya au wanahusika na madawa ya kulevya lakini bado tu tunasikia hadithi. Tunataka sasa hivi mtu yoyote ambae kuwa atashtumiwa au atakamatwa na madawa ya kulevya basi waorodheshwe mpaka majina yao na watangazwe kwenye vyombo vya habari, ili jamii wajue hasa kama hawa ndio wanaoharibu vijana wetu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika Mkoa wa Kaskazini Pemba, kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa jinsi anavyoisimamia ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na utekelezaji wake. Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Pemba imetekeleza shughuli mbali mbali za maendeleo katika mkoa wake, pamoja na kuwa imeonekana katika mkoa huu wa Kaskazini Pemba umeshuka katika kuongeza kipato katika makusanyo yao ambayo walilenga kukusanya kwenye mwaka 2016/2017. Lakini niwapongeze sana wametekeleza miradi mbali mbali, wamejenga vituo vya afya, wamejenga maskuli.

Mhe. Spika, niipongeze Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imetekeleza miradi ya maendeleo mbali mbali katika Mkoa huu wa Kaskazini Pemba, imejenga ujenzi wa soko la samaki Njuguni pia katika kusaidia miradi ya elimu mabanda katika kijiji cha Msuka Jengo la elimu ya maandalizi,

Halmashauri hii ya Wilaya ya Micheweni tayari wameshajenga jengo lao katika Wilaya hii ya Micheweni na tayari limeshaezekwa lakini mpaka sasa hivi jengo hili tunaliona bado halijaingizwa milango wala madirisha, sakafu pia bado. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje aniambie kwa nini jengo hili mpaka sasa hivi bado liko vile vile, je, jengo linaachiwa Halmashauri yenyewe ya Wilaya au Wizara yenyewe ndio wanamalizia pale ambapo pamebakia.

Mhe. Spika, tatizo la vyeti vya kuzaliwa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba bado lipo na linaendelea, cheti cha kuzaliwa kinafika mwaka mzima mtoto cheti kile bado hakijapatikana. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri suala hili vyeti vya kuzaliwa walishughulikie kwa kina, kwa sababu linazorotesha na linasababisha kuwa wananchi wetu kila siku wanapangiwa tarehe wanatoka na kwenda lakini wakifika kule wanarudi mikono mitupu. Kwa hivyo Mhe. Waziri suala hili wizara yako walisimamie kwa kina ili uonekane utekelezaji huu unatekelezwa kwa wakati.

Mhe. Spika, mwisho niende kwenye suala la kupambana na udhalilishaji wa kijinsia ni kweli suala hili la kupambana na udhalilishaji wa kijinsia lipo na linaendelea, lakini kwenye kitabu hichi tumeona mabilioni ambayo yapo yanataka kupitishwa na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika mwaka huu 2017/2018, tukiangalia kuna hizi kesi ambazo zipo na kesi hizi tatizo kubwa ambalo lipo katika nchi yetu ni chombo cha DNA, basi katika pesa hizi ambazo zinataka kununuliwa hizi camera ziingie kwenye chombo hichi cha DNA ili washirikiane na Wizara ya Afya waweze kununua chombo hichi, ili tatizo hili liweze kuondoka. Malalamiko makubwa tunaambiwa kwamba hakuna ushahidi, sijui kunatakiwa ushahidi gani. Sasa wakati wa kupatikana ushahidi umefika Wizara hii washirikiane na Wizara ya Afya na pesa hizi zihamishwe ili ziweze kununuliwa chombo hichi cha DNA.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naunga mkono hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri asilimia mia.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Viwe Khamis Abdalla, anayefuata ya Mohamed Said Mohamed (Dimwa) ambaye simuoni, badala yake nafasi hiyo nitampa Mhe. Hassan Khamis Hafidh dakika tano tu lakini achangie halafu atafuatia Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya dakika tano asubuhi hii ili nichangie bajeti hii muhimu ya Idara Maalum na Vikosi vya SMZ. Nutaanza na Mfuko wa Barabara.

Mhe. Spika, kwanza nampongeza sana Waziri wa Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri kwa kututengenezea *feeder road* zile barabara za ndani. Namuomba Mhe. Waziri anapozitengeneza hizi barabara afanye utafiti wa kujua barabara gani zinahitaji kutengenezwa. Nimegundua barabara zinazotengenezwa hazihitaji kutengenezwa kwa sababu zipo mjini. Barabara ya Kikwajuni, barabara ya Mitiulaya, tunaacha barabara za Magharibi, Welezo na kwengineko ambapo kunahitaji kweli barabara kutengenezwa kwani mama zetu, dada zetu, watoto wetu, wanazalia majumbani kwa sababu mabarabara hayapitiki.

Mhe. Spika, ombi langu kwa Mhe. Waziri safari hii Mfuko wa bajeti ya barabara uangalie Magharibi kuna barabara ya Mhe. Rais aliyeiwekea ahadi ya Welezo ya Hawai haijatengenezwa. Naomba sana Mhe. Waziri aangalie barabara ya Welezo na Magharibi yote kwa sababu ndizo zenye shida, mbali na mji, mbali na huduma muhimu kama hospitali na nyenginezo. Wale Mjini wanapata kila kitu na wapo karibu na huduma muhimu.

Mhe. Spika, pili nawapongeza Wakuu wa Wilaya wanafanya kazi nzuri sana isipokuwa hawana vipando vinavyostahiki na wala afisi zao hazistahiki na vyeo vyao. Wakuu wa Wilaya wanakuwa kama Maraisi wa Wilaya zao lakini vipando vyao haviridhishi, maslahi yao hayaridhishi, naomba sana mambo haya yazingatiwe.

Mhe. Spika, vikosi vya SMZ nawapongeza sana makamanda wote na wapiganaji wote wa Vikosi vya SMZ. Naomba kusema wapiganaji wa vikosi hasa wa ngazi za chini wanatuletea malalamiko kila siku, wanasema kwamba pesa zao zinakatwa, sijui zinakatwa vipi, sijui za chakula, au ni za nini, wanatuletea mambo chungumzima. Naomba sana hili suala lizingatiwe kwa sababu linatutilia aibu makamanda wetu wanalalamika na wanafanya kazi nzuri ya kulinda ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nakwenda katika ukurasa wa 77 katika kitabu cha bajeti ambacho kina kamera. Naomba kujibiwa. Mhe. Spika, kulitengwa bilioni 18 zimepatikana bilioni 13 nataka kujua bilioni 13 zimefanyiwa nini, na hii bilioni 5 itapatikana au haipatikani. Nataka kujua hizi kamera zilizofungwa Zanzibar zina *warrant*, zina *insurance*, kwa muda gani na kama zitaharibika kwa kipindi gani kampuni iliyofunga kamera itatulipa au itakuja kutuwekea. Nataka kujua umadhubuti wa zile zana zinazotumika katika kufungia kamera, lakini pia nataka kujua *break down* ya bilioni 20 zinazoombwa.

Mhe. Mwenyekiti, nina wasiwasi bilioni 18 zimeshaombwa, bilioni 13 zimepatikana, bilioni 20 tena, mradi huu haupungui pesa zinazidi tu. Pia

ukiangalia ukweli kwamba nchi yetu masikini tunahitaji kamera lakini ni lazima tujiulize ni kamera au pesa hizi bilioni 20 kwa sababu tuna matatizo mengi Mnazi Mmoja tuzipeleke Mnazi Mmoja, ambapo kuna matatizo mengi na makubwa. Sikatai binaadamu unapotononoka unahitaji kulindwa kwanza kwa panga, lakini baadaye unahitaji kulindwa kwa kamera sio tatizo, tunahitaji kamera lakini lipi tunahitaji zaidi, *between* kuimarisha Mnazi Mmoja tunapokufa bila ya sababu au kamera kwa muda huu. Hilo nataka kuja kujibiwa.

Mhe. Spika, nampongeza sana Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini kaka yangu Hassan Nassor, Mkoa wa Mjini uko salama na kwa Makamanda wote wa Polisi wa Mikoa. Lakini naomba sana waendelee kulinda mikoa hii. Mwisho nawapongeza sana wapiganaji wa jeshi la KMKM wanahospitali nzuri, naiomba serikali namuomba Mhe. Waziri hospitali hiii aitizame kwa jicho la huruma, ni hospitali nzuri, inatoa huduma nzuri lakin vifaa haina, madawa haina, lakini inafanya kazi nzuri ya kuwahudumia Makamanda wetu pamoja na wananchi wetu.

Mhe. Spika, swali langu kubwa ninalotaka kujibiwa kuhusu kunako camera. Kama maelezo yatanitosha sitozuia fungu, lakini kama maelezo hayatonitosha nitawaomba na wenzangu fungu hili tulipeleke Mnazi Mmoja tukaimarishe hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kipindi hichi, kwa sababu tunahitaji sana kuimarisha hospitali ili tuishi vizuri kwa sababu pale ndio kimbilio la wakwezi na wakulima.

Baada ya hayo machache naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sasa naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) atafuatiwa na Mhe. Ussi Yahya Haji.

Mhe. Ali Suleima Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kuichangia Wizara hii ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum kwa bajeti ya mwaka 2017/18.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote pamoja na viongozi Wakuu wa vikosi vyetu lakini pia na wapiganaji wetu wote kwa kazi mbali mbali ambazo wanazifanya na kulinda nchi yetu, mali zetu na kuhakikisha kwamba tunaishi katika amani na utulivu.

Mhe. Spika, kwanza niseme tu mimi bajeti hii sina matatizo nayo lakini nitatoa maelezo ambayo nitamuomba sana Mhe. Waziri ayazingatie kwa maslahi ya nchi yetu na hasa tukizingatia Wizara hii ndio Wizara mama ambayo tunayategemea katika nchi yetu.

Nakuja kwanza katika nyongeza za mishahara kwa vikosi vyetu vya SMZ. Mhe. Spika, kwa dhati kabisa nampongeza Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ahadi yake kubwa, kasema kwamba vikosi vyetu vinalingana na vikosi vya Tanzania Bara. Niseme maaskari wengi na kwa kuwa na mimi natokea katika fani hiyo wamenifata na wamesema kwamba nitoe salamu rasmi za kumpongeza Mhe. Rais kwa ahadi yake ambayo kaitekeleza kwa asilimia mia moja. Pili katika maelezo yaliyoelezwa hapa kwa Waheshimiwa wenzetu wengi waliotangulia walisemea suala la SST kamera.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wote waliosema hili liangaliwe upya, fedha zake ziende katika maeneo nitakayoyataja kwa ushauri ambao utakaoleta tija kwa wananchi wetu. Kwanza tutizame hali ya maisha ya unyanyasaji unaotokea katika nchi yetu na watoto wetu ambao wanadhalilika siku hadi siku. Naomba DNA mashine inunuliwe ili iondoe adha hii. Ushahidi mara nyingi unapotea haupatikani kwa tendo baya na chafu, lakini maudhi yake ni hatari kwa maisha ya vijana wetu siku hadi siku. Naiomba Wizara iliangalie hili.

Pili Mhe. Spika, niseme tu kwamba fedha hizi ni nyingi na fedha hizi zitatusaidia majimboni. Mimi nalilia sana maisha yangu katika jimbo langu Kijitoupele pamoja na majimbo ya Wenzangu, Mkoa wa Magharibi, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Pemba kusinii, Pemba Kaskazini, mjini sisemi sana afadhali kidogo lakini pia unamatatizo baadhi ya maeneo ni vyema fedha hizi zipelekwe kwenye mradi wa maji kuondoa matatizo katika majimbo yetu. Serikali zetu za Wilaya wamekabidhiwa fedha hizi wasipewe Waheshimiwa Wawakilishi wala Wabunge mikononi, isimamiwe na sisi tushiriki ili kuhakikisha matatizo ya maji yanaondoka katika maeneo yetu. Niseme katika jimbo langu la Kijitoupele bado nalilia sana tatizo la maji asilimia 60 au 55 ndio wanaopata maji, asilimia 45 hawana maji. Hiyo ni hatari katika maisha yao.

Mhe. Spika, jengine nitazungumzia suala la barabara zetu za ndani kama wenzangu walivyosema, kila mmoja analia upande wake, mimi niishukuru serikali kwa kuangalia hili na kusema tu kwamba hivi sasa hivi kuna mpango mkubwa ambao tukiupata huo itatundolewa matatizo katika mambo yetu mengi tu katika njia zetu, Serikali ya Wilaya ikiangalia kuzitekeleza kupitia Manispaa

zetu. Mimi niseme nina barabara kama tano ni adha katika jimbo langu, kwanza njia ya Taveta kuelekea magirisi mpaka, sipendi kuliita hilo jina lakini nitaliita kama linavyoitwa sio kwa kuwadhalilisha wananchi lakini ndio jina lake yaani kwa walevi. Tomondo kwa Walevi hilo ni jina linakubalika kama ninavyoitwa Shihata nalikubali.

Mhe. Spika hiyo ni njia ambayo ina maudhi ...

Mhe. Spika: Mhe. Shihata umeshachangia kama dakika 5 naomba usubiri kidogo nimpishe Mwenyekiti, halafu utaendelea. Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee Mhe. Shihata.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naendelea na barabara yangu ya Taveta Magirisi hadi Tomondo kwa Walevi, naomba barabara hii ifanyiwa matengenezo kwani wananchi wetu wanapata shida. Barabara nyengine ya Meli Nne Uzi, barabra hii ni muhimu hasa siku za mvua zinapotokea watu wengi huwa wanaitumia, naomba barabara hii iangaliwe ya Melinne Uzi mpaka Melinne Tomondo, hii ni barabara muhimu na inatumika na watu wengi, inatokea mpaka Kwarara njia kuu naomba na hii iangaliwe.

Barabara nyengine Mshelishelini, naweza kusema viwanja vya magereza kutokea Mshelishelini hadi Tomondo kwa mbele na hii pia iangaliwe. Matatizo mengine ninayoyapata namuomba sana Mhe. Waziri mara nyingi humwambia lakini tukishakuzungumza hapa inakuwa wakati mwengine imekwisha kwa kuwa ana watendaji wake nitamuomba sana Mhe. Waziri tushirikiane matatizo yanayotokea mafuriko katika jimbo langu mimi la Kijitoupele ni tatizo kubwa la mitaro ya maji.

Mhe. Mwenyekiti, wewe tumeungana katika mipaka yetu tunapata shida sana kutoka nyumba mbili maji yanayoelekea Ziwa Maboga, huu ni mtaro wenye matatizo na ni mtaro unaoleta maafa yasiyotabirika. Ningeiomba serikali kuliangalia hili kupitia taasisi zinazohusika kwa sababu mtaro huo ni mkubwa pamoja na michango mbali mbali ya Mhe. Mbunge, Mhe. Mwakilishi ambaye ni mimi mwenyewe, kushirikiana na Manispaa yetu ya Zanzibar, tumejitahidi kidogo lakini mradi wa ujenzi wa mtaro huu kama haikuingia Serikali Kuu hatuumiliki na hatuuwezi. Naomba hili tuliangalie na yote yaliyotakiwa pamoja na maarifa mazuri aliyoyatoa Mhe. Rais juzi kupitia Wizara ya Ujenzi, naamini likiondoka tatizo la mtaro huu kutainuliwa na kuelekezwa kunakoelekea basi maafa yataondoka katika maeneo yetu na watu kuhama hama katika majumba yao siku za mvua.

Mhe. Spika, jengine mtaro huu uko katika daraja la Kwashunda naliacha tunakwenda Meli nne Uzi na hili ni daraja na mtaro mkubwa unaelekea huko huko Ziwa Maboga yaani uko mpakani kwetu baina ya Mhe. Mwenyekiti, aliyekaa kwenye kiti Mhe. Mwanaasha na mimi Mhe. Mwakilishi wa jimbo la Kijitoupele tumepakana na adha hiyo inatukuta pamoja, huu nao uangaliwe ili tuhakikishe kwamba unaondoa maafa na kuleta manusura kwa wananchi wetu wanaoishi katika nyumba zao hizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine niseme tu kwamba katika kitabu hichi kuna ukurasa wa 81 Wizara ya Afya kuna maelezo mengi yameelezwa. Baraza la Magharibi 'A' na 'B' hapa kidogo mimi ningeomba nije nipate maelezo. Magharibi 'A'na 'B'manispaa zetu hizo au Wilaya kuna fedha ambazo zimeombwa pamoja na mfuko wa *Basket fund* milioni mia tano na ishiri na moja milioni, thamanini elfu mia mbili na ishirini na saba na senti hamsini na nane (Sh. 521,080,227.58) Mimi nitaomba sana hizi fedha zina Manispaa mbili. Huku kwengine zilipokwenda zote moja moja nije nipewe mchanganuo wa fedha hizi, Magharibi 'B' wanapata kiasi gani na Magharibi 'A' wanapata kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa wengine tumeshajitayarisha wananchi wetu wanapata shida ya kwenda hospitali mbali mbali. Kwa mfao sisi jimbo la Kijitoupele tumebahatika Mhe. Sereweji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo na Mhe. Shamsi wakati huo Mbunge, wamejenga hospitali katika eneo la Magirizi Taveta. Mimi niliwaahidi wananchi wangu kwamba mkinipa ridhaa yenu nitahakikisha nalimaliza plasta, milango na madirisha. Mhe. Mwenyekiti, naweza kutoa kauli nzuri kwa Wizara ya Afya kwamba sasa hivi nimefikia asilimia nzuri, plasta nje na ndani tayari, madirisha yote tayari. Sifichi mimi nakuwa muwazi, nimeweza kumiliki mlango wa mbele na wanyuma bado *hard board* na milango ya ndani na *tiles.*

Mhe. Mwenyekiti, naiomba Wizara inayohusika au kupitia manispaa zetu wamalize *tiles* chini, *hard board* juu, *fiting* ya umeme nimefanya ili wananchi wetu wa Jimbo la Kijitoupele wafaidike katika hospitali hiyo tuna asilimia kubwa ya wananchi wetu wa Kwarara, Kijitoupele, Tomondo, Wapangawe Jirani na Meli Nne wanaweza kuja kutumia hospitali hii. Kwanza itakuwa akina mama zetu wanapata kuendesha mipango ya uzazi, watazalishwa hapo hapo. Naiomba sana Wizara au taasisi inayohusika ifanye haraka. Mimi naomba kazi hii ikifanyika mapema basi tutapata manufaa kwa wananchi wetu hawa.

Mhe. Mwenyekiti nije katika mikoa yetu, mimi nawapongeza Wakuu wa Mikoa wote, nawapongeza Wakuu wa Wilaya wote, Makatibu Tawala wote na

wafanyakazi wote wa Wilaya na Mikoa, hasa tukiangalia kwamba wanafanya kazi nzuri, wanajitahidi kwa pale wanapoweza linapotokezea tatizo wameshafika. Ule ndio utekelezaji ambao unaotakiwa linapotokea tatizo ufike. Ningeomba sana wakapata ushauri au wakawa na vikao maalum vya mara kwa mara na viongozi Wabunge na Wawakilishi ili tukabadilisha mawazo na kuweza kuona upande fulani kuna tatizo ili tulivamie liondoke tatizo lile lisiendelee.

Mhe. Mwenyekiti, nawapa pongezi hizo kwa dhati kabisa na nawapongeza kwa moyo mkunjufu kutokana na huduma za kazi zao. Ushauri wangu kwa kuwa Mkoa wa Mjini Magharibi ni mkoa mama una Manispaa Tatu hivi sasa. Iliachwa mali wakati huo tulikuwa na Baraza la Manispaa peke yake la Mjini lakini sasa hivi kuna Magharibi 'A' na 'B' Mhe. Masoud jana alitoa rai na mimi naitoa rai hiyo ili kuongezea. Naiomba Wizara inayohusika na mambo ya magari ya kuzolea taka wapewe wenzetu na wao kama kuna mgao wa magari manane basi manne wapewe mjini mawili yaende kwenye Magharibi, wanapata shida sana na taka nyingi sana zipo Magharibi kuliko Mjini wakati mwengine.

Mhe. Mwenyekiti jengine makontena ya kuwekea taka naiomba tena Serikali kupitia Wizara inayohusika iangalie kupitia Manispaa yote wamemiliki wao Mjini na huko Magharibi tuna shida nayo 'A' na 'B' nayo tuletewe ili kuweka mji wetu safi.

Mara nyingi Mhe. Mwenyekiti yanapotokea maafa ya maradhi ya mripuko yanaanzia katika maeneo yetu ya magharibi, mjini huwa mwisho. Lakini pia Mheshimiwa hupenda kusema ukweli, si vyema kwanza kila zuri linalokuja lipelekwe mjini, huku magharibi kuna nini au katika majimbo ya wenzetu Mikoa ya wenzetu Kusini Pemba, Kusini Unguja, Kaskazini Pemba na Unguja hawayapati yale wanayopata mjini. Naomba Serikali kwa makusudi tuangalie kinachofaa katika nchi yetu nzima vilivyo ili kuondoa manung'uniko ambayo yanajitokeza.

Mhe, Mwenyekiti, nakuja kuzungumzia suala la kinamama askari wa KMKM. Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Wizara yaWanawake na Watoto bora niseme moja kwa moja hivyo panapo tokea udhalilishaji wa watoto wetu siko tayari mimi kusikia neno nikanyamaza, halafu kina mama nao kusikia pana manung'iniko ya kudhalilishwa wakati mwengine pia si vyema kunyamaza. Naiomba Wizara kupitia vikosi vyetu vizuri ambavyo nimevipongeza KMKM, wanafanya kazi vizuri pamoja na vikosi vyote tena nawapongeza usiku na mchana kwa sababu Mhe. nimetoka huko huko askari.

Askari anapoteza muda wake kukulinda wewe mwananchi na mali zetu kwa hivyo kuna kipindi anafikia wakati anasema na mimi sasa hivi kama kaolewa ni muda wake katika kazi umefikia kuolewa ni haki yake ya msingi aolewe na mwanamme vile vile na askari wa kiume ana muda maalum hatakiwi afanye uhuni uhuni lakini akifikia muda wa kuoa na aoe apumzike. Sasa Mheshimiwa nasikitika sana tatizo hili lililojitokeza kwamba askari hawa wa kike wamefikia muda wa kuolewa na wameolewa lakini mambo mawili yanatokea mtu akioa anategemea yule anayemuoa apate mtoto. Mwenyezi Mungu akiwa hakumpa si tatizo lakini bado ni haki yake na kwa njia yoyote atafute mtoto kwa tendo ambalo linakubalika.

Sasa si vyema kusema kwamba askari huyu kafanya tendo fulani ambalo ni la halali kabisa kachukua ujauzito anaambiwa huyu hafai au aondoshwe kwa sababu kachukua ujauzito hilo ni kosa na halikubaliki? Naiomba Serikali kupitia Wizara hii askari wetu hawa warejeshwe kazini, tena warejeshwe na nia njema kabisa na kama walisumbuliwa muda wa miezi mitatu, minne, mitano huko nyuma mafao yao pia yalipwe.

Mhe. Mwenyekiti, haya mengine hayasemeki ni jambo ambalo la kusikitisha kwa hivyo mimi ningeomba hilo Mheshimiwa liangaliwe na nitasimama kidete katika kifungu hiki au kama hakipo lakini hili nililolitoa wazo kama sikupata maelezo mazuri naizua shilingi katika suala hili mpaka nijuwe mwisho. Kwa sababu huu ni udhalilishaji na kule kwenye KMKM nitauzuwia shilingi nijue maelezo mazuri juu ya kurejeshwa askari wetu hawa ambao wamo katika sheria na halali ya ndoa zao na baada ya kupata ujauzito wakaachishwa hili sitokubali na sheria nikiitoa kauli hapa sina tabia ya kupiga buti buti wala sina tabia lakini linaloleta matatizo kwa jamii lazima tuletee kwa nguvu zetu zote ili kutoa haki kwa inayofaa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la masoko mawili nitaayazungumzia Manispaa.....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Shihata una dakika mbili naomba umalizie.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Haya Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo masoko ya Mwanakwerekwe na Soko letu la Mboga mboga hapa Mombasa.

Mhe. Mwenyekiti, nakiri kwamba masoko haya yako chini ya Baraza la Manispaa mjini lakini wakati huo lilikuwa Mkoa wa Mjini Magharibi nataka kutoa rai Mheshimiwa ikiwa Manispaa ya Mjini wakati huo ilikuwa peke yake sasa hivi imezaa Manispaa mbili tujuwe kinachopatikana kinagawia namna gani. Manispaa yetu ya Magharibi 'B' ndio mali yake sasa hivi huku 'B'

nazungumzia 'B' sasa hivi ndio nyumbani, faida yake inapatikana vipi na wanalipwa namna gani naomba nije kupata maelezo mazuri kwa sababu wenzetu hawa wanashida nyingi, wanafanya kazi nyingi kucha tunalalamikia mitaro yetu mibovu, pa kutupia mataka hatuna gari lao bovu wanalo moja tu. Kwa hivyo naomba tupate maelezo hayo na kama yataridhisha sina matatizo na kama hayakuridhisha nitatoa ushauri.

La mwisho pamoja na kusema nitazuia kifungu kama sikupata majibu mazuri lakini natamka rasmi kwamba naiunga mkono taarifa hii ya bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Idara Maalum lakini nije kupata maelezo mazuri ili niunge mkono kwa asilimia mia moja sina tatizo. Mheshimiwa naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Shihata wa Jimbo la Kijitoupele sasa namwita Mhe. Ussi Yahya na Mhe. Miraji ajitayarishe na Mhe. Khadija Omar Kibano wa Jimbo la Mtambwe naye ajiandae.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Mwenyekiti, kwanza awali ya yote nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Ndugu yangu Ahmada Yahya Abdulwakil kwa kupata uteuzi wa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na ameapishwa leo hapa.

Pili, namshukuru Rais ambaye ndio muhimili wa wizara hii kwa uvumilivu, ushupavu na imani anayowaonesha wananchi wa Zanzibar Unguja na Pemba. Pili nimshukuru Waziri wa wizara hii pamoja na watendaji wake wote tukianza Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu na Wakurugenzi pamoja na Wakuu wa Wilaya na Mikoa na Maafisa Tawala namna walivyoshikamana kwa kuiongoza Wizara hii na kuweza kupata utulivu wa visiwa vya Unguja na Pemba nawashukuru kwa dhati kabisa.

Tatu niwashukuru Viongozi wa Vikosi Kikosi cha KMKM, JKU, Valantia pamoja na Zimamoto na kikosi cha Chuo cha Mafunzo kwa namna wanavyohimili kutekeza na kufanyakazi kwa juhudi na maarifa mpaka tukawa tuna utulivu wa visiwa vya Unguja na Pemba.

Halafu Mhe. Mwenyekiti mimi nitazungumzia zaidi Mkoa wa Mjini Magharibi. Mhe. Mwenyekiti, takwimu zinaonesha Mkoa wa Mjini Magharibi una asilimia 46 ya wananchi wa Unguja na Pemba na hii ni takwimu ya sensa ya 2012 leo tuna 2017. Sasa naiomba Wizara pamoja na Serikali kuu kuliangalia sana suala hili kwa sababu kama 2012 Mkoa wa Mjini Magharibi una asilimia 46 ya *population* ya Zanzibar hapo pana tatizo Waziri aje atueleze *population* hii

inazidi kwa kuzaa, *population* hii inazidi kwa kuhamia, *population* hii inazidi kwa nini? Kwa sababu kama tutaiachia tu *population* kuzidi tu tutaupa mzigo mkubwa sana Mkoa wa Mjini Magharibi na wakati wote tutakuwa na matatizo ya huduma ambazo ziko katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa mfano juzi wananchi walilalamika wa hospitali ya Chumbuni kwamba wao wako wengi kabisa kutwa nzima wako kama watu mia tatu mia nne wanaotaka huduma pale na madaktari hawana.

Sasa hiyo haitokei kwa kituo cha afya tu pengine katika maskuli tutapata matatizo kwa hivyo Mkoa huu uangaliwe maalum, Serikali ikae Mkoa huu una *burden* kubwa na kwa kweli tumshukuru sana Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi katika kuhimili hayo. Kwa sababu kama ni 46 kwa 100 *population* hiyo iko hapa ina maana kuna wananchi 598,000 kwa sensa ya 2012 Mikoa mengine yote ina wananchi 702,000 kwa hivyo kama 46 kwa 100 iko katika Mkoa wa Mjini Magharini naiomba Wizara ije itueleza at *least* tupate *awareness* katika mikoa mengine kuna *percentage* ngapi kama Mjini Magharibi 46 kwa 100 Mkoa wa Kaskazini una arubaini na ngapi una *percentage* gani, Mkoa wa Kusini Pemba, Mkoa wa Kaskazini Pemba, hilo ilikuwa la kwanza naiomba sana Serikali iangalie.

Na Mkoa huu una 46 kwa 100 una majimbo 22 ya uchaguzi mimi nafikiri kulingana na mazingira yalokuwepo ya *population* kama hii nafikiri iko haja kuiangalia katiba kifungu cha 120(4) kuna haja ya kuangalia kinasema nini katika kipindi cha miaka minane hadi kumi au wakati wowote Tume itachunguza idadi ya mipaka na majina ya majimbo hayo kwa kiwango kile ambacho inahisi ni wajibu kuangaliwa upya. Mimi nafikiri kama Mkoa wa Mjini una 46% na una majimbo 22 nafikiri kuna haja ya kukiangalia kifungu hiki. Na hii ni 2012 leo 2017 nafikiri *percentage* hii imezidi na nitamshukuru Waziri kama atakuja kutwambia kwamba ikiwa 2012 ile asilimia 13 mpaka Machi tuna *percentage* gani pengine ishazidi 50 kwa hivyo Mkoa huu lazima tuungalie kwa uzuri zaidi.

Halafu kuhusu vikosi vya KMKM, JKU na Valantia nawapongeza kwa dhati kwa namna wanavyofanya kazi, wanafanya kazi katika mazingira yangu magumu sana na Serikali tumshukuru Rais kusema atawaongezea mishahara walingane na vikosi vya SMT na hilo amelifanya, mimi ningelimshauri kwa vikosi vyetu hivi vitatu pamoja na Zimamoto cha nne na cha tano Chuo cha Mafunzo kuangaliwa zaidi na kuwapita hao vikosi vya SMT kwa sababu mazingira wanayofanya kazi ni mazito.

Halafu vikosi hivi kwa mujibu wa katiba kifungu 122 wana tume ya utumishi kwa idara maalum hizi ningaliwashauri sana sana kwa sababu vikosi hivi ndivyo vinavyoilea na kuilinda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hivyo, tume hiyo maalum ambayo ndiyo inayoajiri iangalie vizuri sana vijana wanakavyoajiriwa katika vikosi hivi lazima wawe wazalendo sio kuajiri tu lazima wawe wazalendo na wakiwa wazalendo tutapata nafuu ya kuweza kuilinda hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini tukisema tuajiri tu hawana uzalendo tutakuwa tutapata matatizo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, naiomba Serikali wizara hii inasifika sana katika maendeleo ya mijini lakini katika Mkoa wetu wa Kaskazini, tunaomba waangalie sana ujenzi wa baadhi ya masoko nishukuru kwamba tuna soko la Kinyasini katika Mkoa wetu linaendelezwa vizuri sana. Lakini kuna masoko ya asili kwa mfano soko la Mkwajuni liangaliwe vizuri sana kujengwa upya na soko la Gamba na soko la Mfurumatonga hilo nilikuwa naomba sana.

Jengine la nne, kuhusu barabara za ndani nitamuomba sana Mhe. Waziri kuziangalia sana barabara za ndani hususan katika jimbo letu la Mkwajuni kuna barabara ya ndani kutoka Chunga Gamba pale kupitia Chutama, Kidombo mpaka Kibeni barabara hii ya ndani nayo kwa kipindi hiki nilikuwa naomba waiangalie vizuri na barabara ya mwisho kutoka Mfurumatonga mpaka Mlilile.

Kuhusu maadili ya vijana wetu kuna wenzangu wengi kwamba vijana wetu wanazuiwa kuhusu madisko, kwa kweli tulifika pahala pazito sana tumshukuru sana sana Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa namna anavyohimili na namna alivyolichukulia suala la kurejesha utamaduni wetu na maadili yetu ya Kizanzibari, tulifika pahala pazito ambapo vijana wetu wanajiuza dhahiri hakuna siri. Lakini kutokana na juhudi zake tunamshukuru sana na tumuungeni mkono nawashukuru sana Wakuu wa Mikoa mengine iliyosalia huko bado wamedhibiti hilo na hakuna matatizo kama hayo. Kwa hivyo utamaduni wetu ulikuwa unaanza kupotea tunaweza tukaurekebisha.

La mwisho alizungumza Mhe. Waziri kuhusu hati miliki kwa ajili ya Chuo cha Mafunzo lakini namuomba asiangalie hati miliki kwa Chuo cha Mafunzo tu angalie hati miliki kwa maeneo yote ya vikosi vyetu valivyojenga kambi na mashamba yao waangalie hati miliki. Nimeliona hilo kwa sababu nilipokuwa DC Magharibi alikuja mtu mmoja akanionesha waraka wa 1800 anasema kuanzia kiwanda cha viatu pale mpaka KMKM ardhi ile ni yao nikamfukuza, nikamwambia waraka wako huo hauko tena kuanzia tarehe 12 Januari, 1964 ardhi yote ni mali ya Serikali na kiwanda cha viatu kiko katika mamlaka ya Serikali na mpaka kutoka pale mpaka KMKM ni mali ya Serikali.

Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri kulizungumzia suala la hati miliki aliangalie vizuri kwa maeneo yote ya vikosi ambavyo vina kambi na vina mashamba ama JKU au KMKM au Valantia wapate hati miliki.

Kwa hayo machache sana Mhe. Mwenyekiti naomba kuunga mkono hotuba hii mia kwa mia wala sina matatizo yoyote. Ahante sana

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ussi Yahya Haji Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni waheshimiwa kwa mchango wako mzuri lakini kabla sijamuita Mhe. Miraji naomba nitoe taarifa kidogo inayohusu na wageni wa Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu.

Wageni hao ni kama wafuatao na wageni hao ni wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jimbo la Tunguu jumla yao ni tisa.

1.	Katibu wa Jimbo	Sharifa Maabadi Othman
2.	Mhe. Diwani wa Kuteuliwa	Mauwa Mohamed Ali
3.	Mhe. Diwani wa Wadi ya Ubago	Ussi Ali Mtumwa
4.	Katibu wa Mwakilishi na Mbunge	Hamadi Seif
5.	Ndugu Mussa Milele Peter	
6.	Ndugu Omar Azam Jecha	
7.	Sheha wa Shehia ya Tindini	Ndugu Jecha Ali Mussa
8.	Sheha wa Shehiya ya Binguni	Ndugu Ali Yussuf Mussa
9.	Ndugu Nassor Ramadhan Nassor	

Karibuni sana

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis Mussa tuendelee na Mheshimiwa nimemtaja Khadija Omar ajiandae.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kuchangiza hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, kwanza nianze kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wakiwemo vikosi, Wakuu wa Vikosi na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa kazi zao nzuri za kuitumikia wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana ili hotuba yangu ikae vizuri kwa sababu kuna kitu kidogo naomba nikisema. Naomba niwapongeze sana Club ya Yanga Afrika kwa kuchukua kombe kwa mara ya 27, lakini pia kwa umiliki wa lile

kombe lenyewe kwa sababu tumeshashinda mara tatu. Baada ya hayo sasa naona mambo yangu yatakaa vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye aya ya 31 ya Jeshi la Kujenga Uchumi. Naomba niwapongeze Mkuu wa kKkosi hiki na wasaidizi wake wote, lakini naomba nisaidie tu mchango wangu katika kikosi hiki, kwa sababu mara zote *nature* ya kikosi hiki kina rasilimali watu ambao wanaingia na kutoka, lengo lao kubwa kwenda kupata mafunzo fulani lakini pia kutengeneza utaratibu wa uchumi. Kwa hivyo, wana maeneo ya kilimo, wamepata vijana kazi ambao watapata mafunzo mbali mbali na kusaidia maeneo hayo ya kilimo ambayo nimeyataja. Lakini nina wasi wasi sana tunaona vijana wanaingia na kutoka kila mwaka na maeneo yapo, lakini uzalishaji wao haupo vizuri na sijui kuna kasoro ya kupata watalaamu bora ambao wanaweza wakasaidia ili wakasukuma ule mwelekeo na dhamira kubwa ya jeshi hili.

Kwa hivyo, niombe tu Mhe. Waziri kwa sababu programu zao ukiziangalia hatuoni labda kuwazidishia vifaa, hatuoni kuwazidishia utaalamu katika sehemu kubwa ya uwekezaji wao. Kwa hiyo, tumewapa maeneo mengi lakini hatuoni zile jitihada zao zikatufikisha pale pahala tunapopataka. Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi naomba sana kikosi hiki tukitumie vizuri, tukitumie vizuri kama dhamira ya kuanzishwa kwake tunaweza tukafika pahala pazuri na wakachangia sehemu kubwa ya uchumi wetu kwa sababu vijana kuingia pale pamoja na kupata mafunzo lakini wanafanya kazi pia, wakipoteza nguvu kubwa bila ya matokeo mazuri basi utaona ile dhamira ya kuwapeleka haipo.

Kwa hivyo, hebu twende na dhamira kamili ya kuanzishwa kikosi hiki pia niombe sana kupitia kikosi hiki hiki tulipoanzisha suala la sekta la ya utalii, mimi naomba nikiri na wenzangu wakija watakiri kama wa kweli kama mimi. Hatukujiandaa vizuri kwenye ulinzi wa utalii, kwa ulinzi ule tumekwenda tu *verbal*, kama tungejipanga vizuri tukawa-*train* vijana hawa hawa tukawaundia asasi nzuri ndani yake hata kama hatukuwaajiri sisi pale tunawapa mafunzo yale ambayo tumewapangia lakini tunawa-*organize* tunakwenda kuwapeleka wakalinde watakuwa ni vijana wazuri na ulinzi utaimarika katika sekta hii ya utalii. Lakini leo utalii huku ukenda kuna walinzi wanalinda kila siku matokeo mabaya yanatokezea. Walinzi hao hao ndio wanaosadia *information* za kuibiwa hayo mahoteli yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tungekuwa tuna asasi ndani yake hatuwaajiri vijana, lakini ile asasi inawa-*organize* wao tunawa-*train* baadae tunakwenda sasa kuwaombea ajira katika maeneo yale, basi vijana hawa wasingekuwa wanasaidia uhalifu, wangekuwa wanasaidia ulinzi wa nchi hii kwa sababu

wanaripoti kwetu. Kwa hivyo, ningeomba tu ndani yake basi waone na wafikirie suala hilo. Naomba nihame hapo niende kwenye eneo la aya ya 40 Kikosi cha KMKM.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana na wao niwapongeze kwa kazi nzuri, wamejitahidi tunaona pamoja na ufinyu wa vifaa na vitu vyengine lakini jitihada wanayoichukua kwa sababu tunasikia taarifa mbali mbali za kukamatwa kwa baadhi ya wanaovusha magendo. Lakini niwapongeze pia kwa kukaa katika zile *strategic area*, nikuombe Mhe. Waziri kikosi hiki basi kiwezeshwe vifaa navyo pia kwa sababu ukiangalia kwenye maeneo mengine ambayo wamekaa hakuna hata zile boti za ku-*support* kama kunakuja taarifa ambayo inatokezea ya ghafla mpaka waji-*organize* watoke kwengine waende kwengine. Sasa tuone kila eneo ambalo wamekaa basi kuwepo na boti za kuwa-*support* wao kwa sababu hawa ulinzi wao mkubwa ni kulinda ile sehemu ya mipaka yetu, na wamekaa mwahala mzuri naomba nikiri kwa sababu kila ukitizama ukienda eneo la Nungwi kuna pahala wapo, ukienda Kusini kuna pahala wapo kila maeneo. Lakini sasa suala la vifaa la kuwawezesha basi hili naomba sana liende na utaratibu kama wao wenyewe wamejipangia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana nimwambie mkuu wa kikosi hiki wako pia wafanyakazi ambao hawamsaidii. Mimi siku moja katika mazungumzo ya kawaida kuna mtu mmoja anakaa Ndijani lakini na yeye mdau mkubwa katika hayo hayo mambo ya kusafirisha magendo. Anasema sisi tunafanikiwa mpaka tuzungumze na wao wenyewe askari ndio tunapita pale, hili ni jambo kubwa sana askari aliyekula kiapo anaenda kutoa utaratibu mzima kuwa sasa hivi hatupo, sasa hivi tupo si jambo jema. Nimuombe sana Mhe. Waziri awaangalie na atumie vyombo vyake vimfikishe pahala pazuri tunaamini tutafanikiwa panapo mashirikiano.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwa haraka haraka Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kwenye aya ya 46. Naomba na wao niwapongeze lakini pamoja na pongezi hizo na hongera hizo naomba sana sasa serikali nayo iangalie uwezekano mkubwa kwa sababu hawa wanafanya kazi kubwa. Matokeo tusiyoyatarajia yakitokea basi na wao mpaka waji-*organize* gari moja hili litoke liende pahala hapa, hebu tuone tunajipanga ki-Wilaya kwamba kila Wilaya iwe inajitosheleza na vifaa vyake ya kwenda kuhami moto. Kwa hiyo, tukiwa tuna *fire station* kwa kila maeneo haya yatawasaidia hawa kujipanga vizuri na maeneo ambayo moto unatokezea au majanga yanatokezea. Sasa tuone serikali tunawasaidia tunajua serikali ina dhamira njema nao, lakini ili tufanikiwe vizuri majanga haya tuweze kuyapunguza au kuyahami kwa wakati ambao yanatokezea basi na wao tuwapangie utaratibu mzuri wa kuwapa vifaa vya kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika Kikosi cha Valantia aya ya 52.

Mhe. Mwenyekiti, dhamira kuu kisheria ukiiangalia kuanzishwa kwa kikosi hiki ukisoma utakuta hawa wamepewa fursa kubwa sana, lakini hawaitumii katika kusaidia ulinzi wa nchi hii. Mhe. Waziri najua unajua lakini ukipitia kwa umakini utakuta hawa wamepewa mpaka fursa ya kumkamata mtu na kumpekua, lakini lini wamefanya kazi hiyo? Sasa leo tunaunda kikosi sheria ipo, kazi zipo za kufanya watafanya nyengine na zile ambazo zitatusaidia sisi kutokuwatafuta hawa wenye madawa ya kulevya au waharibifu katika mazingira mengine haifanyiki na sheria inawapa fursa. Basi nikwambie Mhe. Waziri Mapinduzi ya mabadiliko ya kazi za kikosi hiki uyaangalie kwa umakini iende na kasi ile ambayo matarajio yetu sisi ni kufanya kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niende katika Serikali za Mikoa, niwapongeze Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya kwa kazi nzuri lakini naomba kwanza nianze kumtetea Mkuu wa Wilaya ya Kati. Katika ziara za Kamati ya *PAC* kwenye ukaguzi ule tulipita kwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini tukapelekwa Wilaya ya Kati tukaliona jengo zuri wana dhamira nzuri, walijipanga vizuri jengo lile sina uhakika wa miaka mingapi lakini naamini saba inafika. Tufike pahala tukianzisha miradi ya maendeleo kama ile tusiiwache kwa muda mrefu, kwa sababu nayo wenyewe itaharibika. Kwa hivyo, na huku ukitizama hizi programu zao hatuoni fungu la kwenda ku-*support* ujenzi ule bado tunambakisha katika jengo lile la urithi sijui alijenga nani, nadhani Marehemu Karume. Lakini naomba sana tulimalize jengo lile ili na yeye aondoke pale aende katika jengo ambalo lina hadhi ya kukaa Mkuu wa Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, bado nibaki katika Serikali za Mikoa. Ni kwamba lipo tatizo ambalo tuliliona katika masuala hasa ya fedha kwenye kuandaa ma-*internal auditor*, kuandaa zile bodi za zabuni yalijitokeza sana. Mhe. Mwenyekiti, wanatumia bodi ya Mkoa kwa shughuli zao zote, kwa hiyo wanazo fursa kisheria za kuanzisha bodi zao mpaka katika *level* za Wilaya hawa wakafanya kazi zao na wale wakafanya kazi zao sawa sawa na zile *audit committee* ipo ya wizara lakini ma-*internal auditor* wawemo katika Wilaya zao na Mikoa yao. Sasa leo kazi hazifanyiki mpaka atafutwe afisa kutoka Mkoani huko au kutoka wizarani huko. Hilo si jambo jema naomba viongozi wenzangu washirikiane na wizara yao na wizara ishirikiane na hizi Serikali za Mikoa na Wilaya ili kujenga *base* nzuri kwa ma-*internal auditor* lakini kwa bodi zao za zabuni ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Kwa hivyo, kwa ujumla hapa nimesemea kwa maeneo yote ya Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende sasa kwenye aya ya 71 ambayo kumeoneshwa hapa kwa wenzetu wameondosha makontena Darajani, wamesafisha pia juzi pale Michenzani. Mimi naomba Mhe. Waziri nilikuwa najua huko nilikotokea nilitokea serikalini na sijaacha kazi nimechukua tu likizo bila ya malipo. Kulikuwa kuna dhamira nzuri ya serikali katika kuimarisha ile Darajani *Corridor*, kuna michoro ilikuwa tayari imeshatayarishwa *mall* ambayo itajengwa pale. Dhamira ile ni dhamira ya kiuchumi, kujenga *mall* leo ni kutengeneza *business center* ya Zanzibar, kwa sababu wageni wanakuja wanashangaa nchi hii Mji Mkuu wake hauna hata *business center*. Uingie tu katika duka la Suma maana yake ndio duka kubwa nchini, na mule utapata nguo vitu vyengine hupati. Sasa wageni ili wasitushangae basi tuwe *na business center* yetu, na dhamira ile ya serikali ilizaliwa pale na Baraza la Manispaa ikaenda kwenye Serikali ya Mkoa, ikenda katika wizara lakini hadi leo na naamini serikali imefika. Kwa hivyo, dhamira ile naomba wenzetu tuwaunge mkono basi suala lile liende mbele lisabaki tubadilike katika mazingira mapya, sio kila siku tunatangaza tu kutakuwa kuna *Zanzibar Smart City* kama hatukuanzia pale huko kwengine watafuta nini. Kwa hivyo, twende katika utaratibu mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine pia kulikuwa kuna dhamira ya Baraza hilo hilo la Manispaa katika utaratibu huo huo wa kuimarisha uchumi, lakini katika kuimarisha maeneo yake na ndio eneo la mapato nalizungumzia kabisa. Walikuwa wana dhamira pia ya kuondoa ile *diplomatic supermarket* kujenga jengo pale karibu la ghorofa sita kwa saba. Dhamira yao ni nzuri lakini mipango ya kiwizara wamekwama wapi, kwa hivyo maeneo haya mawili Mhe. Waziri atakapokuja atueleze zile dhamira njema za wenzetu, na dhamira hizi za Baraza la Manispaa Zanzibar naomba na wale Manispaa ya Magharibi, na wale Manispaa ya Magharibi "A" na Magharibi "B" wafate wasifukuzie tu Manispaa ya Mjini ijenge siku moja mtu aje atetee kuwa wahamishiwe zile *source* zao za kupata mapato ambazo walishazitayarisha.

Mhe. Mwenyekiti, hata wao Magharibi "A" na "B" kama wana eneo Mjini wamelipata waje waekeze sio eneo fulani litakuwa la huyu, eneo fulani likaja huku liwe la huyu. Mimi naomba sana katika mazingira haya kila taasisi ijitegemee katika kutafuta miradi yake ya kiuchumi pahala popote wa Mjini anaweza akaekeza Kaskazini Unguja, lakini wa Kaskazini Unguja anaweza akaekeza Mjini.

Mhe. Mwenyekti, mimi naomba niungane na wenzangu la kumuomba Mhe. Waziri wa Fedha katika taasisi zote zinazokusanya mapato kwa kusaidia serikali basi lile jaribio la EFD basi liende kwa wote. Leo Baraza la Manispaa,

Mabaraza ya Miji yanakusanya kodi zinavuja sana, zikiwa zile za *parking* leo ukimleta mtaalamu akifanya *estimate* atakwambia *parking* hizi zinakuja na milioni tisiini, lakini uhalisia utapewa hamsini, katika mambo haya tunayokwenda ya *manual*. Sasa tubadilike katika ku-*control* mazingira yetu haya bora ya ukusanyaji wa mapato. Kwa hivyo, Waziri wa Fedha upo vianzio tunavyo vizuri, pesa zipo na tutazipata lakini tujipange tu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika bajeti ya wizara hii sina mengi sana naomba sana niwapongeze na niwaombe wenzangu mafungu ya wizara yote ambayo wamejipangia kufanya kazi zao, basi tuyapitishe bila ya mgogoro wowote. Baada ya hayo naomba niunge mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Kwaza kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Khadija Omar Kibano wa Jimbo la Mtambwe akifuatiwa na Mhe. Mussa Foum Mussa wa Jimbo la Kiwani na Mhe. Mwanaidi Kassim nafasi za wanawake ajitayarishe.

Mhe. Khadija Omar Kibano: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii leo na mimi nikapata kuchangia machache katika Mkoa wangu wa Pemba. Kwa heshima na taadhima napenda kwanza kumpongeza Mkuu wa Mkoa wangu wa Kaskazini Pemba pamoja na Wakuu wa Wilaya zake na watendaji wote waliokaa kitako wakakitunga kitabu hiki cha hotuba ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kwa hivyo, nawashukuru sana kupitisha hotuba hii ili kukaa kitako na kushirikiano kwa pamoja ukaifanyia kazi na sisi tukapata kuipitisha katika bajeti hii inayoendelea.

Kwanza nataka niende upande wa barabara. Mhe. Mwenyekiti, barabara zilizopo katika Jimbo la Mtambwe barabara hizi ni za ndani, kwa sababu kuna barabara za ndani hazijapata kufanyiwa kazi na tangu niingie katika Baraza ili sijapata kusikia au likazungumzwa kuhusu barabara hizi za ndani. Kwa sababu kuna barabara kule za vijiji zilizopo Mtambwe zinakuwa zina watu waliokuwa ni wazalishaji wa zao la karafuu. Kwa hivyo, kwanza tukiingia katika barabara ya kutoka Chanjaani barabara ile kuna kikosi cha KMKM kule na kuna kituo cha karafuu. Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi hiki cha mvua kama kungekuwa sasa hivi kuna zao la karafuu barabara ile sasa hivi ingelikuwa haipitiki na tayari ingelikuwa gari ikishafika kule kupanda juu haipandi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri suala hili la barabara za ndani za jimbo hili azifanyie kazi na azione kwa uangalifu.

Mhe. Mwenyekiti, suala hilo hilo la barabara kwanza liko katika masuala ya Halmashauri. Kwa sababu mimi nilikuja Mhe. Mohammed akanambia hili suala linahusiana na watu wa Halmashauri. Kwa hivyo, nataka na mimi hizi barabara nijengewe kutokana na shughuli zetu zilizoko kule, kwa sababu wananchi wangu wanapata mtikisiko mkubwa wa kufanya kazi zao za kila siku.

Nikija katika masuala mengine nije kwenye Vikosi vya KMKM. KMKM mimi ninachokizungumza hapa kwa upande wao ni kuhusiana na habari ya lindo la mwaka utakaofuata penye uhai na majaaliwa kwa zao la karafuu kwa upande wa baharini. Kama alivyozungumza Mhe. Miraji Khamis Mussa vitendea kazi vitakavyokuweko baharini viwe ni vitendea kazi vya kasi na viwe vinafanya kazi kwa uangalifu. Kwa sababu hawa ni watu waliokuwa wanalinda nchi yetu kwa pamoja kwa upande wa zao la karafuu lilioko katika wizara zetu hizi za Zanzibar. Suala hili watu wa KMKM hawa ni watu waliokuwa wanalinda sana vituo mbali mbali, watu wanaolinda sana katika maeneo mbali mbali halafu wao ndio wanaoinua huu uchumi wa Zanzibar, kutokana na hali hii ya lindo la baharini.

Mhe. Mwenyekiti, tukienda katika masuala ya Kikosi Chuo cha Mafunzo, wao mpaka sasa hivi katika kusikitika kwangu na kuwaona kwanza wao nyumba zao haziridhishi za makaazi. Nyumba nyingi hizi zinakuwa ni chumba kimoja tu mpaka sasa hivi, sijui wizara imeonaje askari hawa wanaokaa katika majumba yale mpaka leo. Kwa sababu watu wanakuwa na familia zao kubwa, wanakuwa na watoto wanne au watano na bado wanaishi katika nyumba zile. Kwa hivyo, naiomba wizara ikiwa itakuwa wanawaonea kwa jicho la huruma askari hawa naomba wafanyiwe mpango na wao wajengewe japo nyumba ya ghorofa moja kwa maeneo ya Pemba na Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, hata ofisi zao mimi naziona haziridhishi kutokana na vyumba ni kidogo sana. Kuna vyumba vya wakubwa hawa wanavyofanyia mikutano, vyumba vya wakubwa wao hawa wanaokaa katika mikutano yao kujadiliana inakuwa vyumba vile haviridhishi. Kwa sababu mabosi mule wanamokaa katika kufanya kazi zao vyumba vile ni vidogo mnakuwa mna viti vitatu au vinne hata ukienda wewe mgeni hupati pa kukaa. Kwa hivyo, naomba serikali iwaone hawa kuja kuwajengea majumba haya na kuwaona hawa ili wafanyiwe kazi katika hili. Kwa sababu masuala yao ya maendeleo au fedha zao za maendeleo mimi naona si kidogo sana, lakini sijui tu ni sababu gani iliyopelekea mpaka sasa hivi wakawa bado hawajaonewa jicho la huruma kwa utendaji huu wa nyumba hizi.

Nikienda katika Kikosi cha JKU, JKU mpaka sasa hivi vijana wetu walioko pale wanajenga taifa, katika kujenga taifa kwa vijana hawa bado naona hawajaajiriwa. Kwa hivyo, nataka Mhe. Waziri aniambie katika miaka hii iliyopita na mpaka hivi sasa tunavyoendelea na kutaka kupitisha bajeti hii ya mwaka huu ni vijana wangapi aliowapangia kuwa watawaajiri baada ya kutoka pale kwenye mafunzo yale.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niende katika masuala ya ndoa na talaka. Hapa ndoa na talaka zimewekwa 180 iwapo ni ndoa hizi sizijui kama ni za mwaka au ni za mwezi. Halafu talaka zimewekwa 10 nazo hivyo hivyo sifahamu kama ni za mwaka au mwezi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri aje anipe maelezo ya kwamba hizi ni ndoa za mwaka au mwezi.

Halafu katika kuchukua hivi vitabu vya ndoa kwa mashekhe naona hizi takwimu zilizowekwa hapa ni kidogo sana kama ni Unguja na Pemba. Namuomba Mhe. Waziri kwa sababu hapa wanachukua vitabu hivi vya kupitisha kwenye ndoa zao kwa Mufti Mkuu wa Serikali. Sasa ninachokiomba mimi naomba Mhe. Waziri anambie hawa Mashekhe wanashughulika vitabu hivi ni wangapi na waliopewa vitabu hivi katika wilaya au mkoa kwa Unguja na Pemba ni wangapi na wakizipata ripoti hizi wanazipeleka wapi. Kwa sababu kuna mashekhe wengi wanakuwa wanafungisha ndoa hizi lakini takwimu hazipatikani kutokana na kuwa wakishafungisha ndoa zile hawazipeleki kunakohusika, wanakaa kutia fedha mfukoni kwa hivyo kile kipande cha serikali kinachoingia pale hakipatikani. Sijui, ninachokiona mimi ni kama upungufu wa elimu au ni tatizo gani, lakini naona ni mambo yao tu.

Sasa kuna ndoa hizi za mkekani. Ndoa za mkekani ni nyinyi sana zinazokuwa zinafanywa katika mashehia na wilaya zetu na mikoa, ndoa hizi haziripotiwi kabisa ndani ya mikoa yetu, lakini linapotokea tatizo la kuwa mtu ameshafanyiwa vituko na mume wake huko basi ndoa hizi zinakuja wilayani ili kuondoshewa lile kero lake. Kwa hivyo, naomba kama ndoa hizi zitafika katika suala hilo ikiwa haikuripotiwa ndoa ile isifanyiwe kazi.

Nikiendelea niende katika masuala ya Baraza la Mji au kodi kama alivyozungumza mwenzangu upande wa risiti kwa wafanyabiashara ndogo ndogo na biashara za jumla. Hizi risiti zinazotolewa katika risiti za jumla watu wanaochukua vitu mule katika maduka, vitu vya rejareja, vidogo vidogo lakini huwa kuna risiti maalum zionatumika. Lakini nahisi mimi hawa watu wa Halmashauri hawafanyi kazi zao inavyopaswa kwa sababu moja. Hivi karibuni tulikuwa tunatoka Unguja kuja Pemba tulinunua vifaa pale ChakeChake tukapewa risiti haina jina la mtu, haina namba ya simu, haina mapokezi, haina

jambo hata moa ni risiti imeandikwa fedha tu shilingi 4,000 ulizotumia basi. Kwa hivyo, mtu kama huyu ikiwa utakuwa umekamatwa njiani na umechukuliwa kitu chako ukataka kuja kumtafuta huwezi kumpata. Naiomba wizara watu kama hawa wanaofanya biashara ndogo ndogo zilizokuwa hazina mipangilio maalum basi naomba watu hawa watafutwe na wakamatwe ili hizi risiti zinazotumiwa hivi zisiende, kwa sababu mapato ya serikali yanakuwa hayapatikani.

Mimi sina masuala mengi masuala mengi kutokana na watu wengi kuwa wameshachangia na mimi nimeshachangia kidogo, naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nawapongeza viongozi wote waliomo humu, penye uhai na majaaliwa Mwenyezi Mungu atupe rehema na amani atupitishie bajeti hii kwa ukamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Khadija Omar Kibano kwa mchango wako Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe, sasa naomba nimwite Mhe. Mussa Foum Mussa wa Jimbo la Kiwani akifuatiwa na Mhe. Mwanaidi na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ajitayarihe.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kupata ruhusa ya kuchangia hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wao wote kwa kutuletea hotuba yao hii nzuri na tunaendelea kuichangia. Vile vile niwashukuru au niwapongeze Mkuu wa Mkoa wetu wa Kusini Pemba pamoja na Mkuu wa Wilaya wa wilaya zote mbili, kwa jitihada zao kubwa walizozifanya kwa kipindi hiki cha mvua. Kwa sababu mambo mengi yametokea kumetokea nyumba zimeingia maji, barabara zimeharibika na wao wamekuwa mstari wa mbele kwa kuyashughulikia masuala haya. Kwa hivyo, vile vile niwapongeze kwa jitihada yao hiyo na tunapenda kuwashukuru wananchi kwa vile wameshirikiana, hapakuangaliwa siasa, itikadi, kwa wale waliovunjikiwa na nyumba zao wamehifadhiwa na wenzao. Kwa hivyo, hilo ni jambo la kusifiwa wananchi wetu na pia waendelee kuvumilia na mitihani kwa sababu hii ni mitihani ya Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na mimi napenda kidogo kuchangia kwa sababu mengi yameshazungumzwa na Waheshimiwa waliyoanza kuchangia, lakini mimi nitaanza na kuchangia vita dhidi ya dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la madawa huko nyuma tumeshalizungumza sana na tunaendelea kulizungumza, kwa sababu ni jambo kubwa sana vijana wetu wengi wanaumia kwa madawa ya kulevya. Ki ukweli sote tuliopo hapa tukiangalia familia zetu au jamaa zetu utaona hakuna mtu aliyekuwa haguswi na jambo hili la dawa za kulevya. Sasa vile vile niwapongeze Wakuu wa Mikoa wote kwa jitihada zao wanazozifanya ili kuhakikisha kwamba suala hili linapungua kwa kasi kubwa sana, kwa sababu ni jambo linaloathiri vijana, watenda kazi wakubwa wa taifa hili wanaathirika na madawa. Kwa hivyo, ni vyema serikali ikachukua jitihada kubwa ya kulidhibiti suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika vita dhidi ya dawa za kulevya naomba ninukuu ukurasa wa 29 *paragraph* ya 67. Hapa kidogo nitaomba nipate maelezo lakini kwanza naomba ninukuu.

Kifungu cha 67 kinasema kwamba:

"Mhe. Mwenyekiti, Mikoa yote ya Unguja na Pemba imeendelea kutekeleza mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya. Katika Mkoa wa Mjini Magharibi wahusika wakuu wa dawa za kulevya 24 wamebainika kuwa wana makosa ya kujibu na hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa".

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nipongeze Mkoa wa Mjini Magharibi kwa jitihada yake kubwa, lakini nataka niulize kwamba hapa hii *paragraph* inaelezea kwamba mikoa yote lakini hapa pamezungumzwa mkoa mmoja tu kwamba wahusika 24. Je, hii mikoa mengine hii kazi hawakufanya au hapa Mhe. Waziri mkono umeteleza? Kwa sababu ningelipendeza kwa vile imetaja Mikoa yote ya Unguja na Pemba basi kila mkoa ilikuwa tuelezwe, ni vizuri ilikuwa tuelezwe kwamba mkoa huu imewakamata watu wanne, mkoa huu watu 10, mkoa huu watu 50 kila mkoa tungeliona jitihada yake waliyoifanya lakini hapa pamezungumzwa mkoa mmoja tu.

Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa maelezo hapa atuelezee kwamba je, hii mikoa mengine haikufanya au kasahau? Ikiwa kasahau basi atueleze kwamba kila mkoa idadi ya wale watu wenye kuuza madawa au kutumia waliofikishwa mahakamani au waliokamatwa. Kwa sababu tunasikia na mikoa mengine. Hata leo nimesikia kwenye Mawio mtu aliyekamatwa Nungwi na madawa ya kulevya na Nungwi iko katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na hilo jambo lilikuwa limeendelea huko nyuma lakini hapa umetajwa mkoa mmoja tu. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze je, hii mikoa mengine watu hawakukamatwa au kasahau katika kuitolea maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile niendelee kuzungumzia habari ya ugatuzi wa madaraka. Kwanza naipongeza serikali kwa jitihada yake kubwa ya kuona kwamba sasa mambo yaliyokuweko kwenye Serikali Kuu yaletwe kwa wananchi. Si jambo baya, lakini Mheshimiwa huu ni mzigo, kwa sababu mambo haya yako Serikali Kuu na tunaona uendeshaji wake, yaani wakati mwegine mambo yanasuasua. Sasa leo tunayapeleka kwa wananchi huko chini tunaweza tukapata mafanikio lakini wakati huo huo tunaweza tukaharibikiwa zaidi. Kwa uoni wangu mimi nitoe mfano, hapa tumeelezwa kwamba mambo yatakayoanza kujaribiwa ni elimu ya msingi, afya na kilimo. Sasa mimi nitoe maelezo kidogo kwa mfano hii elimu ya msingi. Katika skuli yangu ya Mwambe pale katika walimu waliokuwepo sehemu ya msingi ni walimu 28, wanawake 14 na wanaume 14. Lakini pale tuna wanafunzi 2,640, wanawake 1,335 na wanaume 1,305, lakini tuna walimu 28. Ukiangalia upungufu ulioko pale tuna upungufu wa walimu 30, inaonesha ule upungufu ni mkubwa kuliko wale walimu waliopo. Sasa hapa inaonesha kwamba hili jambo ni kubwa nalo ni zito, kila mwalimu pale ina maana wanafunzi wanakwenda *shift* tatu. Mwalimu mmoja ana vipindi 54 mpaka 55, kila mwalimu ana madarasa mawili anayoyaongoza mwalimu mmoja.

Sasa hii hali hata mwaka jana niliielezea, ukiiangalia hii hali kwa skuli ya Mwambe ina maana ni hali nzito, wanafunzi wanaingia *shift* tatu, *shift* ya kwanza inaanza saa 1:15 hadi saa 3:55; *shift* ya pili inaanza saa 4:10 hadi saa 6:00 na ya tatu inaaza saa 7:00 hadi saa 11:55. Hali kama hii hao wanafunzi watakuwa wanasoma au wanakwenda wakicheza tu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika suala hili naionea huruma sana hii wizara, hii wizara tokea huko nyuma ni kubwa na ndio mara nyingi ukaona wizara hii inapata mabuti mengi na ninaamini kwamba itaendelea kupata mabuti mengi kwa hali kama hii.

Mimi namuomba tu Mhe. Waziri kwa mara hii kwa vile ndio ana *ratio* kutoka Wizara ya Elimu kwa upande wangu mimi sitokuwa na mabuti, isipokuwa namuomba tu kwamba hali kama hii niliyoielezea basi hayo mambo yakitengenea tukiipitisha basi hii hali aichukulie hatua hasa kwa skuli ya Mwambe hali si nzuri, walimu kidogo tena sana.

Halafu tatizo linalojitokeza pale tunao walimu waliomaliza cheti na *diploma* hawa angalau ndio wanaosaidia, lakini hao walimu waliopo ikiwa wataajiriwa wote basi bado tatizo halijaondoka, lakini tatizo linajitokeza zaidi kwamba hata hapo inapotokea hiyo ajira basi hata walimu hawa waliomaliza *diploma* pale

hawaajiriwi, anaajiriwa mtu mbali anakuja pale. Hii inaumiza zaidi. Sasa namuomba Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti, hili suala alione, mara hii ndio mwanzo analianza yeye lakini hali yetu ndio kama hii niliyoielezea. Nadhani Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali haya mambo anayajua kwa sababu sio mara ya kwanza kuyazungumzia na sijui kuna uoni gani, kwa sababu ukipeleka kwenye Wilaya yetu ya Mkoani ukiangalia skuli zote ukizipitia basi unaweza kukuta hii *ratio* iliyojitokeza hapa sijui inafuatwa *ratio* gani. Kwa sababu hapa petu sisi pana upungufu mkubwa zaidi ukilinganisha na skuli nyengine.

Sasa naomba kwa mara hii suala nalizungumza sana lakini na mwaka jana nililizungumza lakini matokeo yenyewe hali ndio ile ile. Kwa hivyo, naomba nimesikia tangazo kwamba huenda mara hii wakaajiriwa hao walimu waliomaliza Diploma na Cheti wanafika walimu 300. Kwa hivyo, naomba hili jicho la hurama lijitokeze katika skuli yetu hii. Lakini pia naomba kwa wale walimu waliomaliza Cheti na Diploma wale vijana wetu wa Muambe basi watakapoajiriwa hao walimu hawa wapewe kipaumbele kwa sababu wanajitolea sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo vile vile niende katika Usajili ya Vizazi na Vifo na Kadi za Utambulisho. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba haya masuala yote kwa mara hii yameunganishwa na sio baya. Lakini wasiwasi wangu ni kwamba tulikuwa na sehemu moja kwa mfano pale Wilayani palikuwa panasajiliwa vizazi na vifo. Lakini ulikuwa ukipeleka taarifa zile za vizazi na vifo unaweza ukaa hata miaka mitano, sita, saba cheti bado hujakipata. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba haya mambo yanaunganishwa sehemu moja. Je, hilo suala hutokujakaa miaka kumi cheti hujakipata.

Sasa naiomba serikali na kwa vile wenzangu wamezungumza kwamba hiyo pesa iliyotengwa kwa ajili ya shughuli hizi bado ndogo. Sasa tunaogopa wananchi wetu kuja lalamika sana. Sasa tunaomba kwa hali yoyote hili suala liangaliwe ikiwa pesa iliyotengwa ni ndogo basi iongezwe ili wananchi wasije wakalalamika sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile niende katika suala la barabara hasa hizi za *feeder road* niizungumzie barabara yetu ya Mtambilie Mwambe. Mhe. Mwenyekiti, barabara hii ni katika zile barabara zilizojengwa mimi nathubutu kusema katika kiwango kidogo sana na barabara hizi zimechimbuka au zimeharibika kabla ya kuja mvua. Lakini iliponyesha mvua barabara hizi zimeharibika sana. Kwa vile barabara hizi zimepelekwa katika wizara hii na

kwa vile barabara nyingi zimeharibika hasa hizi za ndani ndani. Kwa hivyo, tunaiomba serikali kwa vile barabara nyingi zimeharibika kwa sababu kubwa ya mvua kwa mara hii kuwe na mfuko maalum au kuwe na kitengo maalum kitakachotengeza barabara hizi ili zisije haribika kabisa kabisa yaani zikamalizika zaidi. Kwa hivyo, tunaiomba wizara husika ilishughulikie suala hili la matengenezo ya barabara.

Vile vile niseme kwamba napongeza zaidi kwamba hizi barabara za ndani zaidi sasa zitakuwa chini ya hizi Halmashauri, Mikoa na zitakuwa zinashughulikiwa zaidi. Lakini nataka niseme kwamba kuna mambo huwa yanajitokeza kwa mfano, tumejenga barabara bado hakuna nyumba kwenye barabara ile. Lakini inavyojitokeza anaweza akatokea mwananchi anakajenga nyumba mpaka akaimaliza bado hakuna makatazo ya aina yoyote inasubiriwa mpaka nyumba ile imeshahamiwa mtu anaendelea kuishi ndio baadaye inakuja wakati mwengine wanavunjiwa au anahamishwa, huu si utaratibu wananchi wetu masikini.

Kwa hivyo, ikiwa kuna namba maalum ya kuwa huwezi ukajenga mpaka pengine iwe mita fulani mita kumi au ishirini za barabara. Kwa hivyo, huo utaratibu ufuatwe. Lakini inawezakana mtu kajenga nyumba kwenye mapito ya maji lakini nyumba ile kwa mfano anaenda Diwani au muhisika yoyote aliewekwa kuna kina kima maalum alichotolewa lazima atatikiwa atoe. Lakini hawezi akaambiwa hapa ulipojenga nyumba hapafai nyumba yako iondoe kabla hujanza *foundation*, anasubiriwa mpaka nyumba inamaliza ana anavunjiwa au yanatokea yanayotokea huu si utaratibu.

Sasa mimi naiomba serikali kwa vile haya mambo yanarejeshwa kwenye wananchi haya mambo yashughulikiwe na mapema ikiwa mtu kajenga kwenye vianzio vya maji ikiwa kajenga kwenye njia za maji basi pale anapoanza kujenga asisubiriwe mpaka ameshajenga au kajenga kwenye barabara karibu na barabara ianze mwanzo kuwaambiwa kuwa hapa si ruhusa kujenga na hatua za kisheria zichukuliwe huo ndio utaratibu. Lakini tusisubiri mpaka keshamaliza mambo yote ndio tena pale matokeo yanajitokeza wananchi wanapiga kelele huu si utaratibu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi baada ya maelezo hayo nasema kwamba naunga mkono hotuba hii asilimia mia juu ya mia. Lakini namuomba tu Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kwamba ile Mikoa mingine kwa ajili ya zile dawa za kulevya je, leo haijachukuwa hatua au vipi au kasahau kwa sababu na yeye ni binaadamu. Baada ya maelezo hayo ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mchana huu kuwa na afya nje. Pia nitoe pongezi zangu za dhati kwa Rais wangu wa Zanzibar na Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohd Shein.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii kukupongeza wewe kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri na watendaji wao wote katika wizara hii kwa hotuba yao nzuri ambayo tumewasilishiwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze katika ukurasa wa 72 kiambatanisho cha 4. Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe tayari wamechangia hotuba hii lakini na mimi kwa vile hotuba yote imejikita katika kitabu hichi itabidi na mimi nijikite katika maeneo hayo hayo waliokuwa tayari Wajumbe wameshachangia lakini na mimi nitachangia.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri pale atakapokuja kutoa hoja anipatie ufafanuzi juu ya suala zima la makusanyo ndani ya mikoa yetu. Kwa nini kila hali ya makusanyo inakuwa hairidhishi na tukizingatia kwamba vianzio vingi vya mapato vipo. Mhe. Mwenyekiti, mfano wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kuna asilimia 41 tukiangalia kuna vianzio vingi vya mapato. Sasa nataka nijue kuna sababu iliyopelekea kushindwa kufikia nusu kile walichopangiwa. Halkadhalika Mkoa wa Mjini Magharibi kuna asilimia 42 kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mkoa wa Kusini Pemba, kwenye makadirio hapaoneshi asilimia kuna sababu gani zilizopelekea hata makadirio yasiainishwe ili tukapata kujua wamekusanya kwa kiwango gani.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika mchango wangu nije Tawala za Mikoa. Mhe.Mwenyekiti, nije katika utekelezaji wa masuala ya jumla katika Mikoa. Nianze na suala la uhamiaji holela suala ambalo linahitaji kufanyiwa mikakati maalum kwa kuzingatia sheria na taratibu zetu ambazo tumeziweka.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli katika Mikoa yetu kuna uhamiaji holela watu wanahamia bila ya utaratibu maalum wanaingia tu. Tukilizungumza hilo tuliangalie na suala la Bandari bubu. Mhe. Mwenyekiti, kusema ukweli suala la Bandari bubu suala hili kusema kweli kila wakati tunalipiga kelele lakini bado halijapatiwa ufumbuzi. Kama tulivyosikia taarifa hivi sasa kuna watoto ambao

wameingia katika maeneo ya Bandari bubu wameletwa kwa niaba ya kufanya biashara ambazo zilizokuwa sio rasmi. Watoto hawa tayari wamepata matatizo na pia serikali hili wameliona. Nataka kujua katika maeneo ya Bandari bubu ambayo wanapitia watu waliokuwa sio rasmi na kufanya vitendo ambavyo si vizuri vitendo ambavyo havistahiki katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli hili suala la watoto kama nilivyopata taarifa kama watoto hawa wameingia na serikali wanalifanyia kazi na tayari wametaka kuchukuwa hatua kuwarejesha wanakotoka.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu tunakuja katika ugatuzi. Mimi Mhe. Mwenyekiti, katika masuala haya ya ugatuzi wa madaraka ni vyema Serikali za Mikoa zikae tayari kupokea mabadiliko hayo. Kwani hayahitaji ufatiliaji wa kutosha pamoja na wananchi kupatiwa elimu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, suala hili kusema kweli elimu inahitajika ipatikane vizuri ili masuala haya yaende vizuri katika hali tuliyokuwa tumekusudia.

Lakini nikija katika suala la barabara za ndani. Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wezangu kuhusu suala la barabara za ndani. Mimi nitaongelea kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Kati. Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyofahamu kwamba serikali imetaka watu kuhama katika maeneo ya mjini ili kuhamia katika maeneo mengine ambayo kama mfano eneo la Tunguu tayari serikali imetoa viwanja lakini bado miundo mbinu haijafika hasa ya barabara.

Mhe. Mwenyekiti, suala la barabara kutoka Jumbi kwenda Fuoni Kibondeni. Barabara ile kusema la ukweli haijatizamwa na tayari serikali kupitia ya Ardhi imetaka viwanja waliokuwa wametoa kuona viwanja vile vinajengwa ili wananchi wahamie, lakini miundo mbinu ya barabara bado. Kwa hivyo, hii itakuwa sio hali nzuri na naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Kati iliangalie ili kwenda sambamba baina ya Wizara ya Ardhi na wao Halmashauri ili kuona barabara za ndani wanazishughilikia.

Lakini pia nije katika masuala ya uzalilishaji wa watoto hasa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba. Mimi nilikuwa nataka nije kupata maelezo katika mikoa hii miwili ambayo inaongoza katika uzalilishaji wa watoto, Wakuu wa Mikoa wamechukuwa hatua gani kuona hali hii inapungua katika mikoa yao au inamalizika kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende katika kikosi cha Zima moto na Uokozi. Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya kamati ilitueleza wazi wazi juu changamoto ya kikosi hichi kuishiwa na bajeti mapema kutokana na uhaba mkubwa wa bajeti

wanaopatiwa. Mhe. Mwenyekiti, wananchi huwa wanalalamika sana kikosi hichi kwa kuchelewa kufika katika matukio kumbe nimebaini kuchelewa kule kunasababishwa na kutopata mafuta katika magari yao ili kufika katika yale maeneo.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili kusema kweli naiomba wizara waliangalie kwa kina kuona wakati wowote hawa wenzetu wa kikosi hichi cha Zimamoto wanakuwa tayari, si tusubiri mpaka janga linatokea ndio waanza kuomba mafuta kwa vile tatizo linapokuwa linakuwa kubwa ina maana linakosa kufanikiwa vizuri.

Lakini pia nije katika kikosi hichi hichi cha Zimamoto Uwanja wa Ndege Pemba. Mhe. Mwenyekiti, tumeenda katika Kituo cha Zimamoto Uwanja wa Ndege Pemba tumeona hali ya wafanyakazi wetu hawa wana eneo liliokuwa haliridhishi. Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli wafanyakazi hawa wanakaa katika chumba kimoja ambacho hakiwatoshelezi tukizingatia hasa mle mnakuwa na wafanyakazi wanawake na sisi wanawake tunajijua mazingira yetu. Kwa hivyo, wafanyakazi wale si vizuri kukaa katika eneo moja katika kazi zao za kila siku ili kuona wanasubiri kazi ziendelee.

Lakini pia nije katika suala la Zimamoto katika eneo letu la Bandari yetu ya Malindi. Mhe. Mwenyekiti pia hapa pana eneo dogo ambalo wamepatiwa hawa vijana wetu wa Zimamoto haliwatoshi lakini pia tukizingatia kama patatokeza hatari ya moto Mwenyezi Mungu atuepushe mbali basi boti lile la haraka katika Bandari yetu ya Malindi hapana.

Kwa hivyo, naomba kupitia wizara hii Mhe. Mwenyekiti, basi wajipange vizuri kuona kikosi cha KMKM na Zimamoto wako karibu kwa sababu likitokezea hili kwa ghafla ili waweze kufanya kazi kwa haraka sio mpaka isibiriwe boti kutoka eneo husika lifike pale Bandarini tutakuwa tayari tumehatarisha hali ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika Chuo cha Mafunzo. Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/18 pamoja na mambo mengi kutaendelezwa na ujenzi wa chuo cha marekebisho ya watoto Hanyegwa Mchana. Katika bajeti iliyopita tuliwaingizia pesa naomba nimulize Mhe. Waziri leo ujenzi huo upo katika hatua gani na unatarajia kuisha lini.

Lakini nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, nije katika Kikosi cha KMKM mimi niwapongeze kwa kazi nzuri wanazofanya. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nina masikitiko yangu kuhusu vijana wa kike ambao

wamefukuzwa kazi. Mhe. Mwenyekiti, tukizingatia vijana hawa tayari tumeshawapa mafunzo, tumeshawapa elimu, na tayari wanajua kila kitu katika mafunzo waliopatiwa ya kijeshi. Basi mimi namuomba Mhe. Waziri suala hili alione na alitizame kwa imani, alifanyie tena utafiti na alifanyie kazi. Tukizingatia vijana wale ni wanawake na pia tukizingatia vijana wale ni wadogo. Kwa hivyo, namuomba tena Mhe. Waziri basi aliangalie tena kwa ubinadamu ili aone japo katika maeneo mengine wanapelekwa kushindwa kutolewa kazini moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuchangia mchango wangu huo, naunga mkono hotuba hii kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Mwakilishi wa nafasi za wanawake Mkoa wa Magharibi. Sasa naomba nimuite Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, akifuatiwa na Mhe. Bihindi Hamad Khamis nafasi za wanawake, Mhe. Mohamed Said Dimwa ajitayarishe akifuatiwa na Mhe. Mtumwa Peya.

Mhe. Hussein Ibarahim Makungu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi hii kufika katika Baraza letu tukufu kujadili hii bajeti muhimu sana.

Pia nikushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri, anajitahidi sana katika wizara hii na maendeleo tunayaona kusema ukweli. Kwa hivyo, mimi sina mashaka yoyote na bajeti ya Mhe. Waziri, kwa sababu ninamfahamu ni mzoefu sana, kwa hivyo mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini Mhe. Waziri nitasema baadhi ya mambo ili kuishauri serikali yengu sikivu, pia najua mawaziri ushauri wangu watauchukua na watauzingatia kwa ajili ya maslahi ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nianze kuvipongeza vikosi vyetu. Lakini kwanza niwape pole wananchi wote wa Zanzibar kwa maafa. Vile vile na Jimbo langu la Mtoni nao niwape pole sana, nawaambia kwamba Mwenyezi Mungu atatupa faraja na tuwe na subra katika kipindi hiki cha mvua, naamini mambo yote yatakuwa sawa tustahamili.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nivipongeze sana vikosi vyetu hasa KMKM, KVZ, Chuo cha Mafunzo na Zimamoto. Mhe. Mwenyekiti, hivi vikosi wanafanyakazi nzuri sana na wanajitahidi sana katika nchi yetu katika maendeleo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitowe mfano mmoja kwanza mdogo, pale jimboni kwangu nina kambi mbili. Kambi moja ni KMKM kwa kweli mimi nasema hawa vikosi wanatusaidia kwa mambo tofauti, nitasema kwa sababu gani. Ile hospitali yetu pale inawasaidia mpaka wananchi mbali mbali kutoka Unguja na Pemba na imo ndani ya jimbo langu, mimi nawapongeza na ninawashukuru. Hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, wanajenga hospitali na wameshaanza kuinua na hasa kinamama wajawazito wanapotaka kujifungua wanapata shida sana kuja Mnazi Mmoja, lakini sasa wanajenga wodi mpya pale.

Mhe. Mwenyekiti, niseme mimi kwa mchango wangu binafsi kwa Baraza hili nitachangia mifuko mia ya saruji kwa ajili ya KMKM, kwa jitihada zao hizo nzuri mifuko mia ya saruji nitawapelekea wapiganaji hawa kwa kweli kazi yao nzuri. Lakini pia niseme changamoto ya Zimamoto. Mhe. Mwenyekiti, Zimamoto ndugu zetu ni lazima tuwapatie Bima ya Afya kwa sababu kazi yao ni mbaya wakati wowote wanapata majanga. Kwa hivyo, naiomba serikali yengu kwa kupitia waziri iwasaidie ili wapate Bima ya Afya kwa ajili wanajitolea kwenye janga linapotokezea.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze na Wakuu wa Mikoa wote, wa Kusini Unguja, Kaskazini Unguja na Pemba yote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia nimpongeze sana Mhe. Waziri wangu wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kazi waliyoifanya nzuri. Lakini pia niseme katika wizara hii halmashauri sasa hivi imepewa na Serikali za Mitaa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niseme kuhusu barabara yangu ya Mwanyanya. Mhe. Waziri barabara ile imetiwa kifusi mara mbili. Awamu ya kwanza mwaka 2013 na 2014 imetiwa pia. Lakini sasa hivi barabara ile haipitiki Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, naomba sana iangaliwe tena barabara ile ili wananchi wetu wapate kufaidika na barabara ile kwa sababu ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 30 kifungu cha 70. Katika kitabu cha Mhe. Waziri anasema;

Kifungu cha 70

"...Mkoa umefuatilia migogoro ya ardhi 83 katika maeneo ya Dole, Kianga, Mwakaje, Maungani, Kijitoupele...".

Lakini maeneo yaliyopatiwa ufumbuzi ni maeneo 40. Sasa haya maeneo 43 yaliyobakia hayajapatiwa ufumbuzi hayajaandikwa, kusema hivi inamaanisha kuwa zitavunjwa nyumba 43 au watapatiwa hati au itakuwaje.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, juzi tumesikia mimi nilikuwa Dodoma wananchi wananipigia simu wanalalamika kwamba nyumba zao zinavunjwa na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi. Sasa mimi sifahamu kwamba hawa wanavunjiwa kwa sababu ya eka tatu wamekaa au vipi, na kama wanavunjiwa kwa eka tatu Mhe. Mwenyekiti, hilo ni kosa kubwa sana. Kwa sababu Zanzibar asilimia kubwa ni eka tatu tatu. Sehemu nyingi sana na hata hii hapa Chukwani ilikuwa eka tatu, kwa hivyo kila pahala pamejengwa, tuangalie na kama nyumba zinataka kuvunjwa Mhe. Mwenyekiti, tuwe na ushauri wawakilishi tupo tushirikishwe, hii ni hatari. Kumvunjia mtu nyumba ni sawa sawa na umeshamuuwa sasa hivi na hawa wananchi wetu ni wapiga kura wa nchi hii.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, tuangalie zahma hii iliyotokezea Kianga sijui, naomba Mhe. Waziri unieleze vizuri kuhusu hii kuvunja nyumba za hawa watu imetupa sura mbaya hasa sisi wana CCM na serikali yetu yote. Kwa hivyo, naomba unipe maelezo mazuri sana Mhe. Waziri ili tupate kufaidika na mimi na wananchi wangu wa Zanzibar.

Nikiendelea kuchangia Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kuna wafanyabiashara wengi katika maendeleo yetu ya Zanzibar kutaka mji uwe mpya, tunataka kujenga *mall* Darajani na Michenzani. Lakini Mhe. Mwenyekiti, niseme kitu kimoja tu, hawa wafanyabiashara ni wengi sasa hivi hawana maduka wala hawana pa kwenda, na wana mpango wa kwenda pale Saateni kufanya biashara tuwapeleke pale, ili wauze biashara zao.

Mhe. Mwenyekiti, niseme suala hili la kuwaondosha hawa wafanyabiashara hawa ni wadau wetu, serikali haiwezi kwenda bila kulipa kodi Mhe. Mwenyekiti. Sasa Mhe. Waziri wa Fedha hebu tuliangalie hili, hawa wafanyabiashara mnawapeleka Saateni na Saateni mazingira yake yako vipi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kwenye kitabu wameandika katika ukurasa wa 32 kifungu cha 74 kwamba Baraza la Manispaa la Mjini limefanya kazi ya upimaji, kuweka alama za mipaka na kifusi Mhe. Mwenyekiti. Sasa wafanyabiashara hawa utawapeleka pale kuna kifusi na mvua hizi biashara gani itafanyika na wafanyabiashara hawa tunahitaji kodi sisi watulipe *ZRB*, *TRA* na kuna *VAT* asilimia 18 wanalipa hawa. Kwa hivyo, mazingira yao tuwarekebishie kwanza ili pale wakipata maduka wale wafanyabiashara na wanunuzi wanakuwa wanafaidika kwa mazingira mazuri. Lakini ukiangalia

pale hapako kwenye hali nzuri, hasa ikija mvua, vumbi kubwa siku ya juakali na wala hakuna lami. Kwa hivyo, mimi naomba sana tuwawekee mazingira mazuri Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 27 kifungu cha 64 kuhusu Serikali za Mitaa zimepewa mamlaka baadhi ya wizara hizi. Mhe. Mwenyekiti, hii sheria ni mpya hapa Zanzibar ndio kwanza tunaianza sasa hivi. Sasa mimi niseme Mhe. Mwenyekiti, katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mimi ni Mbunge wa Utawala wa Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, nimetembea Tanzania nzima na kamati yangu ya Tamisemi, kukagua na kuangalia maendeleo kwenye mkoa tofauti. Nimefika Mbeya, Iringa, Tanga, Morogoro, Katavi ni mikoa mingi Mhe. Mwenyekiti, kukagua miradi ya maendeleo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa maendeleo. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, ni changamoto kubwa sana Wakuu wa Mkoa kuendesha hizi Serikali za Mitaa, inakuwa ni changamoto kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi sisi kodi wanakusanya *ZRB* na *TRA* tunawashukuru sana pesa tunaziona walipwe mishahara mizuri. Watakapokuja kupewa Serikali za Mitaa Mhe. Mwenyekiti, tutakuja kuambizana hapa hapa hizi pesa zitashindwa kukusanywa mimi nakuambia. Sasa changamoto hii kwanza wangekwenda kujifunza kwa wenzetu, wangekwenda Mbeya wangeiona hali kuna changamoto baina ya *TRA* na Serikali za Mitaa kukusanya kodi sasa hivi, wanashindana hata bajeti haipatikani za mikoa yao. Kwa hivyo mimi naomba sana tuliangalie hili na tujifunze kwa undani. Kama sasa hivi serikali imewape Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Lakini pia kuna changamoto zake. Wizara ya Afya kuna watu karibu 2,000 wawalipe wao Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya watu 1,000 halafu na vituo 108 Zanzibar, kwa Unguja na Pemba washughulikie Serikali za Mitaa. Halafu elimu karibu watumishi 2,000 na *primary school* zote washughulikie Serikali za Mitaa. Halafu tukije kwenye kilimo babu shamba 500 wawashughulikie Serikali za Mitaa, ukija kwenye mifugo. Mimi nawaomba mawaziri msikae kimya mseme hizi changamoto mlizokuwa nazo mnakwenda kuwapa hawa ndugu zetu je, itakuwaje huku mbele, ushakwenda kulisha watu kwenye maeneo yetu. Kwa hivyo, mimi nawaomba sana mawaziri msikae kimya mseme mliokuwa nayo Wizara ya Afya muhimu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali muhimu. Kwa hivyo, naomba mseme kwa sababu changamoto ya Serikali za Mitaa zinakuwa na mashaka yake, mimi ni mjumbe wa kamati najua vizuri nimeshatembea huko Bara ndio system hiyo, kila siku matatizo sana kwenye Serikali zao za Mitaa baina ya kodi na kuendesha mikoa ile.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee katika suala hili zima la utalii. Mhe. Mwenyekiti, juzi hapa katika Ofisi ya Rais tumeona Djibouti wamekuja kujifunza hapa utalii, wamekuja wameona Zanzibar wameendelea vipi kiutalii, tumepiga hatua kwa miaka yote kuanzia miaka ya nyuma mpaka leo tumefika hapa na tumekubali utalii Zanzibar wenyewe, na wageni wanakuja. Hakuna mgeni hata mmoja mpaka leo tumefikia hatua hii karibu asilimia 80 ya wageni wanaokuja Zanzibar wanaipenda Zanzibar na wanaendelea kuja, tunatarajia tena kipindi hiki wageni karibu zaidi ya 200,000 watakuja Zanzibar kutembea. Kwa hivyo, kila siku zinavyokwenda mbele tunazidi kuendeleza utalii wetu na serikali inapata fedha nyingi kwenye utalii. Kwa hivyo, mimi niipongeze serikali kwa juhudi zao, wameona utalii ni muhimu kuwafurahisha wageni wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasikitika sana Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kupiga marufuku upigaji wa muziki. Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kitu kimoja haya mambo ya mziki ni sanaa, ukiacha sanaa ni ajira kwa vijana wetu. Leo unakwenda kuzuia huu muziki, kwani muziki una taratibu gani mbaya, yeye anakwenda kuzuwia anasema muziki upigwe siku tatu tu, na siku tatu zenyewe anatoa mwisho saa 6:00.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kumbi tofauti Zanzibar na dunia nzima, kuna kumbi za nje na kuna kumbi za ndani ambazo *disco track* zimejengwa *professional* sauti hazitoki nje. Sasa kuna watu wamesha-*invest* kwenye shughuli hizo. Mimi mmoja na-*declare interest* yangu nimefaidika suala la muziki, na- *declare interest* yangu nimefaidika katika suala la muziki, sitowi shukrani kwenye muziki, na vijana wengi wamejifunza suala la muziki. Mimi nimefika Canada kwa kuwa *professional* yangu ni ya muziki, nimekwenda mpaka Canada na Marekani kwa kuomba *VISA* kutokana na muziki, sijaelewa VISA kwa sababu ya jambo jengine ni muziki tu. Kwa hivyo, nasema huu muziki usichukuliwe tasfiri nyengine. Sasa hivi Nigeria ukiwatizama wasanii wao ni *International.* Wizkid, ukimtizama Davido, ukimtizama Tekno hawa ni wasanii wa Nigeria ni *International* duniani na wanaingiza kodi kubwa katika nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, juzi Bungeni alisema *Professor Jay* Diamond anadaiwa alipe shilingi bilioni 400 kodi, mwanamuziki anaambiwa bilioni 400 alipe. Kwa hivyo, tusiwadharau wana muziki wa sanaa kwa fani hii wanaingiza fedha nyingi na ni ajira kwao Mhe. Mwenyekiti. Lakini hapa Zanzibar tuna matamasha karibu mawili yanafanyika kila mwaka. kuna (*ZIFF) Zanzibar International Film Festival* na kuna Busara ambayo dunia nzima wanajua *ZIFF* inafanyika mwezi wa saba na Busara inafanyika mwezi wa pili, na wageni

wanajua na wanakuja kwa ajili ya matamasha hayo, kuja kuangaliza Zanzibar utamaduni wetu, ngoma zetu na tunaingiza fedha nyingi wageni wakija. Hoteli watakula na watatumia. Leo Mkuu wa Mkoa anazuwia anasema mwisho saa 6:00 Mhe. Mwenyekiti, hii sio kweli.

Mhe. Mwenyekiti, juzi kulikuwa kuna *Fashion Show* Ngome Kongwe, Mkuu wa Mkoa alikuwa sio mgeni rasmi pale, alikuwa Waziri wa Habari, Utalii na Michezo ndio mgeni rasmi pale. Lakini kwa bahati mbaya au nzuri na kwa sababu waziri wetu ni makini sana wa habari akafika mpaka nje kule, kufika nje akaambiwa Mheshimiwa humu ndani usiingie, humo kuna hali sio nzuri ya mavazi, hawa *Fashion Show* watavaa mavazi ambayo sio utamaduni wetu. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo alivyokuwa makini kaondoka akenda zake nyumbani. Akapigiwa simu Mkuu wa Mkoa pale na *Chief of Protocol* akamwambia hapa sina mgeni rasmi. Kwa hivyo njoo wewe ukae Mkuu wa Mkoa. Mkuu wa Mkoa akenda kukaa kwa mgeni rasmi pale akaona ile zahma yote ya vile viguo walivyovaa sio utamaduni wetu Wazanzibari. Mimi mwenyewe nimekwenda na mke wangu saa 6:00 za usiku tumevaa vizuri, kaja *Chief of Protocol* kunipokea nje, akaniambia Mhe. Bhaa twende. Akaja mtu mmoja mwananchi wangu wa jimbo langu akaniambia sikiliza Bhaa usiingie ndani hakuna utamaduni mzuri huku ndani kwa ajili ya nguo. Mimi nikaondoka zangu, lakini Mkuu wa Mkoa wetu hajui kutofautisha haya mambo akenda akakaa mpaka saa 9:00 usiku na akawapa muda mpaka saa 9:00 muziki ulipigwa nje pale wala sio ndani, lakini kwa vile yeye yupo kachukua sheria ya Serikali za Mitaa sijui kama yeye ndio anaweza kufanya hivyo.

Kwa hivyo, naomba ushauri tufanye nini kwa suala hili la muziki kwa sababu madaraka mengine anachukua sio *size* yake Mheshimiwa. Lakini pia juzi kenda kwenye ma- *discotheque* yote ya Unguja akawachukua ma-DJ kawatia ndani akiwemo *manager* wangu maskini ya Mungu Muharami namuheshimu baba yangu kamuweka ndani. Mtu ana sukari, *pressure* kamweka ndani masaa 12 nakwenda kumuomba nampigia simu Mkuu wa Mkoa hataki kumtoa, anasema mimi simtoi.

Juzi kamuweka ndani *DJ* mwengine masaa 12 hivyo hivyo, mpaka ananiambia wewe Mheshimiwa omba radhi, nikamwambia niombe radhi kwa sababu gani na sisi tunalipa kodi, leseni kila kitu, anasema simtoi. Nampigia simu zaidi ya mara tatu, tangu saa 9:00 mpaka asubuhi hapokei simu. Kwa nini afanye hivyo?

Juzi kamchukua tena Jumamosi yule msanii mdogo masikini mtu mwenye ulemavu, hawezi hata kwenda yule Sadiki anaimba taarabu masikini ya Mungu, kamchukua kamtia ndani hapo Mazizini Polisi, kamuweka ndani mpaka saa

tatu asubuhi, akaja mwanasheria akenda pale, polisi wakamuomba radhi yule msanii masikini ya Mungu Sadiki anatafuta riziki yake kwa ajili ya kuimba tu. Leo tutizame hawa sio wahalifu hawaibi kitu, hawampigi mtu, wanafanya kazi kwa riziki zao, wanaishi na watoto wao na familia zao, leo unamchukua unamtia ndani atakula wapi mlemavu yule masikini ya Mungu. Hili jambo watu waangalie serikali haya madaraka ya Serikali za Mitaa Wakuu wa Mikoa wanaweza kuchukua vibaya sana.

Kama Bara, kuna mambo mengi sitaki kusema Mkuu wa Mkoa amechukua hatua hizi kwa sababu mamlaka wanayo. Sasa lazima tuangalie Zanzibar ni nchi ndogo waziri mwenye dhamana yupo, na mimi nataka kujua hili suala la muziki la sanaa mwenyewe Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na yeye nani mwenye dhamana. Naomba Mhe. Waziri unambie uliweke sawa hili. Kwa sababu ukiangalia hapa tuna mambo mengi ya kuangalia mambo haya ya muziki, lakini kuwatia ndani kuna haki za binadamu za nchi hii, tumesaini mkataba sisi wa haki za binadamu, leo unamchukua unamtia ndani masaa 12 mtu anaumwa hujali. Kwa hivyo, mimi naomba sana suala hili la Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba iundwe Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi imchunguze Mkuu wa Mkoa kazi anazozifanya kwa maslahi ya Zanzibar taifa hili, au kwa maslahi yake mwenyewe. Kwa hivyo, naomba Kamati Teule hiyo kama itaundwa Mheshimiwa mimi nitatoa posho wajumbe hao wote nitawalipa mimi, ili wamchunguze na ripoti ije hapa kuangaliwa. Wakuu wa Mikoa wote mimi nawapongeza wa Kaskazini nampongeza sana kwa jitihada zake kubwa za Ijitimai ambayo iko kesho kutwa, anavyojitahidi tunashirikiana mimi na yeye kuifanikisha Ijitimai ile. Kwa hivyo, mimi nampongeza Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Mhe. Vuai anajitahidi sana na kwa ushirikiano wake mzuri kabisa kwa kuweza kufanikisha suala hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba umalizie una dakika tatu zilizobaki.

Mhe. Husseni Ibarahim Makungu: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyojua kwa Serikali za Mitaa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wote ni makada wa CCM, kwa hivyo ni lazima waangalie na hawa watu wa muziki wote ni wana CCM wapiga kura wetu. Kwa hivyo, naomba sana tuangalie kuwapa nafasi wapate kufanyakazi zao vizuri, tusiwatie ndani kwa sababu ya muziki sio wahalifu wala sio wezi. Kwa hivyo, naomba sana tuangalie suala hili na Mhe. Rais pia namuomba tuliangalie sana suala hili, tusichukuwe sheria mkononi tukafanya mambo ya ajabu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nimalizie katika maeneo ya jeshi. Pia Mkuu wa Mkoa anaingilia maeneo ya jeshi. Majeshi wana maeneo ya kambi zao na mipaka yao na wana starehe zao ndani ya kambi. Sasa leo unakwenda kumzuwia jeshi asifanye starehe yoyote, jeshi haruhusiwi kuja uraiani kukaa na raia, kwa sababu hawana ubinadamu mzuri kwa walivyojifunza. Kwa hivyo unakwenda kuwaingilia jeshi, jeshi wakafanye starehe wapi na wata- *enjoy* wapi, wakati binadamu wale wanakesha usiku na mchana kwa kutulinda sisi tunaolala majumbani mwetu. Kwa hivyo, mimi naomba sana Mkuu wa Mkoa mamlaka yake yajulikane, na hizi wizara walizopewa ni tatu au nne wako kwenye majaribio tu sio zote, nyengine amuachie dhamana waziri mwenyewe afanye kazi yake.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano, naomba dakika mbili, nitoe mfano kwa ubinafsi wa Mhe. Mkuu wa Mkoa. Jana kule Ngalawa kuna *Spice Club* katoa kibali kawapa wafanye kazi wapige, lakini nilimuuliza mimi hapa nje, wewe umewapa kibali kule *Ngalawa Club* wafanye kazi wamefanya kazi vipi, akasema wale wana-*function* hawafanyi kazi wana- *function*. Lakini matangazo yanatoka kiingilio shilingi 10,000/- wanawake bure. Sasa tunafanya nini jamani, huku biashara wanafanya wanalipa kodi, wana leseni wanaambiwa wasifanye lakini wale kule wana-*function*. Sasa mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, nimemuangalia sana Mkuu wa Mkoa, lakini kuna matatizo ni lazima iundwe Kamati Teule imchunguze kiundani ili tuweze kujua ripoti yake ije hapa Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako kama itawezekana basi na mimi naomba tuunde hiyo kamati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, halafu suala la madawa ya kulevya. Katika suala la madawa ya kulevya tume-*fail* Zanzibar. Ukiwatizama Wakuu wa Mkoa wenzetu Tanzania Bara, ukimtizama Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam tumeona na wajumbe wamesema, hatuwajui mpaka leo wanaoingiza madawa ya kulevya kwa nini tunawaficha, wanakamatwa watu wa muziki wanatiwa ndani dunia nzima inajua, lakini madawa ya kulevya watu hawatajwi wala hatuwajui. Mimi mwenyewe mjumbe wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, nilikwenda kwa Mkuu wa Mkoa kutaka ripoti iliyofikia ya madawa ya kulevya umekamata watu wangapi, ananiambia ripoti ipo, ripoti ipo mpaka leo mimi sijui. Mimi nakwenda kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa naulizwa kule Zanzibar mmefikia wapi kuhusu madawa ya kulevya, isitoshe Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda Dar es Salaam, kama unataka msaada kutoka kwetu mimi na Kamanda Siro tutakuja Zanzibar kukusaidieni. Lakini hakuna mashirikiano yoyote sina cha kusema kupeleka na kuwaambia tumefikia wapi Zanzibar nani anauza madawa ya kulevya na nani kakamatwa hatujui mpaka leo. Mimi ni mjumbe wa kamati ya viongozi wakuu na hiyo tume ya madawa

ya kulevya iko chini yangu na kule Dar es Salaam ninakokwenda naulizwa, Zanzibar mmefikia wapi sijui mjumbe wa Kamati ya Viongozi Wakuu hajui.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hussein kwa mchango wako.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mheshimiwa nakushukuru. Mimi naunga mkono hotuba ya baba yangu, kaka yangu, Waziri wangu makini Mhe. Haji Omar Kheir asilimia mia kwa mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hussein kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Bihindi Hamad Khamis nafasi za wanawake, akifuatiwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kama muda utaruhusu nimuite Mhe. Mtumwa Peya na Mhe. Jaku ameniomba kwa dakika tano kama muda utakuwepo nitampa hizo dakika tano ahsante Mheshimiwa endelea.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia leo hii nikaweza kuchangia Wizara hii, Mhe. Mwenyekiti kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Kusini Pemba, nimpongeze DC wa Wete, DC wa Micheweni, DC wa Mkoani na Chake. Niwapongeze Makatibu wa Halmashauri zote za Mikoa miwili ya Pemba, niwapongeze Wakurugenzi wa Mikoa miwili ya Pemba pia niwapongeze na watendaji wote wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba na Kaskazini Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja Baraza la Mji Wete niwapongeze watendaji wa Baraza la Mji Wete kwa utekelezaji wao wa kazi na ufanisi wa kutosha, pia nimpongeze Mkuu wa Mkoa kwa kuweza kusimamia majukumu yake ya Afisi yake ya Mkuu wa Mkoa pamoja na utekelezaji wa Wilaya zake zote za Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwenye utekelezaji wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni wameeleza kuwa wamejenga ukumbi wa Mikutano Wilaya ya Micheweni. Mhe. Waziri nilikuwa nataka kujua ni mkandarasi gani aliyejenga ukumbi ule wa Halmashauri ya Micheweni, na ni kiasi gani ya fedha ambazo zilitumika kuanzia *foundation* mpaka kufikia hatua ile iliyofikiwa. Pia Mhe. Waziri naomba unieleze huyu mkandarasi analipwa kwa

kiwango gani na kwa muda gani na kiwango gani ambacho kimefikia hadi muda huu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele niende kwenye JKU. JKU ilianza zamani sana na takriban kuanzia mwaka 1981, majengo yale yaliyopo kwenye Mkoa wa Kaskazini Pemba kwenye JKU Msaani yalianzia hapo. Je, Mhe. Waziri una mpango gani wa kuweza kuyatengeneza majengo yale ili vijana wetu waweze kukaa kwenye haiba nzuri.

Mhe. Mwenyekiti nikiendelea mbele niende kwenye ugatuzi wa madaraka niende kwenye vitambulisho na kadi za Mzanzibari imeunganishwa hapa kwenye vizazi na vifo talaka na ndoa na mambo yote ambayo yanahusiana na haya. Je, Mhe. Waziri una mpango gani wa kutoa taaluma kwa wananchi ili kujua ugatuzi wa madaraka ni kitu gani na ni maeneo gani ambayo naweza kutoa mafunzo haya.

Mhe. Mwenyekiti kwa kuendelea mbele niende KVZ Micheweni takriban miaka 11 kuna jengo ambalo sasa hivi ambalo linajengwa la Afisi ya KVZ, Je, Mhe. Waziri ni mkandarasi gani anayejenga jengo lile na ni kiasi gani ya fedha ambazo zimetumika hadi leo hii na ni awamu ngapi ambazo mkandarasi yule anapewa kwa kujenga jengo lile. Mhe. Waziri kwa sababu ya kusema hivyo jengo lile ambalo linajengwa hadi leo Mheshimiwa halijaonyesha mfano wowote na halijaonyesha kuwa jengo lile vijana wetu wale au ofisi ile wataweza kuhamia kwa wakati. Mhe. Waziri utakapokuja kutoa majumuisho unieleze kwa kina ili wananchi wale au KVZ walioko Mkoa wa Kaskazini Pemba hususan Wilaya ya Micheweni waweze kujua ni wakati gani jengo lile litamaliza.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele niwapongeze tena Wakuu wa Mikoa kwa usimamzi wao wa maafa ambayo yalitokea kwenye Mikoa yetu miwili na kuweza kujumuika pamoja na wananchi ili kuweza kuwapa matumaini ya kuishi na matumaini ya kuendelea na kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Mhe. Mwenyekiti, ahsante *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Bihindi Hamad Khamis wa nafasi za wanawake sasa naomba nimuite Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa jimbo la Mpendae, akifuatiwa na Mhe. Mtumwa Peya na Mhe. Jaku ajitayarishe kwa dakika tano.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushkuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini niende moja kwa moja leo nataka nianze kwa aina ya kipekee, nataka niwape pongezi wote kwa pamoja maana nikizungumza hivyo Waziri, Naibu Waziri, Mkatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, pamoja na makamanda na wafanyakazi wao wote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti nimetoa pongezi hizi kwa pamoja kwa sababu ya kazi nzuri sana ya Serikali yetu inayofanya na mimi ninaamini kama tutaendelea hivi baada ya miaka miwili wapinzani watatusikia tu tutaenda vizuri, kwa sababu Wakuu wa Mikoa wote na Wakuu wa Wilaya tumechagua majembe yanayofanya kazi vizuri sana hongereni sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye mapitio ukurasa wa 19 kwenye ukurasa wa 19 katika namba ya pembeni 47 naomba ninukuu:

> "Mheshmiwa kikosi cha Zimamoto na uokozi kimetoa huduma za Zimamoto na uokozi katika matukio 370 yaliyoripotiwa katika vituo vyote Unguja na Pemba, na katika matukio hayo kikosi kimefikia kwa wakati katika matukio 250 na katika matukio 120 haikuwahi kutokana na changamoto mbali mbali zilizojitokeza, kama kuchelewa kupata taarifa".

Sasa mimi nilikuwa naanza kupata ukakasi ikiwa matukio 250 tumefanikiwa 120 hatukufanikiwa ukitizama 120 ukiongeza 5 inakuwa nusu kwa nusu, sasa nataka kujua Mhe. Waziri utakapokuja ufanisi uko wapi hivi tunafanya tathmini au tumeandika tu nataka tufanye tathmini na Mhe. Waziri aniambie basi tulikuwa tuna moja lakini tumekosa hichi, lakini tumekosa hichi. Ukosefu wa taarifa hainipi sana akilini kwangu.

Mhe. Mwenyekiti, niende tena kwenye kitabu hichi cha mapitio ukurasa wa 28 kwenye No. 66 ambayo matukio ya udhalilishaji katika mikoa yetu, mimi nimefika pahala nataka kujua hivi hawa watu wanaodhalilisha watoto, wanaodhalilisha kinamama na wengine wana akili timamu? Ningeomba Serikali yangu niishauri sana kwanza mtu huyu tukishakumkamata tu tumpeleke akapimwe akili ana akili timamu. Lakini tukikuta ana akili timamu tuanze sasa kubadilisha sheria yetu, kwa sababu sheria hii imekuwa inawapa *loophole* wadhalilishaji sana, ukienda katika Mahakama ya Mkoa ina *limit*, Mahakama ya Wilaya ina *limit* lakini na Mahakama ya Rufaa ina *limit.* Sasa naona tu Mhe. Waziri atakapokuja aniambie hapa hawa wote wamepimwa akili watu wangapi maana yake hawa hawana akili. Haiwezekani kama mtu ana akili

zake halafu anakwenda kumdhalilisha mtoto mdogo mtoto wako ndio mtoto wa mwenzio na mtoto mwenzio ndio mtoto wako haiwezekani.

Mhe. Waziri hapa wa Vijana na watoto ananisikia lazima tubadilishe sheria hizo si hivyo tutafika pahala pabaya na nadhani mimi nafikiri tulikuwa haya mambo hatuyashughulikii lakini sasa tunayashughulikia ndio tumepata wingi wake, tumepata kujua wahalifu hawa wanafanya kazi gani. Mhe. Waziri ikifika pahala tukiwa watoto wetu wanadhalilishwa tena sehemu nyeti ambazo tunategemea ndio wanalelewa inakuwa hali ngumu sana, mimi naomba Serikali ichukue hatua kubadilisha sheria hii mimi naona hawa hawahitaji kufungwa wanahitaji kuwekwa gerezani maisha mpaka wafe wasitoke. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi sasa nakwenda moja kwa moja katika bajeti hii tunayozungumza moja ambalo nataka kulizungumza Serikali katika mapitio imesema imenunua gari 17 gari za zimamoto na thamani yake, twambie basi ilifuata angalau taratibu za manunuzi, nataka kujua tu.

Sasa niende kwenye Manispaa moja kwa moja nitaanza na hapo lakini Manispaa nataka kujua *packing* ambazo zipo zile ni muda gani, kutoka muda gani muda gani zinalipiwa lakini na makusanyo yake yanakuwa Shilingi ngapi kwa mwezi ili tuweze kujua. N ataka nishauri kuweza kuweka *electronic device* angalau basi tu-*charge* tukiona tunatumia vifaa vile kuliko kuweka risiti zile za *manual* tukiweka risiti za *manual* tutapigwa sana, nataka kujua hilo ili tuweze kufahamu. Lakini pale pana wafanyakazi wafanyakazi wale juzi nilikuwa nawauliza bila ya kujua wa sehemu mbali mbali wewe unalipwa kiasi gani na nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwaona wafanyakazi wa mshahara wa chini kwa kuwaongezea mshahara, yule mama kaniamba mimi nilikuwa napata laki moja na nusu, sasa napata laki tatu.

Lakini ukitizama muda wake wa kufanya kazi amefanya kazi miaka 30 nilikuwa najiuliza sana hivi kulikuwa hakuna *increment* anayoweza kupata yule au walikuwa wanajilipa wenyewe na hao maafisa utumishi wamekuwa wachoyo kuwaongeza angalau posho la kila mwaka. Sasa nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri ufanye mapitio katika mishahara yao ili kuona je walilipwa *increment* watu wale au hawakulipwa kwa sababu naona bado mishahara iko chini sana inaonekana hawastahiki kufanya hivyo nikuombe sana Mhe. Waziri nakujua unaweza ukalifanya hili jambo ukawaonea huruma watu hawa.

Lakini nije kwa Waheshimiwa Madiwani Mhe. Mwenyekiti, waheshimiwa madiwani ni waheshimiwa kama sisi wanapigiwa kura kama tunavyopigiwa

kura sisi, wanapigiwa hodi kama tunavyopigiwa hodi hii mara yangu ya pili nataka kusema hawana mshahara utaitwa mshahara bila ya pesa, utaitwa Mheshimiwa bila ya pesa haiwezekani angalau basi Serikali iwaonee huruma iwaongezee posho au ijue inawalipa mshahara.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye safari ya Mstahiki Meya hivi karibuni alifanya safari ya kwenda Ujerumani na katika picha moja ambayo nimeiona alipelekwa sehemu moja ya *Botanic* ambayo kuna miti ya aina na asili mbali mbali. Katika kikao cha bajeti kilichopita nilimuomba Mhe. Waziri tena namshukuru sana alinikubalia kutumia vijana wetu kutumia lile eneo la sehemu ya bustani ya Migombani, Mhe. Waziri nikushukuru sana kwa kutupa ruhusa ile kwa kukaa na Mhstahiki Meya. Lakini na sasa ningekuomba ufanye ziara baada ya mwaka uone mafanikio gani tuliyoyapata pale na miti gani tulipanda iko siku mstahiki Meya wa Ujerumani atakuja kurudisha ile ziara na nadhani unaweza kumpeleka Migombani kuona *botanic* nzuri ambayo imefanyika, nikusihi sana Mhe. Waziri ufanye ziara na vijana wale wanatamani sana kukuona uone miti ya asili iliyopandwa na miti mizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti nije kwenye miradi hii ya ZUSP kwanza mtaro unaotoka kwa Binti Amrani niliwahi kuzumia mara moja nikasema mimi na wananchi wangu tutafanya maandamano ya amani sana na tutajifunga kitambaa cheupe kabisa. Kwa sababu mtaro unatoka kwa Mchina mwanzo unaoingia kwa bint Amrani unatuzidishia maji, lakini si kutuzidishia maji tu hata nyumba baadhi zinaathirika sana zinakatika kabisa *foundation* zinafanya hivi ni mtaro mkubwa lakini sasa turudi tuangalie. Mimi niiombe Serikali ijitahidi sana kuumaliza mtaro ule na tuone jinsi gani tutaweza kuondosha maji hapa katika nyumba za bint Amrani maafa yale yametupata sana, ndio maana tukasema basi tulijadili jambo lile la dharura. Mhe. Waziri nataka uje uniambie hapa hapa ni lini mtaro ule wa bint Amrani unaweza kumalizika.

Mhe. Mwenyekiti, nije barabara kutoka Mchina mwanzo kupitia Mpendae mpaka Jang'ombe kuna semu ya Lofi na sehemu ya mbele kidogo ya Jumba la Vigae ambayo pana mashimo pale ya karo zile bado hayako sawa, na siku moja nataka niseme na wananchi wanisikie sasa hivi tunaweza tukapata hasara kubwa ya ajali. Kwa sababu baada ya kuharibika ile miundombinu ya chuma tukaweka zege sasa hayajakaa vizuri na gari pale ikija mvua ndogo tu balaa linakuwa kubwa sana. Mhe. Waziri nikuombe sana ufuatilie suala hili liweze kwenda sawa.

Lakini nije katika Manispaa au ugawano wa manispaa zetu Magharibi 'A' Manispaa ya Mjini, pamoja na Manispaa ya Magharibi 'B' Mhe. Manispaa

ilikuwa ikimiliki masoko mawili kabla ya kuwa zile bado Halmashauri. Sasa leo Manispaa zile zinadai kuwa zipelekwe katika Manispaa zao sasa huyu Manispaa mama atabaki na nini. Wakati na yeye anafanya biashara kule na analipa na yeye ndio mwenye kitovu kile niseme moja tu nataka nishauri. Manispaa ya Magharibi 'A' na Manispaa ya Magharibi 'B' Manispaa hizi zitafute eneo la kujenga lakini huyu mama wa manispaa maana yake Manispaa ya Mjini iweze kuchangia nao wapate chochote, lakini wakubali ili hizi zilipwe tu kama yeye ni mfanyabiashara wa pale.

Mhe. Mwenyekiti sasa niende katika vikosi vyetu nakwenda moja kwa moja kwenye kikosi cha Mafunzo. Mimi leo nataka nishauri sana jinsi ya kutumia rasilimali tulizokuwa nazo, Chuo cha Mafunzo kina rasilimali kubwa sana kwanza nilitaka kuona kuna kitu kinaitwa *double allowance* ambazo tunawalipa askari wetu, moja askari analipwa *allowance* ya chakula akiweko kazini na chakula tunampa, lakini yule asiyekaa zamu analipwa sawa sawa na *allowance* zile zile ambazo analipwa hebu tulitizame tena hatufanyi *double payment* na kwa nini tusiangalie anayeingia kazini kipindi gani, lakini na kipindi gani haingii kazini tukaangalia zile *allowance* zao za chakula tukawapa ili pesa nyengine tukaweza kuzihifadhi.

Lakini jengine nataka kusema kambi ya Mafunzo ya Bumbwini ina rasilimali sana na hili muda mwingi ninapochangia nakuwa nasema na sichoki kusema kwa sababu siku moja Mhe. Waziri utapekua *Hansard* zangu na utaangalia manufaa makubwa ambayo tunayoyapata. Moja kuna sehemu ya pwani kubwa ya nje pale ambayo kuna mabwawa ya kufugia samaki, sasa mabwawa yale lazima tuyashughulikie sijaona hata kutenga pesa humu kusema tunayashughulikia na mabwawa yale yanatoa samaki wengi sana. Kuna Mheshimiwa MBM mmoja siku moja kabla ya kuteuliwa tulikwenda pale tukapata chakula cha asubuhi na samaki wengi sana, sasa nataka kusema tujitahidi kufanya kila tuwezalo mabwawa yale tuweze kuyaunda vizuri na kupata samaki wengi, na tukifanya vile OC hizi ambazo tunawaingizia wenzetu Magereza zitapungua katika jambo la vitoweo lakini jambo la chakula.

Jengine tufanye *rice irrigation* katika zile sehemu ambazo kama kuna kambi moja tuweze kufanya *rice irrigation*, tuone basi chakula kile tunazalisha kila mara, hii OC ambazo tunaweza kuzitia tunaweza kutumia kwa mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo linanipa ukakasi Mhe. Waziri ni nyumba za wafanyakazi za sehemu mbali mbali Pemba na Unguja hazipo katika hali nzuri. Kuna wengine wanapewa chumba kimoja na watoto. Inasikitisha lakini kuna

wengine wanaingia usiku mvua kama hizi inabidi wavae ma- *rain coat* ndio walale wapate angalau ajihifadhi, ningeomba sana tujitahidi.

Mhe. Mwenyekiti, niingie Kambi ya JKU niipongeze sana kwa kazi kubwa ambayo wanayoifanya. Lakini nayo bado inasehemu ndogo sana hasa Pemba, makaazi hayapo vizuri, na askari ni kidogo kule. Wakati wa kilimo ningependekeza tuhamie kule angalau tufanye *operation* ya kuwapeleka askari na kufanya kazi ile ili tupate mazao mazuri kule Pemba kama zana halisi ya kuundwa kwa jeshi hili ningeomba sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye KVZ niwapongeze na wao kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanayoifanya. Pia niwapongeze kwa kuanzisha kiwanda cha viatu katika eneo lao. Wamefanya ubunifu mkubwa na hongereni sana. Nataka kujua Mhe. Waziri ni kiasi gani pesa za malindo zinazopatikana kwa mwaka, na ni kiasi gani zinatumiwa kwa chakula cha askari wanapokuwa lindoni na kiasi gani zinasaidia mafuta na kiasi gani zimepangiwa. Nimeona huku mmewapangia shilingi arubaini na tano milioni kwa kuchangia. Mimi naona kwa kikosi hichi kinafanya kazi za ulinzi kubwa fedha hizo ni kidogo mno. Nilitaka nijue na nione matumizi halisi yanakwendaje.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kikosi cha Zimamoto nikipongeze kwa kazi zake pamoja na kusema bado kinatakiwa kifanyiwe tathmini ya maandiko yao waliyoyaleta. Niwapongeze sana kwa kazi kubwa wanayoifanya, kilio changu kikubwa ni kwenye kambi ile ya Wete. Wanaishi katika hali ngumu sana na sio mazingira halisi ya kuishi mwanadamu na hili nalisema mara ya pili Mhe. Waziri. Nataka ukija unambie ni mikakati gani imepangwa mbali ya kile kiwanja kilichokuwa pembeni pale tumesema tunakijenga. Lakini pia ni mikakati gani ya kuweza kuondoa shida ya wapiganaji wetu pale panapoweza kuwaondoa.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie Kikosi cha KMKM na wao wamefanya kazi kubwa sana, lakini kambi nyingi za Pemba ziko mitaani ambapo askari wale wanaweza wakaumia mara moja kwa siasa za kule kwetu Pemba. Niwaombe sana washughulike na jambo hili ili kuona kambi zote kwanza zinapatiwa hati miliki na zinakuwa mbali na wananchi lakini nyengine wananchi wanapita pale kati kati ya Kambi inakuwa si vyema kwa wapiganaji wetu, tujitahidi sana.

Mhe. Mwenyekiti, KMKM la mwisho nataka nijue ni kiasi gani inapata faida katika Bima ya afya kwenye hospitali yetu ya KMKM. Jengine ninalotaka kusema hili nalishauri kwa mara ya pili, vikosi hivi vyote vinafanya kazi kubwa. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) alianza kulidokeza pale na

tusione sasa hivi tuko kwenye amani kubwa lakini tunapoingia katika uchaguzi Zanzibar inabadilika na hawa watu ndipo wanapofanya kazi kupita kiasi.

Mhe. Mwenyekiti, niombe sana askari wote waweze kupatiwa Bima ya Afya pamoja na wanafamilia wao. Hii italeta afya mshahara wenyewe umeongezwa juzi lakini baada ya kuongezwa na huku biashara zimeongezwa bei hawawezi kukidhi jambo hili. Niombe sana Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Waziri ukija hapa uniambie na kwa hili Mheshimiwa sitounga mkono hoja yako kama hujaniambia hasa tuna mpango gani wa Bima ya Afya kwa askari wote wa vikosi vyote hivi vinavyoendelea. Nikuombe sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Ugatuzi D by D, ugatuzi ni mzuri sana kwetu lakini ninachotaka kusema bado tunaiga. Kwa sababu *population* yetu ni 1.3 na ukigawa kwa *average* kila Wilaya katika Wilaya zetu 12 utapata watu laki moja na elfu tano. Bado *Centro Government* ina nguvu sana. Mimi nadhani Zanzibar ni sawa sawa na Mkoa mmoja wa Bara. Tukiangalia nchi yetu ya Bara bado nusu kwa nusu hawakufanikiwa itakavyo. Kenya tumeangalia wao hawakufanikiwa kabisa katika mpango huu.

Sasa niombe sana kama tutataka hasa aidha hapa inaelekea tumeiga au tumelazimishwa kufanya hichi kitu na wafadhili au kuna kitu chengine, lakini bado hatujawa hivyo. Hata hivyo kama tutarudi tena kwenye ugatuzi, niwaombe sana Wakuu wa Wilaya mfanye kazi kubwa sana ili kufikia hatua hii ambayo serikali imeitaka. Mimi sina hofu nayo lakini hofu niliyokuwa nayo bado Zanzibar tuna *population* ndogo, *Central Government* mnao uwezo mkubwa sana, tofauti na kuangalia Kilimanjaro ndio Mkoa lakini *Central Government* iko Dodoma kwa sasa, inaweza kuwa isi-*afford* lakini yule *regional* Kamishna ndio anayeweza kufanya kazi kule muda mwingi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu naona unataka kuniwashia taa yako. Mwisho niwapongeze sana wana Kamati ya Ushindi wa Yanga akiwemo Mwenyekiti, Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu), Mhe. Sada Mwenda, Mhe. Miraji na Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) pamoja na Mtendaji wetu Dau Hamad Maulid, amefanya kazi kubwa kuhakikisha timu ya Yanga inachukua ubingwa. Nakushukuru sana na niseme tu naunga mkono hoja hii kwa asilimia 98 asilimia 2 nataka nizichukuwe mwenyewe mpaka nipate jawabu lilokuwa sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) wa Jimbo la Mpendae kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Mtumwa Peya Yussuf, lakini kama nilivyosema mwanzo kuna waheshimiwa wameniomba dakika tano tano nitawapatia dakika tano kama muda utaruhusu. Mhe. Mtumwa Peya naomba uanze na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ajiandae.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia machache katika hotuba hii. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwa wazima wa afya na mimi kuweza kusimama hapa kutoa machache ambayo ninayo. Lakini pia nimshukuru sana Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na kuweza kuwasilisha hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi moja kwa moja nianze kwenye kikosi cha KMKM, Kikosi hichi nawapongeza sana kwa kazi zao nzuri wanazofanya. Humu wameainisha katika kazi zao wanazozifanya kwanza wanatoa huduma za afya kwa wapiganaji lakini pia kwa raia. Mimi nawapongeza sana kwenye hospitali yao pale Kibweni. Hospitali ile haiwasaidii wakaazi wa Kibweni tu mimi naweza kusema asilimia 98 ndani ya jimbo langu la Bumbwini tunatumia Hospitali ile ya Kibweni. Kwa hivyo kwanza niwapongeze sana kwa huduma zao nzuri ambazo wanazitoa pale. Pia kwa kuweza kuimarisha yale majengo kwa kutaka kutoa huduma za mama na mtoto.

Mhe. Mwenyekiti, panapo mazuri na mapungufu kiasi fulani pale yapo. Huduma nzuri zinazotolewa pale ukiangalia kuna mashine moja ya *X-ray* pale hapana. Wagonjwa wengi wanaokwenda pale na hata wagonjwa wa ajali tunawapeleka pale wanapatiwa huduma wakati wa kufanya X-*ray* inabidi tuwatoe pale tuwasafirishe kuwapeleka aidha Mnazimmoja au Al Rahma baadae urudi naye tena pale. Katika fungu lililooneshwa hapa sijakiona kipengele hichi kama itaingizwa X-ray katika hospitali ile. Namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja anambie kwamba je, hii huduma ya X-ray pale je, kwa wao hawana umuhimu nayo au ni lini wanaweza kuipata huduma hii ya x-ray kutuwekea katika kituo kile ili kuweza kufaidika askari lakini pia ina raia walio wengi wanaopata huduma katika kituo kile.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea hapo hapo kwenye Kikosi chetu cha KMKM, kipindi cha nyumba huko tulikuwa tunajua kwamba pale katika Chuo kile kuna mashine ambayo mashine ile ilikuwa ikisaidia sana wale askari wazamiaji hata raia wanaozamia watu wanapopata ajali ya kuzama. Wakati anapookolewa pale yule mzamaji anakuwa hali yake haipo vizuri sana. Kulikuwa na mashine hii

mzamiaji yule au raia yoyote anayeokotwa wakati wa kuzama anaingizwa kwenye mashine ile na akitoka hali yake inakuwa nzuri. Lakini kwa taarifa ya muda mrefu mashine hii pale KMKM haipo. Namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja anambie kwamba hii mashine kwa nini sasa hivi pale haipo na je, wanautaratibu gani wa kuweza kuitafutwa mashine ile na pia anambie gharama zake ni kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, nije hapo hapo KMKM ndani ya Jimbo langu la Bumbwini nina kitu cha KMKM, kipo Bumbwini Mnarani. Kituo kile kipo mbali sana na maeneo ya wananchi. Hapa hata usafiri wale hawana, wakipata tatizo inakuwa ni usumbufu mkubwa sana. Nimuombe sana Mhe. Waziri awafikirie wale watu kule, awawekee usafiri wa aina yoyote ili wakipata tatizo angalau waweze kujisaidia kufika sehemu ambayo inahusika.

Nikiendelea nakuja kwenye suala la hawa Zimamoto, hawa kuna hii sehemu inasema kwamba "kuboresha huduma za Zimamoto na Uokozi". Kweli Zimamoto na Uokozi wanafanya kazi nzuri sana, linapotokea tatizo haraka sana wameshafika. Lakini kuna jambo moja naomba kuliulizia. Kuna yale mavazi ambayo wanavaa Zima Moto wakati unapotokezea moto. Mavazi haya inavyosemekana ni machache sana kwenye sehemu hii ya hawa wafanyakazi wa Zima Moto.

Je, Mhe. Waziri naomba ukija uniambie haya mavazi ya Zima Moto lini yatapatikana ili watu wetu linapotokea tatizo waweze kuwa nayo ya kutosha kuweza kuokoa maisha yao lakini pia kuokoa maisha ya lile eneo pale linapotokea tatizo hili. Utakapokuja Mhe. Waziri naomba hili unipe maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye KVZ pamoja na Mafunzo, ndani ya Jimbo langu nina kambi mbili nyengine kambi ya KVZ lakini pia nina kambi ya Mafunzo. Kwanza ukiangalia kambi hizi zipo karibu sana na wananchi. Nimuombe sana Mhe. Waziri kambi hizi achukue juhudi za makusudi kabisa zizunguushiwe uzio ili waweze kujistiri wale askari wetu pale. Ukiangalia yale majengo ya KVZ wanayokaa askari hawa ukiangalia hayapo vizuri. Nimuombe sana Mhe. Waziri majengo yale yafushughulikiwe lakini na yale majengo ya kule Mafunzo pia nayo yashughulikiwe. Kwa sababu pale askari wanaishi na wake zao na familia zao na watoto wao wako pale, ukiangalia yale majengo kwa kweli hayakaliki. Nimuombe Mhe. Waziri achukuwe juhudi za makusudi kabisa majengo yale yashughulikiwe, yajengwe na yatiwe uzio ili wale askari na wao waishi katika hali ya usalama zaidi, ukizingatia hasa hali zetu za kisiasa tulizonazo katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nakuja katika suala la barabara za ndani. Kijiji cha Pangatupu, kijiji hichi sasa hivi kimepatwa na mtihani mkubwa sana. Ukiangalia huduma zao zote unapata Misufini, maeneo yao ya kupita ile barabara yao imeharibika vibaya sana. Mito yote imejaa maji, kutoka Pengatupu kuja Misufini hakupitiki na kule akina mama wanahitaji huduma za afya lakini kuna wanafunzi wanatoka Pengatupu wanakuja kusoma Misufini, ni muda mrefu sasa hivi tokea zimeanza mvua hizi wanafunzi hao wanashindwa kwenda kusoma kwa sababu njia haipitiki kumejaa maji.

Mhe. Waziri kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' niombe sana ile barabara iende katika ikatiwe vidaraja lakini pia itengenezwe ili kuwaondoshea usumbufu wananchi hawa wa eneo la Pangatupu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nakuja kwenye suala la CCTV. Mhe. Waziri suala hili ni muhimu lakini pia kuna mambo mengine muhimu zaidi. Ukiangalia kuna hili suala la DNA kila siku ushahidi unakosekana na masuala ya udhalilishaji yamekuwa mengi. Niombe sana hii CCTV ikatwe, fedha yake badala yake ipelekwe kwenye suala la DNA inunuliwe hii mashine ya DNA ili angalau huu ushahidi sasa upatikane na hawa wahalifu waweze kujulikana.

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru sana Mkuu wangu wa Wilaya ya Kaskazini 'B', Mkuu wangu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, kwa mashirikiano yao makubwa na pia baada ya kutokea maafa ndani ya Kijiji changu cha Pangatupu nimshukuru sana Mkuu wa Wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B', kuweza kuniunga mkono na kuwasaidia wananchi hawa wa Kijiji cha Pangatupu.

Mwisho kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia 99 asilimia moja nazuia mpaka nikipata majibu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mtuma Peya wa Jimbo la Bumbwini kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya Mhe. Jaku kuendelea hawa wachangiaji waliomba dakika tano wamo katika orodha majina yao yapo kwa hivyo nilitaka niwambie hilo. Sasa namwita Mhe. Jaku Hashim atafuatiwa na Mhe. Hidaya na Mhe. Mussa Ali Mussa ajitayarishe na mwisho kabisa kwa dakika hizo tano tano mlizoziomba atamalizia Mhe. Amina Iddi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa muda ulionipa lakini ulisikia dakika tano nimekwambia dakika 15, hii Wizara ni nzito ndio maana tukaomba kuichangia kwa siku mbili mpaka tatu. Lakini mimi

Mheshimiwa nitaheshimu muda wako kumi na tano ukigawa kwa mbili utapata saba na nusu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nikushukuru sana...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim naomba unisikilize kidogo, umeniomba dakika tano ..

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Muda wangu uulinde Mhe. Mwenyekiti ...

Mhe. Mwenyekiti: Nakufahamisha kwa sababu umeanza kuniomba nikuongeze dakika nyengine. Kama hivyo itakuwa haitoshi, haitowezekana Mheshimiwa nakuomba basi uje uchangie jioni niwape nafasi wale wengine. Kwa sababu umeomba dakika tano, kwa hivyo na mimi nakupa dakika tano.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, basi kwa ushauri wa *back bencher* na wataalamu wengu nilikuwa nao pembeni Mhe. Mwantatu na Mhe. Suleiman wamenishauri leo jioni mtu wa mwanzo kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti: Nakuomba uchangie kwa hizo dakika tano ulizoziomba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nitachangia jioni kwa hizo dakika 15.

Mhe. Mwenyekiti: Asante Mhe. Jaku Hashim.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Basi Mheshimiwa wananambia Waswahili wanasema kuna msema unapokuta maji yakoge mwanzo hujui kama mbele utayakuta.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na kumshukuru Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Muhammed Shein nirudie tena na tena kwa kuwafariji wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba. Kilichonivutia zaidi jana kwa Mhe. Ali Suleiman Shihata alipokuwa Pangawe na mbunge yule na aliposema maneno haya:

"Serikali ina jukumu la kuwasaidia wananchi hii ndiyo sera."

Kauli hiyo aliitowa, kwa hivyo Mawaziri na Manaibu Waziri mjue msimamo wa Rais wetu ulivyo alikuwa kijito Upele alisema maneno hayo.

Vile vile niendelee tena kumshukuru Mhe. Rais kwa uteuzi alioufanya kwa ndugu yangu Ahmada Yahya Shantimba kutoka Muyuni. Niwaombe wale *back bencher* wenye tabia ya kutaka kuitetea serikali, niwaambie kwamba mpangaji

ni Mungu. Kuna baadhi ya *back bencher* hujibu hoja za serikali kama wao ndio wasaidizi wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, msije mkashangaa Mhe. Yahya, keshokutwa akawa Naibu Waziri wa Mawaziri, haya mpangaji ni Mungu hakuna aliyetegemea kama Mhe. Yahaya atakuja hapa. Mhe. Yahya mimi nikutakie kila la kheri si muda mrefu pengine Mungu akijaalia utavuka mstari wa mbele kule. Kuna watu humu Wawakilishi baada ya kuungana na *back bencher* wanakuwa wanaisaidia serikali kujibu, ni jambo la kushangaza. Wasisubiri uwaziri au Unaibu Waziri Dkt. Shein anaona nani watendaji waendelee kustahamili tu Uwaziri na Unaibu Waziri mpangaji ni Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nichukue fursa hii kumpongeza Mkuu wa Wilaya ya Kusini kwa kazi aliyoifanya nitakuwa sijamfanyia haki. Mkuu wa Wilaya, hubaguwi mtu, huchaguwi mtu unapiga kazi tu na hivyo hata kwa Mungu fadhila zako utazikuta. Lakini hali kadhalika Mkuu wa Micheweni Abeid, kazi unayoifanya tumeiona kwa muda mfupi tu. Mimi nafikiri baada ya muda sijui kama hutochukuwa Mkuu wa Mkoa huko mbele Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe masikitiko yangu kwa Meya wa Mji wetu ni aibu tokea mwaka juzi, miaka mitano iliyopita nilipiga kelele kigari kile anachokipanda viksi hakielekei na hadhi yake. Mhe. Waziri mtendeeni haki, bajeti yake hii muidhinishieni pesa mtu anafuatana na Rais, Makamu wa Pili, ana kigari kile ni aibu. Mhe. Waziri nafikiri kasikia kilio chake hicho.

Mhe. Mwenyekiti, lakini, kadhia iliyowakuta vijana wetu hawa, leo kutiwa mimba imekuwa makosa? Alah! kitu cha ajabu. Mhe. Haji Omar Kheri, waziri dhamana naomba hawa vijana uwarejeshe, kilio cha wengi kina matatizo yake. Kama mwanamke kuchukuwa mimba makosa na akaondoshwa kazini ni kitu cha ajabu, hapa sina msalie Mtume. Nafikiri mada ushaijua nisipoteze muda kuna mambo mengi ya kuchangia lakini narudia tena vijana wametiwa mimba na waliondoshwa kazini warejeshwe. Hata akaja akisikia Rais wetu hili hatolikuwabali itakuwa aibu kwetu kwa Serikali hili ninavyo amini kwa Rais wetu alivyokuwa msikivu na utendaji wake na umakini wake. *(Makofi)*

Lakini nije kuhusu bomoabomoa Mhe. Mwenyekiti, ndugu yangu kaligusa hapo Mhe. Bhaa leo Serikali inakuwepo kuna Sheha, Naibu Sheha, Halmashauri sijui mtu anajenga mpaka nyumba anahamia unakwenda kumbomolea maisha haya maana yake mtu bora akose pahali pa kula atakaa chini ya muembe pakulala pahali muhimu, tuwe wa kweli tuna dhima kwa Mwenyezi Mungu pa kula unaweza kula chini ya muembe, lakini pa kulala

mtu keshajenga miaka yote Serikali ilikuwepo, Naibu Sheha, Sheha, Halmashauri mpaka nyumba anahamia ardhi hii haitoshi.

Mhe. Bhaa kazungumza hapa lakini la kushangaza na kutia huruma naishauri Serikali tena wazee mtakapo kutana huko kwa Bwana Mkubwa jana nilizungumza nilimshauri hapa Waziri wa Nchi (OR) Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) lakini nafikiri ushauri hakusikia alikuja kuzungumza kwa jazba na mliambiwa hapa na Mhe. Rais tulimwita Mhe. Waziri mkaelezwa na mtu aliyetoka na *credit* mimi sijisifu, Mawaziri, Manaibu Waziri mnapojibu hoja za Wawakilishi jibuni kwa ufasaha, akasema *Kullu Haki Wakullu Muruwa.* Jipeni haki japo kuwa chungu aliwambia maneno, lakini unauliza kitu kuisimamia Serikali katiba ya Zanzibar kifungu cha 84 Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongeza shughuli zake kutakuwa na vifungu vya katiba zitafanya kazi kwa mambo yafuatayo:

a) Kutunga sheria pale ambao utekelezaji wa jambo tunahitaji kuwepo kwa sheria hiyo.

b) Kujadili shughuli za kila wizara wakati wa kikao cha mwaka na Bajeti wa Baraza la Wawakilishi.

c) Kuuliza masuala mbali mbali Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi.

Hii ndio katiba ya Zanzibar ilivyokuwa tunakwenda kisheria humu ndani, lakini leo Waziri anakuja anashtuka anakurupuka imekuwa nongwa. Jana nilipokuwa nachangia mimi hapa niliuliza hapa elimu yangu mimi ndogo ndio nikawa sijapata Uwaziri wala Unaibu Waziri na nikataka ufafanuzi tu naona Mhe. Issa alikuja akajibu kwa jazba hapa na haya maneno kwenye kitabu chake katuandikia. Sasa mkiwa mnataka msihojiwe mawaziri mambo mengine mengine msiandike lakini matachokiandika itabidi tukiseme. *(Makofi)*

Msikiandike mkawa hamuandiki hatukihoji sisi lakini mnakiandika kitu kiko wazi sisi tufanye nini. Mheshimiwa kuhusu kadhia hii Mhe. Waziri hapa nataka kidogo nitulie unisikilize vizuri hata kuzungumza kwangu kwa aina yake Mhe. Waziri hebu nambie leo tumevunja Darajani, tumevunja Michezani, tumevunja eneo la Kariakoo miaka mingapi tumekaa Mhe. Waziri...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku malizia

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa niweka *stop watch* bado kama dakika 2:30

Lakini leo tunajenga karibu watu 3,000 pana ajira duka moja wanne au watano hebu nambie lengo liko wapi lengo leo tunaondosha skuli kwa kujenga *Mall*. *Mall* tayari pale Bwawani nafasi ishatolewa kwa muwekezaji, Mall ishawekwa pale Michenzani leo imekuwa skuli si bora kuliko kwenda kujenga *Moll*. Huku Serikali inasema tuondowe msongomano Darajani huku mnaongeza msongomano leo mji unakuwa, kuna Fumba huko mpya imejengwa tupeleke huko ndo maendeleo yenyewe. Paje kuna maeneo Jimboni kwangu yako wazi tupeleke. Leo tunajenga mjini tunajidanganya si kitu kizuri mie niombe ushauri Mheshimiwa kama utauchuku au hukuuchukua lakini hiyo ndio hali ilivyo.

Nije katika Manispaa ya Magharibi 'B' kuna jaa pale linawakera wafanyabiashara lishashindwa kusimamia pamoja na kazi kubwa Mkurugenzi Amour lile jaa kaliondesheni limejengwa kinyume na utaratibu linakera watu, leo Ofisi ya Dawa na Vipodozi iko pale pale ni aibu uchafu ulioko pale.

Mheshimiwa jengine nataka kwa maelezo haya magari yanayofungwa kule Mji Mkongwe nani dhamana ni Manispaa, Polisi Jamii kazungumza Mhe. Nadir hapa nitahitaji maelezo. Nani kapewa dhamana hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Jaku malizia

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa kwa kumalizia nije katika matatizo ya *fire* hawa watu wanafanya kazi kubwa lakini vitendea kazi hawana, redio hawana leo wamekwenda juzi Kitogani umeona yule mabanda ya wafanyakazi wanavyolala mule ndani, ni kitu cha kusikitisha.

Mheshimiwa kwa kumalizia Soko ya Darajani nafikiri Serikali sasa ishafika wakati walibinafsishe Serikali ishashindwa kusimamia, pamoja na mapato yote yanayokusanywa pale leo soko lishakuwa chafu muda wote ule.

Mhe. Mwenyekiti, nami nikushukuru lakini hili la Kisima Majongoo mwaka wa saba nalisimamia mtaro ule Kisima Majongoo, Kikwajuni ile ni aibu mwakani, mwakani mpaka tunakufa humu ndani lakini hampiti humu Waziri mkisha funga *tinted* zenu mawaziri hamuioni hali ya chini ikoje. Lakini hali ya Kisimamajongoo hairidhishi hata kidogo kwa usalama na raia wanapita na mali zao.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile kuna hii boti inayokuja keshokutwa ni kitu cha ajabu Mhe. Mwenyekiti. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku nmaomba ukae ahsante kwa mchango na imani Mhe. Waziri ameusikia sasa namuomba Mhe. Hidaya dakika tano na Mhe. Mussa Ali Mussa dakika tano na mwisho kabisa atamalizia Mhe. Amina.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kunipatia nafasi kuweza kuchangia machache kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, na miye kwa kuanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia na leo kukutana tena hapa kwenye hali ya uzima na afya ili kuweza kukamilisha majukumu yetu ambayo tunaendelea nayo na kuyafanya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kuanza moja kwa moja nianze kwenye suala la Serikali za Mitaa. Serikali za Mitaa zipo na zinafanya kazi na tuwashukuru sana Masheha wetu lakini pia Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa pia.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja akishirikiana pia na Mkuu wa Wilaya wa Kaskazini 'A' kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kuturekebishia Mkoa wetu pamoja na Wilaya yetu ile ili kuona tu mapato ya Serikali yanaingia lakini pia kuona wananchi wa Mkoa na Wilaya ile ya Kaskazini 'A' wanaishi kwa hali ya usalama na amani na kazi zinaendelea kama kawaida. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwanza nigusie hapa kwenye suala la Serikali za Mitaa Mhe. Mwenyekiti tunajua kama kwenye mitaa kuna Masheha na suala la Masheha linatokana na Halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti, Masheha wapo na kazi wanafanya lakini hapa ningemuomba sana Mhe. Waziri hawa Masheha wanapoteuliwa kweli maoni yanatoka kwa wananchi wenyewe ya kijiji ndio wanaopendekeza majina na ndio wanajua wao yupi anafaa. Lakini pia ningemuomba sana Mhe. Waziri angezingatia zaidi haya majina ambayo yanapendekezwa akayafanyia uchunguzi, kwa sababu kama mwana kijiji atapeleka jina lakini kuna mambo hawawezi kujua juu ya yule mtu anakwenda kufanya ile kazi. Kwa hiyo, tunaona kuna utofauti mkubwa baada ya hawa Masheha kupatiwa hii fursa ya Usheha kuifanya hii kazi yao kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri juu

ya swala hili na yeye angeingiza mkono wake akanza kulisimamia hili swala kwa ukamilifu ili tu hizi kazi za Shehia zikaweza kufanyika kwa urahisi na haya majukumu mengine hizi Wizara zingepunguka kwa kweli hali inakuwa ngumu kuanzia huko chini na ndio maana haya majanga mengine yanakuja mpaka huku juu.

Mhe. Mwenyekiti, pia niangalie kwenye swala la vikosi Mhe. Mwenyekiti miye nitazungumza kwa ufupi sana, swala la vikosi na Serikali hizi za vikosi hivi vya SMZ kuhusu suala la ajira kwa vijana ni suala ambalo linatupatisha tabu na linatutia kwenye majukumu mazito. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala la ajira vijana kwa kweli tunahangaika sana na tunapata changamoto kubwa kwa sababu vijana wimbi kubwa sana ambao wanachukuliwa wanawekwa kwenye makambi wanapewa mafunzo na wanapatiwa, yaani kama tuseme ahadi sijui au ndio nini mbali mbali wanazozipata kule wakiwa kule kwenye yale makambi kwa kuweza kujenga mioyo yao, lakini pia kuwekwa na tamaa ya kwamba tu ajira zitakapoanza mtachukuliwa na kupelekwa.

Lakini tuu pale ambapo ajira zile zinakuja inakuwa ni tofauti vijana wale huwa wanabaguliwa na kuwekwa kando na kutafutwa wale ambao pengine hata hawahusiki.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala kwa kweli linatuumiza vichwa na linatupa wakati mgumu sisi wengine ambao hata pengine hatusiki huku kwa kweli Mwenyekiti tungemuomba sana Mhe. Waziri aliangalie swala hili kwa macho manne maana si mawili, macho manne aliangalie ili tu suala hili liweze kupatiwa ufumbuzi juu ya vijana wetu hawa waojitolea kila siku ni hao hao na kila siku utakuta vijana hao wako nyuma kimaendeleo lakini wako nyuma kiajira pia. Lakini pia vijana hawa hawa palepale tayari wameshapatiwa zile ajira kuna changamoto kubwa ambazo wanakumbana nazo huko.

Mhe. Mwenyekiti, kubeba ni suala la kawaida kama ni mwanamke umeshakuwa mtu mzima Mwenyezi Mungu akishataka kukupa mimba huna vya kuikataa utaipata tu, sio kama vijana hawa tayari wameshapata ile ajira mtu kashafurura uso ashajua mimi hapa naweza nikashughulikia familia yangu na maisha yangu leo baada ya miaka miwili unamsimamisha eti sababu umempima mimba ana mimba. *(Makofi)*

Mimba ni ya miezi kidogo anaweza akajifungua akaendelea na kazi kwa hivyo kama waliwasimamisha kwa onyo basi nawaomba tu Wizara wawangalie

vijana hawa na waweze kuwarejesha kwenye kazi zao hizo kwasababu wao wafikiri tayari wameshampa mafunzo yule kijana muda wa miaka miwili si kidogo, jee wajiulize endapo watamuacha kijana yule kule mtaani atafanya nini wakati tayari yeye keshampa mafunzo ya kukamata bunduki na yakufanya mengine akija akaifanya huku mitaani atamlamu nani. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti namuomba sana Mhe. Waziri juu ya suala hili aliangalie kwa macho mengi na alifanyie kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia niende suala la gereza ambalo lipo kwenye kijiji cha Kinumoshi, Miwani.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri aliangalie kwa ukaribu zaidi lile gereza la wafungwa pale ambalo lipo miaka mingi tangu siye wengine hata mayai yetu hayajaundwa gereza lile linafanya kazi na lipo miaka mingi lakini kwa kweli linakabiliwa na changamoto nyingi sana ikiwemo barabara lakini ikiwemo hali ya miundombinu pia haifai, kwa kweli wanapata shida sana barabara haifai kila mtu anaiju barabara ya kutoka Mndo kuelekea Miwani kwamba barabara hii ni mbovu, kupindukia.

Lakini tukiangalia gereza lile liko katikati baina ya barabara hii na mabonde ya mipunga na mto unapita kukatisha miwani kwenda Kinumoshi kuelekea Bumbwisudi kwa kweli hali iliyopo pale si nzuri hairidhishi na hata tuseme wafanyakazi wa pale pamoja na wale wafungwa waliopo pale watake kuitumia njia ya kupitia Miwani kutokezea kuja juu huku pia nayo njia hiyo haipitiki, kwa kweli wako katikati ya mwitu tuseme kwa sababu njia si kupandishia Miwani wala si ya kupandishia Kizimbani ambayo wanaweza wakaitumia wakaweza kupata unafuu wa safari yao, kwa kweli wako katika hali ngumu lakini pia majengo yao hayaridhishi ni mabovu na yako katika mbaya zaidi. *(Makofi)*

Tukizingatia zaidi kipindi hiki cha mvua huwezi kusema hata upite kwa miguu pale ukamate angalau yake mapingili ya muhogo uweze kujiteleza ufike kule unakokwenda huwezi kwasababu hali ya njia ile si nzuri hata kidogo ni sawa sawa na matuta yalipingwa na mtu ambaye kwamba hajui kwa hiyo, yakawa yamewekwa kiaina yake tu peke yakekwa hiyo hawawezi kuitumia njia ile hata kidogo.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti ningemuomba sana Mhe. Waziri awaangalie sana kwa jicho la huruma na awafanyie miundo mbinu yoyote japo kuwa fusi pale linatosha kwanza kwa kipindi hiki ili mradi tu ile hali iliyopo pale iweze

kuwastiri wao lakini pia na wananchi wanaoishi katika maeneo ya Kinumoshi pamoja na Miwani.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia na miye nafasi hii ya dakika tano lakini nipongeze sana Waziri kwa hotuba yake hii na naiunga mkono asilimia mia moja. Ahsante Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hidaya Ali Makame Mwakilishi wa Vijana kutoka Kaskazini sasa naomba nimwite mchangiaji wa mwisho Mhe. Amina Iddi nafasi za wanawake.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana na mimi kunipatia nafasi

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa samahani sana nilimwita Mhe. Amina Iddi naona umesimama wewe lakini Kumbe umenikumbusha najua umenikumbusha kwa hivyo basi naomba nikwite Mhe. Mussa Ali Mussa wa jimbo la Ole naye nikupe dakika tano baadaye achangine Mhe. Amina. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti nakushukuru na miye kwa kunipa nafasi hii ili nichangie kidogo hizo dakika tano nataka nizitumie haraka haraka kwanza nataka niwapongeze Wazanzibari wote ambao wameshirikiana na wenzao wakiwasaidia kupambamba na maafa yaliotokea ya mvua kubwa.

Pili nataka niwape pole wale wenzetu wote wa Unguja na Pemba waliopatwa na maafa kutokana na mvua kubwa za masika lakini pia nataka nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba pamoja na Mkuu wa Wilaya kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kufanya kazi kubwa, ikiwemo hiyo Kamati ya Ulinzi na Usalama na mimi mwenyewe nikiwemo, kwa kufanya kazi kubwa sana kutokana na maafa yaliyotekezea kuharibika kwa nyumba pamoja na barabara zetu kule Pemba.

Sasa nataka niingie kwenye makusudio yangu makudusio yangu nataka kuzungumzia vikosi hivi vya SMZ, JKU, Mafunzo na KMKM, Zimamoto. Waheshimiwa wote waliosimama hapa nimewasikia wakiwasifu sana lakini baada ya kazi ni maandazi baada ya maandazi ni kazi. Kwa nini hatukuwapa zawadi basi tumewasifu wamefanya kazi kubwa hasa wakati ule wa uchaguzi. Sasa kwa nini hatukuwatunza hawa napendekeza mimi kwa Waziri atakapokuja awape mikopo wajenge majumba, awape mikopo ya usafiri, awape wapate vespa na mapikipiki ya kuendea kazini kwa sababu mtu anapofanya kazi anatakiwa apewe maandazi au awajengee awatafutie eneo awajengee awape

nyumba za mikopo nafuu hapo ndio tutakuwa tumewasifu, lakini kwa kuwasifu kwa mdomo tu haijawa sifa hiyo.

Jengine nataka niwambie baada ya hiyo sifa wale makamanda walioko kule wakiona askari amefikia miaka sita, saba wampe vyeo utamkuta askari yuko JKU ana miaka kumi na kuendelea hana hata ukoplo au ana kijikoplo si vizuri wewe ushakuwa kamanda una mawe tele mabega kwa nini huyu kijana wako wa chini humnyajui kwa hivyo namshauri waziri amwage vyeo kule kutokana na kazi waliofanya vijana wetu, uchaguzi wa marudio amwage vyeo kama si wao mimi nisingekuwepo hapa na mwengine yoyote vile.

Nakwenda kwenye uvunjaji wa majumba Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana mtu anapoanza kujenga anaanzia kwa Sheha, anakwenda Halmashauri, anakwenda mpaka anafika Idara ya Upimaji mote humo haiendi bure anakwenda na pesa *cash* anakuwa na risiti anakuwa na *document* zote anaruhusiwa kwenda kujenga. Anajenga nyumba anahamia, anakaa, anazaa watoto wanakwenda shule baadaye anakuja mtu nyuma anavunja nyumba ile tunakwenda wapi. Wakati alipokuwa akiomba mwananchi huyu wewe ulikuwa wapi kwa nini ulijiweka ofisini tu hukumfata ukenda kumuangalia anapojenga. *(Makofi)*

Sasa unakuja kumvunja nyumba wenzetu wanatuharibia siasa wanafanya makosa mpaka kwa Mwenyezi Mungu kumvunjia mtu nyumba yake ni kosa kubwa wewe yako ivunjwe utakubakuli. Nasema sheria ya kuvunja nyumba kuanzia sasa hivi itolewe na Mahkama tena Mahkama Kuu sio Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa hana haki ya kuvunja nyumba ya mtu. Mahakama ndio yenye mamlaka serikali ni Rais, Mahakama na hili Baraza la Wawakilishi au atuletee hapa tuje tupitishe kwamba kijiji fulani kikavunjwe. Lakini kutoka tu mtu akenda akasimama akavunja nyumba za watu hili jambo sio zuri na halikubali. Leo tunabeba lawama majimboni hakukaliki hatujui nini tujibu, watu wametuchagua kwa kutuamini leo asubuhi anakwenda kazini akirudi nyumba yake imevunjwa anaambiwa umejenga bondeni. Nilipojenga ulikuwa wapi, kwa nini ulinipa kibali cha kujenga? Waliovunjiwa wote walipwe nimekwenda kwa Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais nimetokwa na machozi mzee kama mimi kulia si uchimvi. Wamekuvuruga vuruga kule Mwera, na kule Mwera ndio ng'ome ya Chama cha Mapinduzi, wamefanya nini? Wapiga kura wetu wanawavunjia majumba waende wapi, wanatufanyia mambo gani. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mahakama ndio itoe amri ya kuvunja nyumba, tena Mahakama Kuu sio ya Wilaya wala Mahakama ya jimbo...

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mussa Ali Mussa…

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka uangalie umri.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umeomba dakika tano, kwa hiyo nakwambia ahsante kwa mchango wako.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Basi Mhe. Mwenyekiti, siwezi kushindana na mtoto wangu nimpendae. Naunga mkono hoja kwa asilimia 95 na asilimia 5 nazizuia mpaka atakapokuja nipa sababu waziri ya wananchi wa Mwera wale kupoteza majumba yao. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mussa Ali Mussa wa Jimbo la Ole naona Mhe. Waziri amekufahamu mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Amina Iddi Mabrouk naomba zile dakika tano mlizoziomba ziwe tano za kweli.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia kukutana hapa tukiwa wazima na afya njema, lakini pia nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuichangia bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuungana na wenzangu kwa kuwapa pole wale wote waliopata maafa mbali mbali katika kipindi hiki cha mvua. Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu awajaalie subra katika kipindi hiki kigumu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kwa dhati kabisa nichukue fursa hii adhimu kumpongeza kipenzi chetu Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upendo na imani aliyoionesha katika kipindi hiki kwa kuungana na wananchi bega kwa bega wale waliofikwa na maafa kwa kwenda kuwatembelea na kuwafariji, kwa kweli ameonesha imani kubwa sana. Namuomba Mhe. Rais wetu bado tunampenda na bado tunamuamini aendelee kuchapa kazi.

Mhe. Mewnyekiti, baada ya hayo basi pia niungane na wenzangu kwa kuwapongeza Wakuu wetu wa Mikoa yote na Wakuu wa Wilaya kwa jinsi wanavyofanya kazi za kuwaletea wananchi wetu maendeleo. Naamini kwamba wanafanya kazi katika kipindi kigumu, katika mazingira magumu lakini

wanajitahidi sana kuwafanyia haki wananchi wetu. Lakini zaidi nimpongeze Mkuu wetu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, kijana huyu kwa kweli anafanya kazi kubwa na nzito katika kuhakikisha kwamba Mkoa wetu wa Mjini Magharibi unakuwa katika hali ya salama na amani. Namuomba Mhe. Mkuu wa Mkoa na yeye aendelee kuchapa kazi na sisi tuko nyuma yako.

Mhe. Mwenyekiti, masheha ni kiungo kikubwa sana kati ya serikali yetu na wananchi kwa ujumla, hivi sasa ninavyozungumza hapa Mhe. Mwenyekiti Mkoa wetu huu wa Mjini Magharibi mpaka hivi sasa bado hawajateuliwa masheha wapya. Naamini kwamba sote tunatambua masheha katika Mkoa wetu huu wa Mjini Magharibi wako wengine wanaumwa na wako vitandani na inawapelekea kutofanya kazi zao ipasavyo. Pia inawapelekea kazi zile za usheha zifanywe na baadhi ya wake zao au pia na watoto wao.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna masheha wameshafariki kwa muda mrefu, vile vile kuna shehia mpya ambazo zinafika 60 zimeteuliwa. Kwa hivyo, sehemu zote hizi ninazozitaja kwa sasa hivi hazina masheha, Mhe. Waziri namuomba sana atakapokuja kutoa majumuisho atwambie basi na sisi Mkoa wetu huu wa Mjini Magharibi ni lini utateuliwa masheha wapya ili waweze kufanya kazi zinazostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije katika kitabu cha Mhe. Waziri ukurasa wa 28, kuhusu matukio ya udhalilishaji katika Mikoa yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la udhalilishaji wa watoto wetu na wanawake ni suala mtambuka na linatugusa sote humu ndani na walioko nje. Katika taarifa yake ndani ya kitabu chake amezungumzwa kwamba kuna kesi 633, kuna kesi ambazo ni 77 tu kwa sasa hivi ndio zimeshapatiwa ufumbuzi. Kama ni asilimia basi ni asilimia robo tu ndio zilizopatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hali hii inatusikitisha sana, hali hii inatuumiza sana hasa sisi kama tukiwa wazazi. Mhe. Mwenyekiti, mtoto wako anapotoka asubuhi akenda skuli au akenda madrasa kwa kweli mzazi unakosa raha mpaka mtoto yule umuone amerudi nyumbani. Mhe. Mwenyekiti, na serikali kwa ujumla hali hii tutaenda nayo mpaka lini ya kuwa na wasi wasi na watoto wetu na inaonekana hali inazidi kuwa tete katika Mikoa yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba basi Mhe. Waziri nitazungumza katika wizara ambazo husika kwa mfano Wizara ya Afya na Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto lakini kwa kuwa Mhe. Waziri na yeye amezungumza ndani ya kitabu chake hiki nimeona ni vyema na mimi nigusie

kama mwakilishi mwanamke. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho atwambie basi serikali na wizara yake kwa jumla imejipanga vipi kuhakikisha kwamba wanapunguza matukio haya katika Mikoa yao na Wilaya zao.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Amina Iddi.
Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, kidogo tu labda nigusie katika kikosi...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nilisema mwanzo dakika tano, dakika tano zimeisha na nimekuongezea na nimekuongezea kwa hiyo naomba…

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naheshimu muda wako naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Amina Iddi kwa mchango wako lakini kabla ya kuakhirisha kuna matangazo mawili niyaseme hapa.

Waheshimiwa Wajumbe wa CCM wanatakiwa waende ukumbi wa juu kuna kikao kutoka kwa Mnadhimu, lakini kuna taarifa ya msiba. Waheshimiwa Wajumbe, tunapewa taarifa kwamba Mhe. Nassor Salum Ali wa Jimbo la Kikwajuni amefiwa na mkwe wake, maziko yatakuwa kesho saa 4:00 asubuhi Kiembesamaki na kuzikwa Mwanakwerekwe.

Waheshimiwa Wajumbe, na mimi nawashukuru wote mliochangia na pia kwa utulivu wenu bado wachangiaji wapo lakini naomba wale ambao hawajachangia basi waandae kwa maandishi michango yao na kupeleka wizara husika. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana naakhirisha kikao hiki mpaka saa 11:00 jioni.

(Saa 6:44 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Sasa hivi nitampa nafasi Mhe. Tatu Mohamed Ussi. Mheshimiwa karibu.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuwa mtu wa mwanzo jioni hii ya leo. Kabla sijaanza mchango wangu nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kunipa pumzi nikasimama hapa jioni hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ katika bajeti ya mwaka 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa wakati alipokuwa akiisoma ambayo imeeleza kifungu baada ya kifungu, lakini pia nimpongeze Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora Idara Maalum kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake kwa ufasaha.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo mchango wangu utakwenda kwenye Idara Maalum za SMZ. Kwanza nipongeze Vikosi vyote vya Ulinzi vya Zanzibar kwa juhudi zao wanazofanya katika kutulinda wananchi. Lakini pili katika vikosi hivyo moja kwa moja nitakwenda kwenye Kikosi cha ulinzi cha Zimamoto.

Mhe. Naibu Spika, nikishukuru kikosi hiki kwa kazi zake inavyofanya, kinajitahidi katika kuokoa majanga yanayotokea kwa wananchi. Pia nataka nizungumzie kikosi kilioko katika Shehia yangu Mkoani pale bandarini kutokana na matatizo waliyonayo.

Mhe. Naibu Spika, kikosi hiki kinafanya kazi zake kwa ufasaha na kwa umakini sana, lakini tatizo la kikosi hiki ni makaazi. Kwa kweli pale walipo kikosi hiki hawana nyumba, wapo sehemu ambayo wametengewa kukaa, lakini kwa bahati mbaya sehemu ile wanayokaa kikosi hiki imefanywa ni kituo cha magari. Kwa hivyo wanapata usumbufu sana. Hivyo naiomba Wizara husika au Serikali iliangalie tatizo hili ili askari wetu hawa wapate nafasi ambayo wataweza kujengewa kituo kwa kukaa vizuri kwa kufanya kazi zao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nipongeze pia Kikosi cha KMKM pale Mkoani kwa jitihada zao wanazozifanya, kwa sababu sasa hivi wanaboresha nyumba yao. Kwa hivyo ni jambo la kufurahisha sana. Nawaomba waendelee na jitihada hizo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo kutoka kwenye vikosi moja kwa moja mchango wangu utaelekea kwenye programu za mikoa ukurasa wa D7 mpaka D11. Kwanza niwapongeze Wakuu wa Mikoa yote ya Zanzibar, Wakuu wa Wilaya wote kwa jinsi wanavyotekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Pia pongezi za pekee kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba

pamoja na Wakuu wake wa Wilaya wa Chake Chake na Mkoani kwa jitihada zao wanazofanya katika kuwatumikia wananchi wa Mkoa huu, nawapongeza sana.(*Makofi*).

Vile vile niwapongeze Makatibu wa Mabaraza ya Miji Chake Chake na Mkoani kwa sababu wao ndio wanaokusanya mapato ya serikalini. Nawapongeza kwa jitihada hizo waendelee nazo.

Mhe. Naibu Spika, katika kazi zilizofanywa katika Mkoa wa Kusini nimeziona ni kazi nyingi, pia kuna kazi iliyofanywa na Baraza la Mji Mkoani, nawashukuru sana kwa kazi hiyo. Lakini nije katika sehemu ya barabara. Mhe. Naibu Spika, kilio changu kiko katika barabara inayotoka Mbuguwani kuelekea Tironi hadi Kionwa. Mheshimiwa barabara hii imekuwa siku nyingi nikiizungumzia na niliuliza maswali nikaambiwa iko katika Ofisi hii ya Tawala za Mikoa. Sasa naona leo hapa ndio pahala pake.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, barabara hii naiombea kwa serikali iangaliwe kwa jicho la huruma kwa sababu barabara hii ina wananchi wengi wanaoishi katika kijiji cha Tironi na Kionwa yake. Barabara hii ina wakulima wa mazao ya muhogo na migomba walio wengi wanaotoka sehemu ya mjini kuelekea sehemu hiyo ya Tironi. Lakini vile vile barabara hii katika Kijiji cha Tironi kuna skuli ambapo wanafunzi wake wanatoka katika sehemu mbali mbali zikiwemo Mbuguwani, Manyaga pamoja na Tironi yenyewe, na barabara hii ni mbovu haipitiki hata kwa baiskeli haiwezi kwenda, acha siku hizi za mvua lakini hata hizo siku ambazo hakuna mvua haijanyesha. Kwa hivyo naiomba Serikali barabara hii iangaliwe kwa jicho la huruma sana kwani kuna akinamama wanaolima katika mabonde yale ya Tironi, lakini pia kuna watoto wetu ambao wanakwenda skuli lakini siku za mvua kutokana na barabara kuwa haipitiki watoto wetu wanashindwa kwenda skuli. Hivyo naiomba serikali kuiangalia barabara hii.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango huo niende ukurasa wa 28 kifungu cha 66 ambacho kinazungumzia jumla ya kesi za udhalilishaji. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli suala hili kila siku linatuumiza roho hasa sisi tukiwa wazazi. Nimeona hapa kuna jumla ya kesi 633 za udhalilishaji zilizoripotiwa. Kati ya kesi hizo ni 77 tu ambazo zimepata ufumbuzi. Sasa nilikuwa naiomba Serikali kwa sababu kesi zilizokuwa hazijapata ufumbuzi ni nyingi, naiomba Serikali kutumia vile vigezo ambavyo wametumia kwenye kesi hizi 77 ili na hizi nyengine zilizobaki zipatikane ufumbuzi kwa sababu kila tukikaa kesi za udhalilishaji zinazidi kuendelea.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo sina mengi nilikuwa na machache tu kwa leo, isipokuwa niwape pole wale wote waathirika waliopata maafa katika mvua hizi zinazoendelea kunyesha, kwani hadi leo kwetu Pemba bado mvua inaendelea. Kwa hivyo niwape pole na wale ndugu zetu wa Nyarugusu waliopata kimbunga juzi Mwenyezi Mungu awape moyo wa subra.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango huo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Kwanza nikushukuru Mhe. Tatu Mohamed Ussi kwa mchango wako mzuri, lakini Waheshimiwa Wajumbe nina wachangiaji wanafika kama 15. Kwa maana hiyo itabidi wengine wakubali kupeleka kwa maandishi ili tuweze kumaliza shughuli yetu hii leo.

Ningewaomba sana kwa sababu nadhani mengi sana yameshazungumzwa na kama tutakuwa tunazungumza naamini kwamba yatakuwa yanajirudia rudia. Kwa hivyo kwa wale ambao wanahisi wana yao ambayo wanataka kuzungumza, nitawaomba sana watumie dakika tano tano, nitawataja na watumie dakika tano tano nitawapa nafasi. Lakini nitamuomba Mwanasheria Mkuu atengue kifungu cha Kanuni ya Muda ili tuweze kuendelea kwa hizo dakika tano na baadae tuweze kuwapa Waheshimiwa Mawaziri na wao wachangie wana masuala ya kujibu, nitachagua mawaziri wenye masuala ya kujibu watajibu halafu baadae tutamkaribisha Mhe. Waziri kwa ajili ya kuja kufanya majumuisho.

Nafikiri nimeeleweka vizuri Waheshimiwa. Kwa hivyo naomba nimpishe Mhe. Mwanasheria Mkuu aweze kutengua kifungu cha Kanuni ya |Muda. Mwanasheria Mkuu karibu.

KUTENGUA KANUNI YA MUDA

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutengua kanuni ya mjadala ambayo ni kanuni ya 58(6).

Mhe. Naibu Spika, kanuni ya 58(6) inatoa fursa ya kuchangia na mjadala. Kwanza kwa vile ambao wanahitaji kuchangia wako wengi na muda wenyewe hautoshi, basi nitoe hoja ya kutenga kando kanuni hiyo na uruhusu zitumike dakika tano badala ya dakika 20 kwa kila mjumbe kwa mujibu wa kanuni hiyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwanasheria Mkuu ametoa hoja wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa tunaendelea naomba nitaje majina ya watu ambao...

UTARATIBU

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, nimesimama kwa kIfungu cha 63 kuomba utaratibu na muongozo wako, kwenye jadweli letu la ratiba inasema wizara hii inamalizika kesho na watu waliokuweko hao uliowataja wanakidhi haja ya kumaliza leo, kuendelea kuweza kutengua kanuni ni kufilisi wajumbe wako wa Baraza lako tukufu wasijadili kwa kina wizara hii ambayo ndio wizara mama na wizara refu. Naomba muongozo wako ili tuweze kuendelea.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa ni kweli kwamba tulikuwa hii wizara imalizike kesho, lakini kutokana na dharura mbali mbali na nyinyi mnazijua dharura zenyewe. Kwanza tuna shughuli peke yake ya Ramadhani karibu inakuja, lakini ratiba yenyewe iko *tight*. Kwa hiyo, tulikuwa tunaona afadhali tumalize leo ili kesho tuanze na ratiba nyengine. Naomba hili tukubaliane sisi ni watu wazima tunafahamu kwamba kunakuwa na dharura na tunafahamu mengi tumeshayazungumza hapa, tutoe nafasi hiyo. Mhe. Mohamed Said Dimwa naifahamu kanuni yako lakini na busara hapa itumike vile vile. Kwa hivyo, nimeomba na tayari nimeshawaomba wajumbe na wamekubali, sasa sioni sababu tena ya kurudi nyuma hapa. Tuendelee.

Waheshimiwa Wajumbe wachangiaji watakuwa ni Mhe. Suleiman Sarahan Said, mchangiaji wa mwanzo, wa pili atafuata Mhe. Abdalla Ali Kombo, wa tatu Mhe. Omar Seif Abeid, atafuata na Dkt. Makame Ali Ussi na mwisho kabisa atakuwa Mhe. Makame Said Juma. Nimesema Waheshimiwa Wajumbe dakika tano zinatosha kabisa, kwa hiyo naomba sana tufanye kwa dakika tano na tuangalie sana muda. Pongezi, hongera tuzipunguze Waheshimiwa tunaanza Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, nashukuru angalau kwa kunipatia hizo dakika tano. Mhe. Naibu Spika, mimi nichukue mambo yote kwa ujumla, kwanza nimuombe Mhe. Waziri na Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira wote kwa pamoja niwaombe twende Chake Chake kwenda kuiangalia kwa pamoja, mji ule ni mpya ambao unataka kujengwa kwa mafanikio na upendeze, na mji ule hauna maeneo au nasema maeneo ya wazi. Kwa hivyo, ningemuomba waziri katika kujumuisha majumuisho yote kwamba sina muda wa kuzungumza amuombe Waziri wa Ardhi twende pamoja katika kuujenga mji wetu wa Chake Chake ambao ni mji mkuu wa Pemba. Kwa hivyo, nachukua kwa jumla ili kupunguza baadhi ya maneno mengi ambayo Mhe. Naibu Spika, ameniwekea kufuli, kwamba muda wenyewe ni mchache. Kwa hivyo, atakapokuja waziri hapa naomba kwamba anikubalie tumuombe na Waziri wa Ardhi twende pamoja kwenda kutafakari Chake Chake.

Mhe. Naibu Spika, la pili ningemuomba waziri kwamba kwa kweli nishachoka, kwa kweli ile njia ya Msingini inaitwa njia ya Sele Manga, mtu anayeanguka na vespa anaitwa Sele Manga, mtu anayejifungua Sele Manga, Mheshimiwa akinitengezea njia ile wala hana tabu ya kuipa jina, jina imeshajipa Sele Manga. Kwa hivyo, ningemuomba tu kwa mwaka huu Mheshimiwa piga, chinja, uwa aniokoe Mheshimiwa wangu nimeshachoka kusema, nimeshachoka kuweka ahadi. Kwa hivyo, namuomba sana maana yake Mhe. Naibu Spika, pale ananiangalia vya kutosha lakini sijui hata nikamate lipi niache lipi, lakini hilo Mheshimiwa namuomba sana mara hii atakapokuja aniweke popote lakini njia ya Msingini aitengeneze, namuomba sana Mheshimiwa wangu.

Jengine kelele nyingi za Mkuu wa Wilaya wangu wa Chake Chake. Mhe. Waziri namuomba miaka zaidi ya 50 lilikuwepo jengo pale Chake Chake likitumika la Mkuu wa Wilaya, jengo lile lilitupwa na lilikuwa halina mtu yeyote anayelitaka. Jengo lile limetengenezwa kwa pesa za serikali na lilikuwa na ahadi ya Mkuu wa Wilaya kurejeshwa mule, lakini baada ya matengenezo jengo lile limepata mwenyewe. Mheshimiwa ningemuomba sana tukamrudisha Mkuu wa Wilaya mule ili kumpa hadhi yake na pia kwa ahadi zile tulizompa. Mara nyengine tutamtoa mtu atakuwa hakubali tena kutoka kwa sababu akitoka harudi, ningemuomba sana Mheshimiwa hilo likafanyika.

Mhe. Naibu Spika, jengine ningemuomba kwamba haya mengine ya masoko yetu ya Qatar ya Kuwait, Ras al-Khaimah yote tutayachanganya huko huko tutakapokwenda Chake Chake. Kwa hivyo, hilo Mheshimiwa nikwambie zaidi.

Mhe. Naibu Spika, zaidi ya hapo ni kwamba nilikuwa namuomba sana tufanye ushirikiano mkubwa sana na hii kamati ya maafa. Watu wengi waliokuwa

wamekaa majumbani mwa watu ambao wametupa moyo sana tuje tushirikiane kuyarudisha maeneo yao haraka iwezekanavyo, ili tuondokane na hili tatizo na mara nyengine likitokea itakuwa ni rahisi kutupokelea. Ningemuomba sana Mheshimiwa pamoja na kwamba sio kazi yake sana, lakini inamuhusu, maana yake Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ndio waliokuwa wasimamizi wakuu na walioweka ahadi nyingi. Kwa hivyo, ningemshauri sana Mheshimiwa tukaja tukayaondoa matatizo hayo.

Jengine niseme kwamba, pamoja na matatizo ambayo tunayo lakini suala la ugatuzi hili nataka niwaombe wawakilishi wenzangu. Wizara hii ni wizara kubwa sana, wizara nzito sana, mimi nachelea hizi pesa zilizotiwa tunapiga kelele kwamba ni nyingi nasema ni kidogo. Ugatuzi ambao Mheshimiwa nataka baadae atakapokuja hapa atwambie ugatuzi wake anaanza kuuchukua lini? Juni, Julai, lakini najua ugatuzi uliopo hapa sina muda wa kusoma kitabu lakini najua ni skuli za maandalizi na za msingi; mahospitali katika hospitali zile ambazo ziko ndogo ndogo za chini, kilimo, uvuvi na mambo mengi.

Kwa hivyo, ningeomba sana katika bajeti hii tukaangalia kutokana na ugatuzi, sisi tusitie mikwala la kuweka vizingiti tutizame zaidi maendeleo. Hebu tuangalie ugatuzi utatusaidia nini katika maendeleo haya. Tungefanya kama kuangalia au kujaribu kwa sababu kila nikiangalia hii bajeti, nikiangalia na makazi yenyewe ya ugatuzi, maana yake nina skuli yangu pale Chake Chake hali hazitizamiki. Lakini namsubiri agatuke na mimi nimkamate. Sasa ningeshauri sana tukampa nguvu tukaweza kuendelea ili na sisi tukaweza kupata nafasi.

Lakkini mimi nataka niseme Mhe. Naibu Spika, katika jumla ya sehemu nyingi siwezi kusoma muda huu lakini kuna sehemu nimeona umenunua magari na mambo gani, sijui na Pemba utaisidia nguvu kama *fire* au magari mengine, kwa sababu nimeona vyombo kama vya pikipiki haya labda utakapoona kuna nafasi uje utwambie tu kama Pemba angalau utawasaidia pikipiki ngapia na nimeona zitakuja.

Kwa hivyo ningesaidia kwamba kwa hali ambayo sasa hivi Mhe. Naibu Spika, Pemba tusikifanye kama kisiwa kidogo ambacho kilikuwa hakina maafa. Sasa maafa yameshajitokeza kuliko hata Unguja. Kwa hivyo ningekuomba kama vikosi vyako uviongeze nguvu ili viweze kusaidiana na mazingira ambayo yatajitokeza hapa baadae. Mhe. Naibu Spika, sitizami muda lakini ukibakisha dakika moja uniambie.

Lakini chengine nilikuwa nazngumzia Mheshimiwa suala la mazingira na usafi. Mhe. Naibu Spika, kabla ya Baraza la Mji halijakuwa Baraza la Mji lilikuwa likiitwa *'Topas*" ilikuwa kazi zake ni usafishaji na utengenezaji mzuri wa nyumba pamoja na usafi wa nyumba ya mtu. Leo tukikaribia masika hakuna anayetengeneza msingi, hakuna anayelima majani, hakuna anayefanya kila kitu, kazi yote inaachiwa seriakali. Lakini nyumbani kwake ukigusa mlango anakupiga panga mtu. Sasa ningeshauri kwamba dhamana ya nyumba yake mtu ahakikishe anaifanyia usafi wakati wa mazingira kama haya, uchafu utakuta nyumba nyengine nje karo zinafufurika lakini hajali kwa hilo kwa sababu anamkera mwenzake. Lakini ukimgongea mlango anakwambia mlango wangu unaogonga unakuhusu nini. Lakini mazingira ya nyumba kwa sasa hivi nyumba nyingi utazikuta zina mageti, lakini nje ya geti Mheshimiwa hakupitiki

Mhe. Naibu Spika: Umebakia dakika moja Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said : Hee! Haya Mheshimiwa ahsante nakushukuru pia hapo lakini.

Mhe. Naibu Spika, usafi ni kitu peke yake na mazingira na nataka nazingumze kwamba zamani ilikuwa haya mambo ya misingi kitu gani tukikaribia tu katika mvua za Machi kwenye Febuari usafi wa nyumba na mazingira yote yalikuwa yanasafishwa ili kwa kusubiri mvua. Sasa hatujali na hili.

Kwa hivyo Naibu Spika, ahsante sana kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi naunga mkono hoja asilimia mia moja.(*Makofi*).

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunigaia hizo dakika kidogo za kuweza kuchangia.

Lakini mimi moja kwa moja mchango wangu unakwenda kwenye *page* namba 11 mstari wa nne kutoka chini ambapo kunaonekana kwamba inasema, "Hadi kufikia Machi 2017 Idara Maalum kupitia Kitengo cha Ujenzi wa Barabara ilikuwa imetumia jumla ya shilingi milioni mia sita tisini na sita nukta nane kwa ajili ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 1.1 kiwango cha lami kati ya barabara za kilomita 3.1 zilizopangwa".

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi kuna jambo ambalo lilikuwa linanipa wasi wasi juu ya uhalisia wa hii pesa naona nyingi sina tatizo lakini kama ni hivyo, kwa nini Mheshimiwa mimi ningependa kujua barabara yangu ya Konde/Msuka, barabara ambayo ina shida, kuna kituo kikubwa cha KMKM ambacho ni askari wetu wanaotulinda. Kwa nini mpaka leo pamoja na ahadi ya

Rais ikawa haijatekelezwa na baada yake zikachukuliwa pesa shilingi milioni mia sita tisini na tisa karibu milioni mia saba. Je, pesa hizi zingepelekwa kwenye barabara nyengine serikali ingawa hizi ni pesa kwenye *feeder road*, lazini zote ni mali ya SMZ na walioko kule ni watu wetu.

Kwa hivyo mimi naomba sana kwa jambo hili la ujenzi wa barabara sisi tuangaliwe zaidi kulikoni kuweka kipande cha nusu kilomita cha barabara.,Kkule mimi nina barabara mbili ambazo ni muhimu. Hiyo barabara ya Konde/Msuka na barabara ya Konde/ Makangale ambapo barabara zile kuna wawekezaji asilimia nyingi ya mapato yanatokana na utalii yapo katika jimbo langu na barabara ile ni ukweli usiofichika kwamba haipitiki ina visima, ina na kila kitu barabara yenyewe. Kwa hivyo naomba sana Mheshimiwa serikali iangalie kwa jicho la huruma barabara hizi za Konde/Msuka na Konde/Makangale ili ziweze kujengwa angalau kwenye mwaka huu wa fedha pamoja na ahadi nyingi zilizokwisha kutolewa.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye ukurasa wa 12 Programu ya Usimamizi na Utumishi wa Idara Maalum. Mimi naendelea kuzungumzia suala la wale vijana ambao walipata uja uzito na wakawa wamesimamishwa kazi pamoja na kuwa walifuata sheria wakaenda katika Utumishi, Idara Maalum yao watatu wakarejeshwa na wengine wakazuiliwa. Lakini sasa wapo wale ambao wamerejeshwa na hawa mimi siwezi kutafuna maneno ni vijana wetu makada wetu, watoto wetu wa Chama cha Mapinduzi wanaokipenda Chama cha Mapinduzi.

Kwa hivyo naiomba mimi serikali ifanye bidii Mhe. Waziri mimi nataka nijue sababu gani hawa mpaka leo hawajarejeshwa kazini. Kwa hivyo naomba jambo hili la msingi ambalo wenzangu wameshalizungumza kwa wingi kwamba iko kila namna ya haja ya watoto hawa kuwarejesha kazini, kwa sababu tayari wameshatumikia kwa muda mrefu. Lakini pia nilitaka kujua hatma ya mishahara yao toka walipozuiliwa iko vipi au mishahara hiyo inakwenda wapi ya hawa vijana hawa. Naomba Mhe. Waziri nipate jibu hilo.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nimeona katika Jeshi la Kujenga Uchumi B2 *page* 14, nimeona pale wamesema Mheshimiwa kupitia Programu ya Mafunzo na Uzalendo na Uzalishaji za Amali, JKU imetoa mafunzo kwa vijana elfu mbili mia mbili na sita kuhusu uzalishaji wa kilimo na mifugo na mafunzo wa uzalendo na vijana mia moja na tisini mpaka wamemalizia mwisho vijana mia saba tisini na sita ambapo ukiwachukulia hawa hesabu yao ni karibia vijana elfu nne mia tatu hamsini na nne ni nguvu kazi kubwa ni vijana wengi ambao sisi alau kama tungewatumia vizuri na kutakuwa na mpango maalum wa

kuwatumia vizuri vijana hawa wakaweza kuchangia kwenye pato la taifa alau shilingi mia tatu kwa siku kwa mtu mmoja. Serikali kwa mwaka wa fedha kipindi kimoja wanao uwezo wa kuliingizia taifa shilingi milioni mia tatu na ishirini na sita na laki tano na hamisini. Kwa hiyo mimi napendelea kwamba vijana wote ambao wamepata mafunzo kupitia Idara hii ya JKU, vijana hawa wawezeshwe kwa kupewa nyenzo ili waweze kuchangia ukuaji wa uchimi wa nchi yetu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sijui kama dakika zangu zimekwisha lakini niende kwenye KMKM na boti za uokozi Kikosi cha uwokozi hicho. Mimi nina kilio kikubwa kwamba sasa umefika wakati wa kuwa na boti za uokozi, boti hasa za uokozi kwa ajili ya visiwa vyetu. Kama tunavyojua nchi hii ni nchi iliyokuwa imezungukwa na visiwa. Kwa hivyo usafiri wake ni wa baharini ukiachilia mbali kwamba mambo mengine, lakini kuwa na boti za kisasa kwa ajili ya uokozi ni jambo lililokuwa halihitaji mjadala.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo Waziri atakapokuja ...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika moja.

Mhe. Omar Seif Abeid: Nimemaliza Mheshimiwa.

Kwa hiyo Waziri atakapokuja nitamuomba aniambie nini mpango wake katika kuzitafuta hizi boti ambapo sisi tuna wataalamu wazuri huku KMKM wa mambo ya baharini kuweza kupatiwa boti hizi maalum zikatengwa kwa ajili ya uokozi pale inapotokea ajali ya dharura kati ya Unguja na Pemba, Bagayomo au Bara au na Tanga ambapo tumeshuhudia kila mwaka kipindi cha upepo wa Kusi watu wetu wanapata ajali.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho nilikuwa nachukua nafasi hii nakuomba dakika yako moja kwa ajili ya kuzungumzia maendeleo yaliyopatikana katika Mkoa wangu.

Mimi kwanza nachukua nafasi hii kuwapongeza Wakuu wa Mikoa wawili wa Kusini na Kaskazini. Mkuu wa Mkoa wa Kusini ni mwanamke pekee. Kwa hivyo UWAWAZA pamoja kuipigia kelele lakini pia mngepaswa kutuma pongezi maalum kwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini. Mkuu wa Mkoa wa Kusini ni mwanamke wa kupigiwa mfano, yalipotokea majanga mara hii kule Pemba ya ajali Mkuu wa Mkoa Mwanajuma alisimama mbele kama si juhudi zake lile jengo la *ZSFF* leo lingekuwa halipo. Hongera sana Mkuu wa Mkoa.(*Makofi*).

Sasa nachukua nafasi hii kuomba kwamba iko haja sasa ya serikali kuwaona kama Wakuu wa Mikoa wanafaa kuongezwa wanawake. Kwa hivyo Rais katika uteuzi wa mara nyengine pia mimi napendekeza achague wanawake kama alivyo Mhe. Mwanajuma, wapewe nafasi za juu.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja Mheshimiwa kwa asilimia mia moja.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante nakushukuru Mheshimiwa. Waheshimiwa minong'ono imezidi hatusikilizani hatuelewani humu ndani. Naomba sana mpunguze kuzungumza. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na baadae atakuja Mhe. Makame Said Juma una dakika tano tu jitahidi uzitumie vizuri.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa kunipa fursa hii na mimi niwe mmoja kati ya wachangiaji katika Wizara yetu hii muhimu sana ambayo kwa kweli tuna matumaini nayo makubwa sana kutuletea maendeleo.

Mhe, Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Mhe. Haji Omar Kheri kwa kusimamia utaratibu huu mpango huu wa ugatuzi tangu mapendekezo, utafiti, hadi kuandika andiko ambalo sasa hivi ndilo tunalolizungumzia hapa. Huko Mikoani sasa hivi kuna Maafisa Tawala yaani kuna Makatibu Tawala tayari wameshakuwepo na sasa hivi kuna utaratibu unapangwa wa mapendekezo ya kuanza sekretereati za Mikoa kuunda Mabaraza ya Wadi, Kamati za Mashaurinao za Shehia na muundo mpya wa mamlaka za serikali. Hizi zote zikikamilika zitasaidia sana kuleta maendeleo katika vijiji vyetu na majimbo yetu na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, ninachokiomba kwa haraka haraka ni kwamba kuna vikosi vyetu hivi vya SMZ. Vikosi hivi huwa vinaajiri kila baada ya muda pale inapohitajika. Sasa nashauri sana kuna vijana wetu ambao kwa kweli wametumikia sana muda mrefu, wengine wako makambini huko. Naomba sana vijana wale wachukuliwe ingawa najua wengine watakuwa wamepita umri lakini wahesabiwe wale kama ni askari kwa sababu wameshapata mafunzo ya uaskari waajiriwe hata kama watafanyakazi kwa muda wa miaka 5 tu wastaafu lakini wapewe tunza yao ya kuajiriwa.

Jengine ambalo ningependa kupendekeza ni suala la usajili wa vitambulisho. Kwanza naipongeza sana serikali kwa uamuzi wake wa busara kabisa wa kuziunganisha iliyokuwa Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho na Afisi ya

Usajili, Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka na kuwa afisi moja. Hii natoa pongezi sana kwa sababu mambo haya ya vitambulisho yakiwekwa pamoja ufanisi unakuwa mzuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, lakini ninachoshauri ni kwamba pametokea matatizo makubwa sana ya lawama kwamba wengine hawapati vitambulisho, wengine wananyimwa mambo mengi kama haya. Nashauri sana haya kwa kuunda Idara hii mambo haya yasitokee tena na naamini hayatatokea.

Jengine ambalo napenda nilishauri ni kwamba katika majimbo yetu naiomba sana Wizara hii iangalie majimbo kwa mujibu wa hali ilivyo. Kuna majimbo yana miteremko, kuna majimbo yako tambarare, kuna majimbo ya aina mbali mbali mengine yana miti na yale yaliyokuwa hayana miti. Sasa vipaumbele viwe kwa mujibu wa majimbo.

Mhe. Naibu Spika, Jimbo langu mfano la Mtopepo barabara zake zinaathirika sana wakati wa mvua ikinyesha mvua kidogo tu maji yanapita kwenye barabara kwa sababu hakuna miundo mbinu ya maji ya kupita, hizo njia tunazopita sisi zinazopita gari na maji yanapita humo humo. Kwa hivyo kunakuwa na mashimo makubwa sana. Kwa hivyo waziangalie sana barabara zile kwenye majimbo yale ambayo yana matatizo kama hayo ili tatizo hili la barabara lisiwepo kwa sababu barabara hizi wanatumia wenye ulemavu, wanatumia wagonjwa, wanatumia watu wa aina mbali mbali hata watoto kwenda skuli.

Nikitoa mfano tena kwenye jimbo langu hasa hata hizi daladala hakuna kwa sababu barabara hazipitiki. Sasa hii imekuwa ni shida sana wanafunzi wakitoka majumbani kwao kwenda skuli mbali pengine wanachukua muda mrefu na mara nyingi si ajabu wakachelewa au watoke usiku wawende kwenye shughuli. Kwa hivyo napenda sana Mhe. Haji Omar Kheri atumie umahiri wake na umakini wake aliouzoea ayaangalie sana majimbo haya kwa mujibu wa mahitaji yake yalivyo.

Mhe. Naibu Spika, Decentralization *by Devolution (D by D)*, huu ni ugatuzi wa madarakwa kwa kweli ambao umeanza nchi nyingi na ziko nchi zimefanikiwavizuri sana, lakini ziko nchi ambazo pia hazikufanikiwa. Mfano katoa mwenzangu hapa kwamba Kenya haikufanikiwa vizuri na Tanzania Bara pengine nao kuna matatizo. Sasa nashauri tuangalie sana kusimamia ugatuzi ili uende vizuri yasije kutokea matatizo yale, kwa sababu huu ugatuzi ni ghali sana, una gharama kubwa sana. Kule kunahitajiwa watu wenye utaalamu, kunahitajiwa yatakapoundwa haya Baraza hayo kuajiriwa watu vile vile waendeshe Mabaraza hayo. Sasa yote hayo yanahitaji fedha na mambo yote

haya ya huduma za afya, huduma za elimu itakapokamilika huu ugatuzi itabidi yawe chini ya Serikali za Mitaa. Kwa hivyo inatakiwa bidii kubwa sana iwepo ili mambo haya yaende kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie tu kwenye ulinzi hapa. Kwa kweli nimegusia vikosi lakini kwanza nivipongeze vikosi vyetu hivi sana vimejitahidi sana kulinda amani kwenye nchi yetu na kama si vikosi hivi nadhani kwa wale ambao walikuwa wanafanya fujo wangeweza kutesa wananchi sana. Lakini kwa umadhubuti wa vikosi hivi mambo ya ugaidi yote yaliweza kudhibitiwa.

Kwa hivyo nashauri vikosi hivi vipatiwe yale mahitaji ambayo vinahitaji ili viweze kuendesha kazi zao vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa maliza muda wako umekwisha.

Mhe. Dr. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo narudia tena kuipongeza wizara hii ya Serikali za Mitaa na Idara Maalum kwa ujasiri wao wa kuendesha shughuli hizi za ugatuzi ahsante sana.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa. Sasa namwita Mhe. Makame Said Juma.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Naibu, na mimi nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia japo kidogo.

Mchango wangu nakubali kama hautakuwa mkubwa kama ulivyo lakini nitaanzia suala la uokozi. Mhe. Naibu Spika, ingawa limezungumzwa sana suala hili lakini na mimi itabidi nilichangie kivyangu kama ninavyolifahamu, kwa sababu kila mtu ana ufahamu wake katika jambo fulani.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niwapongeze wanajeshi wetu wa KMKM kwa jitihada wanazozichukua mbali mbali kuokoa mazao yetu na kuokoa baadhi ya wananchi wetu ambao kuwa wamepata matatizo katika nchi yetu. Lakini pia na kuwadhibiti maadui ambao wanaisakama nchi yetu. Natumaini hili ni jamba la kuwapongeza.

Lakini Mhe. Naibu Spika, wanajeshi wetu hawa ipo haja kuwa na mabadiliko, kwa sababu kuna wenzangu walizungumzia sana katika masuala ya uokozi kwamba wapatiwe boti za kisasa. Mhe. Naibu Spika, Mwenyekiti, mazingira ya

bahari kila mmoja anayajua kwa namna ilivyo. Bahari ikichafuka sifikirii kama kuna boti ambayo itatoka juu kwenda baharini, kwa sababu na wala sifikirii kama vyombo vitafuatana kimoja kiko mbele na kimoja kiko nyuma au kimoja kiko mbele kinakuja kwa mwenzake na chengine kinakuja kwa mwenzake, halafu chengine kipate ajali kiweze kurudi nyuma kikamuokowe mwenzake, kama bahari inachafuka sio rahisi, kurudi nyuma hata kidogo kwa sababu mazingira ya bahari kama imechafuka chombo hakikubali kuzunguka, kikizunguka kinapata ajali. Kwa hivyo tunapata tatizo sana na wenzetu hawa wa KMKM wanashindwa kuokoa kwa sababu ya mazingira ya bahari yanayochafuka, sasa ipo haja.

Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu napendekeza iwepo haja kwa askari wetu hawa kupatiwa ndege aina ya *helicopter*, kwa sababu inaweza kufanyakazi kwa wakati mmoja mara mia moja na akafika maeneo ya mbali kuliko usafiri wa boti ambao hata kama itakuwa na kazi kiasi gani kutoka masafa mangapi, lakini haiwezi kwenda masafa hayo kama bahari imechafuka.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri afanye kila itakavyokuwa ili waokozi wetu hawa wapatiwe *helicopter* ambayo itakuwa na uhakika wa kuzunguka katika nchi yetu. Lakini isiwe kama hivi kupatiwa vyombo tu vya uokozi ambavyo vitakuwa kama ni boti, sifikirii kama vitafika kwenye ajali. Kwa sababu nakumbuka juzi tu karibu tuwapoteze watu 53 kwa kupata ajali baharini, ajali ile imetokea naamini wazi kwa mazungumzo waliyozungumza kulikuwa na vyombo karibu, lakini kwa sababu ya mazingira magumu ya baharini huwezi akarudi nyuma kamuokoa mwenzako, kwa sababu ukirudi nyuma tu basi na wewe tayari unazama. Lakini kama kutakuwa na usafiri wa ndege ambayo itaweza kuruka mara moja na sasa hivi wakati mawasiliano yako, basi natumaini ajali hizi za baharini zitapungua.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niende katika mazingira. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu safari hii ametupa mvua nzuri ambazo pamoja na changamoto zake na ajali mbali mbali, mazingira yetu yameharibika, miundombinu imeharibika. Lakini pamoja na hayo pia kuna mazao yetu yanaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, usafi wa mazingira ni kitu muhimu sana na umuhimu wake naamini wazi wakati huu wa mvua lazima yataharibika. Kwa sababu nakumbuka kuna matatizo ya maambukizo ya maradhi. Hivyo ipo haja wananchi wetu kujiweka tayari na upokezi wa maradhi haya kwa sababu lazima yatakuja. Lakini nakumbuka sana katika mazingira ya visiwa, kwa sababu nakumbuka mimi kwetu Kojani wakati kama huu maradhi ya mripuko yanakuwa mengi sana, na yanakuwa mengi kwa sababu muhimu. Kwa sababu

kikifika kipindi hiki cha mvua cha mchoo, wadudu ambao wanaosababisha mazingira machafu na kusambaza kwa haraka basi huwa wengi sana na wadudu hawa natumai sijui kama hawajafanyiwa utafiti huenda ikawa changamoto sana na maradhi haya kila leo yakaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, msimu huu tunaoelekea kwa mazingira ya kwetu kutakuwa na nzi wengi sana na nzi hawa wanasambaza maradhi kuliko kitu gani. Sasa hivi nakuambia kweli kwa mgeni kuingia nyumbani mwangu hawezi kula chakula, kwa sababu ya mzunguko wa nzi. Sasa ipo haja serikali kufanya utafiti wa kutosha na kuangamiza wadudu wale ili kuondoa matatizo, lakini kwa kusema tu tutafute madawa ya kuweka kinga za maradhi ya kipindupindu, sifikirii kama tutapiga hatua.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nije katika Wilaya Ndogo ya Kojani...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe muda wako bado dakika moja tu malizia.

Mhe. Makame Said Juma: Inshaallah Mhe. Naibu Spika, nakumbuka kwamba Wilaya Ndogo ya Kojani iko na imetengwa maalum. Lakini Mhe. Naibu Spika, Wilaya hii toka inalipoteuliwa mpaka leo ina wafanyakazi wanne, walikuwa wanne lakini mmoja kafa na wanne huyo aliyeongezeka ni mlinzi. Mhe. Naibu Spika, nimwambie Mhe. Waziri afanye fungu la huruma Wilaya hii nayo tunataka ikuwe. Nakumbuka au nina uhakika kwamba Wilaya yake Ndogo ya Tumbatu imekuwa kubwa lakini bado hii kila leo inaendelea kufa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi naiombea sana hii Wilaya Ndogo angalau nayo iangaliwe kwa jicho la huruma. Tunashukuru tumepata kijengo kidogo kwa kuanzia, lakini kufikia hapo tu tukaiondoa ikabakia na kufa.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi pia naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia juu ya na tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Sasa ni zamu ya Mhe. Rashid Ali Juma Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo baada ya hapo atafuata Mhe. Salama Aboud Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, baadae atafuata Mhe. Dkt. Khalid Salum Waziri wa Fedha na Mipango.

Waheshimiwa Mawaziri nimechagua wale ambao watakuwa na majibu ya kujibu katika hoja hii. Kama kuna Mhe. Waziri ambaye hana hoja ya kujibu

basi naomba aseme kwamba yeye hatojibu, kwa hivyo nimtowe kwenye *list* yangu. Mhe. Rashid karibu.

Mhe.Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa jitihada zake na nguvu zake zote anavyozielekeza katika kusimamia kuwatekelezea huduma wananchi anaowaongoza.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nina mchango mdogo sana katika kitabu hiki, kama ulivyoeleza kwamba tueleze yale mambo ambayo yametugusa katika wizara yetu. Lakini Mhe. Naibu Spika, kitabu hiki ukikitizama kuanzia ukurasa wa 50 mpaka ukurasa wa 55 unaeleza shughuli zile za Vikosi vyetu vya SMZ, vikosi maalum au idara maalum lakini pamoja na shughuli za mikoa ambayo ipo katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Katika shughuli zote zilizopangwa kwenye Idara hizi Mhe. Naibu Spika, utaona kuna shughuli kuu ya kuweza kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu, vile vile namna gani tunavyoona bajeti hii inaomba jinsi ya kuhifadhi raia wetu kuwa na utulivu kwa raia wetu, kupata salama kwa raia wetu na kuwalindia mali zao.

Lakini Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza haya, mimi nashukuru sana kwamba safari hii bajeti imekua na bado bajeti hii sio kwamba inaweza ikakidhi kufikia asilimia mia kwa mia, na mwakani naomba iendelee kukua zaidi ya hapa ilipokua. Na ninayasema haya kwa sababu katika kuyatekeleza haya Mhe. Naibu Spika, ndio tunakumbana na huduma zile ambazo zinasaidia wizara zetu kutekeleza majukumu yake. Wizara yangu ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo sehemu kubwa sana za kufanikisha kazi zake, zinategemea ufanikishaji wa kazi zilizopangwa ndani ya programu ya wizara hii ambayo tunaichangia bajeti yake.

Mhe. Naibu Spika, ni wazi kwamba pameelezwa masuala yanayohusiana na Mkoa huu wa Mjini/Magharibi. Sheria tumezitunga sisi hapa, sheria zinazohusu wizara yangu tumezitunga sisi lakini vifungu ambavyo vimo ndani ya sheria hii ndio vinavyowataka Wakuu wa Mikoa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria hizi zilivyo. Sheria inasimamiwa na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo lakini kuna vifungu vinavyoeleza namna gani Serikali za Mitaa zinatekeleza namna ya majukumu yale yalivyo.

Kwa mnasaba huo Mhe. Naibu Spika, nataka niwaambie wazi kwamba na mimi nawapongeza sana Wakuu wa Mikoa, hususan Mkuu wa Mkoa wa

Mjini/Magharibi. Nampongeza kwa jitihada zake anazozifanya na kwa kazi zake nyingi, kubwa na nzuri alizozifanya kwa kipindi kifupi tangu kuingia kwenye madaraka haya ya kushika nafasi hii ya Mkuu wa Mkoa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, huyu nataka niseme ni kiongozi mahiri kinyume na inavyoonekana, inaonekana labda kiongozi mahiri ni Waziri ambaye amesimamia hili, Waziri kwa sababu kalifanya hili. Lakini nataka kusema kwa kazi zilizofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi, kwa kupitia sheria hizi anazozisimamia na yeye bado amefanya kazi za umahiri, na namtaka sana Mhe. Dky. Ali Mohamed Shein aendelee kumpa msimamo na kumpa moyo wa kuendeleza kazi zake. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa majukumu ambayo yamo katika wizara yangu, hususan kwa masuala ya upigaji ngoma,miziki na masuala mengine. Mhe. Naibu Spika, tunakwenda kwa mujibu wa taratibu, sheria na kanuni za nchi. Kwa hivyo kiongozi anapotekeleza masharti yaliyokuwemo katika sheria zetu, basi huo ni wajibu wake. Endapo Ofisa aliyeruhusiwa kaweza kwenda kutekeleza majukumu yake basi amekwenda kutekeleza kwa mujibu wa sheria zile. Mimi naamini wazi kwamba miongoni mwa kazi zilizofanywa zimetekelezwa kwa mujibu wa miongozo tuliyotoa. Kwa wale wote waliopata matatizo, waliopata misukosuko inaweza ikatokezea.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka wakati tunatengeneza suala zuri hapa la watoto wetu namna gani washiriki katika sherehe za siku kuu za Iddi El Fitry na Iddi Al Hajji tuliwapangia muda. Miziki tumeondoa kabisa, madisko tumeondoa kabisa katika viwanja. Lakini vile vile tukakubaliana kwamba na shughuli tuzifunge saa 4:00, aliyetekeleza haya ilikuwa ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi ingawaje sheria iko katika wizara nyengine.

Kwa hivyo kutokana na hali hii Mhe. Naibu Spika, nasema wazi kwamba pamoja na sheria yetu kuelekeza kama ilivyoelekeza kama ilivyoelekeza, lakini utekelezaji tunapokiuka sheria ni lazima ufuatwe, utekelezaji ni lazima usimame katika mikondo ya sheria na sheria ziendelee kuchukuliwa pale zinapokiukwa.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru sana vijana kwa kuendelea kujiajiri wao wenyewe, lakini pia nawaomba sana kwamba waendelee kufuata sheria, taratibu na kanuni za nchi zetu.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuchangia hayo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri nakushukuru sana. Sasa hivi anayefuata ni Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba nichangie Wizara hii ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara ya Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, nianze tu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama ndani ya Baraza hili tukufu. Nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuendeleza serikali hii na kuendeleza maendeleo ndani ya nchi hii na kuhakikisha kwamba Wazanzibari wanaishi kwa amani na utulivu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na watendaji wote, Wakuu wa Mikoa, pamoja na wapiganaji wa Vikosi vya SMZ kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha kwamba serikali hii wananchi wake wanaishi wakiwa huru, lakini wanaishi wakiwa na utulivu, amani na bila ya bughudha yoyote.(*Makofi*).

Pia niendelee kuwashukuru na kuwapongeza kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuweza kuweka taa za barabarani. Taa hizi zimefika pahala ukiangalia eneo la Michenzani, Magomeni, Amani ukifika usiku mji wote unakuwa mweupe. Kwa hivyo kuweka taa zile kwa kweli wamefanyakazi nzuri, naomba niipongeze wizara kwa sababu sasa wananchi wetu wanatembea kifua mbele bila hofu wakati wote wa usiku bila ya tatizo lolote.

Mhe. Naibu Spika, vile vile limeweza kuongeza usalama kwa maana kwamba hata wale ambao wanafanya mambo mabaya nyakati za usiku basi wanashindwa kuyafanya kwa sababu wakifanya watafanya vichochoroni, lakini kwenye barabara sasa hivi yamepungua kwa asilimia kubwa, lakini hata ajali za barabarani zimepungua kwa asilimia kubwa kutokana na taa hizi ambazo ziko barabarani.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue fursa ya pekee pia kuwapongeza sana wapiganaji wa Kikosi cha KMKM, kwa kweli wanafanya kazi kubwa na niwapongeze sana kwa uamuzi wao wa kuijenga ile Hospitali pale Kibweni. Hospitali ile imekuwa ni tegemeo la wananchi Wazanzibari, watu wanatoka Magharibi na Mashariki, lakini wanahakikisha kwamba wanakwenda pale na wanapata huduma sahihi. Kwa kweli hasa sisi wanawake limekuwa ni tegemeo letu kubwa sana. Naomba niwapongeze kwa hili na niwaombe na vikosi

vyengine pia waendelee kupanga mikakati yao ya kuweza kuwasaidia na kutoa huduma kwa wananchi wa Zanzibar.(*Makofi*).

Vile vile Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru sana Wizara hii ya Nchi Ofis ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Vikosi vya SMZ, kwa maamuzi yao ya makusudi ya kufunga *CCTV Camera* katika maeneo yetu ya Mjini na baadhi ya sehemu za Magharibi. Kwa kweli uamuzi huu ulikuwa hauna mjadala ni uamuzi sahihi, kwa sababu teknolojia hii kwa hapa kwetu ni mpya lakini teknolojia hii ikizoeleka na ikitumika vizuri, basi wananchi wote wataweza kuishi kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa taratibu za nchi bila kikwazo chochote, na kuondoa yale mapungufu ambayo sasa hivi yanaweza kuonekana wazi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nitoe shukrani za pekee na pongezi za pekee kwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba. Kwa kweli ni mwanamke jasiri, anahitaji sifa na anafanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Naomba niliseme hili kwa sababu moja kubwa ifuatayo.

Mhe. Naibu Spika, wakati wa mwezi wa tatu ziara katika Mkoa wa Kusini Pemba, wakati tunaona umuhimu wa kupanga mji wa Chake Chake Pemba, basi Mkuu wa Mkoa huyu tulikwenda kwenye maeneo ambayo Waheshimiwa Wajumbe sasa hivi wanaweza kusema maeneo ya kupumzikia, lakini akafikiria maeneo ya kuegesha magari, pia maeneo ya soko kule Pemba wanaita Kuwait na Qatar. Lakini haya yote ni jitihada ambazo Mkuu wa Mkoa huyu kwa makusudi anazichukua kwa kushirikiana na taasisi karibu zote.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, wakati nilipokwenda pale nilikuta kaniwekea kikao kabisa cha watendaji wa kila sekta wanaohusika na hili, kuanzia wizara yangu lakini na Wizaran nyengine, kuhakikisha kwamba ufanisi unapatikana katika utekelezaji wa mpango wa mji ule. Kwa hivyo naomba niwatoe hofu sana Waheshimiwa Wawakilishi lakini naomba niwatoe hofu wananchi kwa ujumla wake kwamba mji wa Kusini Pemba ni mji ambao sasa hivi unapangwa na utaendelea kupangwa na yaliyopangwa yote yataendelea kutekelezwa kwa muda mfupi sana.(*Makofi*).

Lakini chengine ambacho naomba nikiseme Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wenzetu Vikosi vya SMZ wanafanya kazi kubwa, naomba niwapongeze, lakini Wakuu wa Mikoa wote wanafanya kazi kubwa kusimamia sheria na kusimamia taratibu. Kwa kweli tunafarijika sana hata sisi ambao tunashirikiana nao kwa karibu tunaona zile kazi wanazozifanya. Na mimi naomba tu nitoe wito kwa wananchi wa Zanzibar kupitia Baraza lako Tukufu kwamba tutoe mashirikiano

ya kutosha katika kuhakikisha kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanafanya kazi zao kwa ufanisi zaidi kwa mashirikiano yetu. Na kila taarifa ambayo tunaona sio sahihi katika maeneo yetu basi tuwaombe wananchi watoe taarifa ili wenzetu hao waweze kuifanyia kazi vizuri zaidi.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, naomba kabisa niliombe Baraza lako tukufu Wajumbe wenzangu wapenzi wa Baraza hili tukufu tuweze kuung mkono hoja hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na kuweza kuipitisha bajeti hii muhimu ili tuweze kufanya kazi zetu na tuwape nguvu ya kuweza kuyasimamia haya ambayo tumekusudia wayafanye.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante sana*.(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Sasa nimpishe ameniomba Mhe. Naibu Waziri wa Elimu anataka kidogo kuzungumza, baadae atafuata Mhe. Dkt. Khalid Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii kuchangia machache yaliyoulizwa juu ya suala la ugatuzi katika elimu. Nichukue fursa hii kufafanua kidogo na kuwakumbusha Wajumbe wenzangu kwamba suala hili la ugatuzi ni suala la kisheria na ni Baraza hili hili la Wawakilishi lililopitisha Sheria Na. 7 ya Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa 2014 na mamlaka za Mikoa pia ya 2014. Kwa hivyo ni suala la utekelezaji. Si suala la kuuliza uhalali wake uko vipi, tayari limeshapitishwa na Baraza la Wawakilishi, lililobakia ni utekelezaji. Hilo napenda kuwakumbusha kwa sababu baadhi ya Wajumbe waliona kama wanalitilia shaka labda halikufanyiwa kazi au hivi na hivi. Sasa tuko katika hatua ya utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, ningependa pia kuzungumzia suala la kwamba kulikuwa na wasi wasi huo ugatuzi wenyewe uko vipi. Lakini mimi nitazungumzia katika elimu, kwamba tunapozungumzia ugatuzi maana yake ni kwamba baadhi ya majukumu ya Wizara yanahamishiwa katika Serikali za Mitaa, sio yote ni baadhi. Sasa katika elimu katika hii hatua ya awali ni kwamba tutahamisha baadhi ya majukumu yafuatayo:

Kwanza, nauli na posho za walimu hizi zitashughulikiwa katika Halmashauri na Baraza la Mji. Pili, maposho kwa maafisa, bila ya shaka hawa ni maafisa wa elimu pia yatahamishiwa huko huko. Maposho kwa walimu wa vituo vya

maandalizi nayo pia yanahamishiwa katika sehemu zinazohusika. Jengine ni gharama za umeme, maji na matengenezo madogo madogo.

Aidha na la mwisho kabisa gharama za uhamasishaji na uandikishaji wanafunzi. Haya mambo yote yalikuwa yanafanywa na makao makuu ya Wizara, lakini sasa yanahamishiwa huko. Masuala mengine yaliyobakia yataendelea kusimamiwa na Serikali Kuu kwa maana ya Wizara. Maeneo hayo ni kama yafuatayo:

Mishahara bado wataendelea kulipwa na Wizara, udhibiti wa ubora wa elimu ambao tunaingiza masuala ya mitaala, mitihani na tathmini, haya yote yatasimamiwa na Makao Makuu kwa sasa.

Jambo jengine ambalo litasimamiwa na Wizara ni masuala ya sera, sheria na masuala mengine yenye mwelekeo wa kitaifa. Haya yatasimamiwa na Wizara. Aidha suala jengine labda pia lilikuwa linauliziwa uliziwa sana ni suala la ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa yaliyoanzishwa na wananchi ni mengi haya. Haya bado yatashughulikiwa na Wizara ya Elimu katika hatua hii, pamoja na madeni na malimbikizo ya walimu. Kwa hivyo wale waliodhani kwamba labda tunauhamisha mzigo wote tunaupeleka huko aah! kuna baadhi ya mambo ndio ambayo tunahamishia katika sehemu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na Mwakilishi mmoja aliuliza juu ya upungufu wa walimu hasa katika skuli ya Mwambe, akadhani kwamba labda Makao Makuu ya Wizara ikijiondoa, maana yake kwamba tatizo lile litakuwa kubwa zaidi, alikuwa na maana hiyo. Nataka nimtoe hofu kwamba suala la upungufu wa walimu tunalo na ni kubwa na Wizara inaendelea kulifanyia kazi. Hivi karibuni tu tunatarajia kuajiri walimu kama 51 kule Pemba na tumewagawa kwa mujibu wa mahitaji. Kwa hivyo Wilaya ya Mkoani tutawapatia walimu 15, Wilaya ya Micheweni 20 ukilinganisha Micheweni kuna uhitaji mkubwa zaidi hata kuliko Mkoani. Sasa hawa wa Mkoani 15 hawa watagawiwa kwa mujibu wa mahitaji vile vile ikiwemo Skuli ya Mwambe na Chambani ambazo zina uhitaji zaidi. Kwa hivyo, namtoa hofu kwamba tutawagawa walimu hao katika kipindi kifupi kinachokuja.

Lakini kulikuwa na shaka kama huku katika Serikali za Mitaa, Halmashauri za Baraza, Serikali za Mikoa na Wilaya zina uwezo kiasi gani. Nataka nihakikishe kwamba Serikali za Mikoa na Mitaa wana uzoefu mkubwa kabisa katika kusimamia masuala ya elimu. Hivi sasa tunafanya kazi nao kwa karibu na wakati mwengine wanatangulia wao zaidi hata kuliko sisi Makao Makuu Wizara, wanafanya kazi za kuimarisha ubora wa elimu katika maeneo yao,

wanafanya kazi ya kudhibiti utoro katika maeneo yao. Katika nukta hii nitoe pongezi maalum kwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kufanya kazi hii. Lakini pia wana uzoefu katika kuchangisha na ujenzi wa miundombinu ya skuli, napo hapa nataka nitoe pongezi maalum kwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini na Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake na Mkoani katika suala hili.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nataka nithibitishe haya niliyoyasema kwamba tulielekezwa kuikamilisha Skuli ya Ngomeni, sisi Wizara ya Elimu na Serikali ya Wilaya na Mkoa kwa kushirikiana pamoja tulifanya kazi hiyo kwa muda mfupi kabisa. Kwa hivyo, Wakuu hawa wana uzoefu wa kutosha na kwa sababu suala hili wamekuwa na mazoea ya kulifanya miaka na miaka, kilichotendeka sasa tunasema ni *just formalization* tu lakini uwezo huo wanao na tusiwe na mashaka watafanya kazi kwa uwezo mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumaliza hayo nieleze kwamba tunapotathmini utendaji wa taasisi….

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia ukija kutumia muda mwingi unamkosesha Mheshimiwa kuja kumalizia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Namaliza dakika moja tunapolinganisha taasisi basi lazima tuangalie mambo mawili muhimu. Kwanza tunaangalia ile raslimali tuliyowapa, pesa tulizowapa. Je, zinakidhi kufanya hilo ambalo sisi tunatarajia. Kwa hivyo haya ni muhimu sana, tusitathmini nje ya maeneo ambayo ndio yaliyohusika na kazi zenu.

Jengine la mwisho kabisa napongeza sana Vikosi vyetu vya ulinzi kwa uweledi wanaoonesha katika kufanya kazi zao, zile kazi za ziada wanazofanya labda za ujenzi tusizitathmini sana kwa sababu zile ni kazi za ziada, kazi zao za msingi ni ulinzi.

Naomba nimalizie maelezo yangu kwa kuunga mkono hotuba hii mia moja kwa moja *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Sasa tumpishe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, ajitayarishe Naibu Waziri wa Wizara husika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia Hotuba ya Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Naomba nitoe mchango wangu lakini pia kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo ambayo yameguswa na nahisi naweza kusaidia ufafanuzi katika maeneo hayo.

Lakini kabla ya hapo nitoe pongezi nyingi sana kwa Rais wetu Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. Nimpongeze kwanza kwa kutekeleza ahadi yake ya kuwaongezea mishahara ya kima chini kwa wafanyakazi wa kawaida kutoka shilingi laki 150 hadi 300,000, lakini vile vile askari wetu wa vikosi, askari wa Idara Maalum kutoka Shilingi laki mbili na laki tatu hadi laki nne na elfu sita.(*Makofi*).

Mhe. Rais amefanya hivyo kwa kutambua kazi nzuri inayofanywa na Idara zetu Maalum, jukumu lao la kutunza amani na utulivu katika nchi yetu.

Nichukue nafasi hii pia kumpongeza ndugu yangu Ahmada Yahya Abdulwakil ambaye Mhe. Rais amemuamini na amemteua kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, tunamkaribisha sana karibu*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Wahehimiwa Wakuu wa Mikoa yote, Wakuu wa Wilaya wote, Wakuu wa Vikosi na watendaji wote na wafanyakazi wa Afisi hii kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kutekeleza majukumu yao, lakini nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwasilisha kitabu chake na hotuba yake vizuri sana asubu ya jana, hotuba ambayo imejaa sana maelezo ya hekma. Lakini vile vile imesheheni utekelezaji wa majukumu ya Wizara yaliyowekwa katika mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, katika kutoa ufafanuzi nizungumzie suala la *CCTV* kwa kifupi kabisa. Waheshimiwa Wajumbe wengi wamelizungumza suala hili na wengine wamelizungumza kwa hisia tofauti. Lakini niseme tu kwamba mradi wa *CCTV* una sehemu kubwa sana ambayo sio kamera ambazo tunazozielewa. Kamera ni sehemu ndogo sana ya mradi huu na matumizi ya fedha yaliyotengwa basi matumizi yale ni asilimia 0.03ya bajeti ile. Kwa hivyo ni mradi ambao ni mkubwa na una masuala mengi sana. Mradi huu tulianza kuutekeleza tokea mwaka 20015/2016, tukaweka bajeti katika mwaka 2015/2016 ikatekelezwa. Kwa maana hiyo tuliamini Waheshimiwa Wajumbe wote wanauelewa wa mradi huo.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia tumeendelea kuutekeleza katika mwaka 2016/2017 na sasa tutautekeleza katika mwaka 2017/2018. Ni mradi wa miaka mitano, kwa hivyo tutaendelea nao hadi mwaka wa fedha 2019/2020. Hivyo

ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe wasiwe na wasi wasi na mradi huu ni mradi ambao umewekwa kwa maslahi ya taifa letu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo lakini niseme na jengine kidogo, wengine walichanganya na masuala ya *DNA* kwamba lazima zipatikane mashine za kupunguzia *DNA.* Niseme tu bajeti ya vifaa vyote vya Wizara ya Afya bajeti yake ipo, wala haihusiani na bajeti hii. Tumeweka bajeti ya kutosha kwa ajili ya vifaa. Sasa ni jukumu la Wizara yenyewe kuamua katika vifaa vile, ni vifaa gani watavipa umuhimu lakini bajeti yao ipo ikiwemo hiyo ya *DNA.* Sasa hili la *DNA* na *CCTV* tusiliunganishe.(*Makofi*).

Lakini la pili nizungumzie kuhusiana na suala la majengo ya Idara zetu, wengi walisema kwamba majengo yamechakaa na ni kweli Serikali inalijua hilo. Serikali iliunda kamati na tayari zimeshafanya kazi ya kufuatilia na kufanya tathmini ya kazi inayohitajika. Ndani ya miaka mitatu hii Serikali imepanga kuhakikisha kwamba majengo yote yanatengenezwa ya Idara zote za SMZ. Kwa mwaka huu wa fedha ujao 2017/2018 tumepanga kwanza kuanza na Vikosi vya KMKM na Mafunzo, na maeneo sita, maeneo matatu kila Kikosi yatafanyiwa kazi ndani ya mwaka wa fedha 2017/2018. Na fedha zilizotengwa ni wastani wa bilioni 1.62 kwa ajili ya kazi hizo na mwaka wa fedha ujao tutapanga vile vile kuendelea na kazi hiyo ya matengenezo ya majengo ya Idara zetu mbali mbali Vikosi vyetu vyote. Kama nilivyosema ndani ya miaka mitatu hii tunataka kukamilisha kazi hii.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini suala la sare na suala la vyarahani pamoja na kile Kiwanda cha Viatu, nalo Serikali tayari imeshalifanyia kazi. Watu wa Wizara ya Fedha, watu wa Ofisi hii ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na idara maalum za SMZ wameshakwenda India, wameshaona kitu gani wanakihtaji. Sasa hivi kinachofanyika ni kukamilisha *process* ya tenda ya ununuzi wa vifaa hivi. Na hapa tumetenga kiasi ya bilioni 1.3 kwa ajili ya sare za Serikali, vifaa pamoja na vyarahani kwa ajili ya Kiwanda cha Valantia, lakini vile vile kiwanda chao cha kutengenezea viatu vya maaskari. Fedha hizo zimetengwa ndani ya bajeti ambayo tunaendelea nayo hivi sasa ya 2016/2017. Kilichobaki ni kufungua *LC*. Kwa hivyo hayo yapo na Serikali inayajua na tayari imeshayafanyia kazi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kuna suala liliulizwa la Mhe. Mwantatu la kwamba bajeti ya Zimamoto fungu lao hasa lile la *OC* alisema ni dogo. Mwaka jana au mwaka huu tunaomalizia nao 2016/2017 tulitenge shilingi milioni 480, lakini kwa mwaka huu unaokuja wa fedha 2017/2018 zimetengwa Shilingi milioni 850 kwanye *OC* peke yake, ni ongezeko la mara mbili asilimia mia moja na hii

imetokea kwa Kikosi cha Zimamoto kwa kuelewa umuhimu wao na hali yetu ya kifedha. Lakini pamoja na uchache wa fedha tulizonazo tumesema kwa umuhimu wa Kikosi hichi na kazi zake na kuzithamini kazi zake basi wameongezewa kwa asilimia mia moja.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lilitolewa pendekezo la kuweka tozo katika mauzo ya mafuta kwa ajili ya kuongeza fedha zilizotengwa kwa ajili ya matenenezo ya barabara zetu za ndani. Hapa niseme hili wazo sio baya, ni wazo zuri, tunaelewa kabisa umuhimu wa barabara zetu za ndani. Lakini niseme tu suala la kuongeza tozo tokea mwaka jana mwaka wa fedha tunaoendelea nao 2016/2017, Serikali iliamua kutoongeza kodi yoyote na msimamo huu bado unaendelea katika bajeti ijayo ya 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni makubwa ya kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira mazuri ya uwekezaji, lakini mazingira mazuri ya biashara lakini pia kutowabebesha wananchi wetu mzigo kutokana na kuongeza kodi. Kinachofanyika sasa hivi ni kuhakikisha kwamba kodi zilizopo zinakusanywa kwa ukamilifu wake. Huo ndio msimamo wa serikali lakini niseme kwamba hili ni wazo zuri, tunaweza tukalifikiria katika mwaka ujao wa fedha. Ni vyema tukalifikiria katika mwaka huo kwa sababu hivi sasa wadau wote tulikwishawashirikisha, wameshatoa maoni yao, wale walipakodi wenyewe wanajua kupitia wawakilishi wao kwamba mwaka huu wa fedha pia unaokuja hatutoongeza kodi. Kwa hivyo si busara kuongeza kodi katika kipindi hichi lakini ni wazo ambalo tunalichukua kwa mwaka wa fedha ujao wa 2018/19.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna suala jengine la mtaro kwa Binti Hamran. Mradi wa huduma za jamii mijini unaendelea na kazi za kuchimba mitaro katika maeneo mbali mbali. Niseme tu mradi huu tokea ulipoanza umeweka maeneo sita ambayo yanajengewa mitaro kwa nia ya kuondosha maji ya mvua na kuondoa usumbufu, lakini vile vile kupunguza mafuriko katika maeneo yetu ya mjini ambayo yalikuwa kwa muda mrefu sana yanahatarisha afya za wananchi wetu. Mifumo hiyo ipo katika eneo la Kijangwani, Kibandamaiti ni mfumo mmoja, msingi wake utajengwa katika awamu hii ya pili ya mradi wa *ZUSP*.

Lakini kuna mfumo wa Mtopepo na Karakana ambao huu umekamilika na sasa hivi kwa kiasi kikubwa sana matatizo yameondoka, kazi zilizobaki ni ndogo ndogo. Kuna mfumo mwengine Mnazi Mmoja nashukuru sana umefanikiwa vizuri, maji sasa hivi katika kiwanja chetu cha Mnazi Mmoja hayakai, kazi zilizobaki ni ndogo ndogo sana. Kuna mfumo mwengine wa Darajabovu,

Kwamtipura, Shaurimoyo, Chumbuni na Mwembemakumbi utaendelezwa katika awamu hii ya mradi wa *ZUSP* na kazi inayoendelea sasa hivi ni kulipa fidia za wananchi ambao kwa namna moja au nyengine wataathirika katika mradi huu. Kuna eneo jengine Magogoni kupitia Nyerere, Bwawa la Sebleni Mikunguni, Saateni nalo hili litajengwa katika awamu hii ya pili ya mradi wa *ZUSP*.

Mhe. Naibu Spika, eneo alilolizungumza Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) tunaita mfumo E, kwa maana *system*, hii ipo kwenye maeneo ya Magomeni, inaanzia kwa Mtumwajeni, Mpendae, Kwa Binti Hamrani, barabara ya Jang'ombe, Meya, Jang'ombe Urusi, Migombani na Kilimani. Eneo hili tayari kwa kiasi kikubwa limeshajengwa mitaro yake, kilichotakia ni kuunganisha Jang'ombe, Mpendae na Kilimani. Sasa watu wataona kwa mara hii pia maji hayakuweza kwenda vizuri kwa sababu bado kazi haijakamilika. Kinachofanyika sasa hivi ni kulipa fidia. Tunahakikisha kwamba fidia hiyo italipwa ndani ya miezi miwili kati ya Juni/Julai, lakini mradi mzima nao tunautarajia utakamilika ndani ya kipindi cha miezi sita.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Dimwa asiwe na wasi wasi umo ndani ya mpango na utatekelezwa kama ilivyopangwa na utakamilika ndani ya kipindi cha kifupi, kilichobaki ni kuunganisha ili maji yaweze ku-*flow* vizuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo na mimi naomba sasa nitamke rasmi kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Sasa tutampitisha Mhe. Naibu Waziri na yeye ajibu baadhi ya hoja. Katibu Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisiri ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za (SMZ): Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa fursa na mimi nikaweza kutoa angalau mchango wangu katika hotuba hii ambayo inahusu Wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika michangio yangu nitaenda kwa kutoa baadhi ya ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kutoa pongezi zao mbali mbali ambazo

zilitugusa sote watendaji pamoja na wasimamizi na zaidi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pongezi hizo tumezipokea kwa mikono miwili na ni imani yangu kwamba inaonyesha dhahiri jinsi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaona jinsi tunavyochapa kazi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nianze kwa kuanza na suala hili ambao Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerey) kuhusiana na masuala mazima ya uzururaji wa mifugo katika mji wa Chake Chake. Naomba niseme kwamba wakati agizo la kudhibiti wanyama wanaozurura katika Mkoa wa Mjini/Magharib, agizo lile ni kwamba lililenga katika maeneo yote ya miji yetu ya Unguja na Pemba. Kwa mantiki hiyo ni kwamba hata maeneo ya Mji wa Chake Chake nako mifugo hairuhusiwi kuingia katika mji ule wa Chake Chake.

Mhe. Naibu Spika, natumia fursa hii kumwambia Mhe. Mwakilishi kwamba tumeshatoa maagizo kadhaa katika kuona kwamba utekelezaji wa jambo hilo unafanyika katika maeneo ya miji Unguja na Pemba. Hivyo basi ni imani yangu kwamba agizo hilo linafanyiwa kazi na kama kuna baadhi ya wengine hawajatekeleza majukumu hayo au maagizo hayo ni kwamba kidogo wanakwenda kinyume na utaratibu na hatua zitachukuliwa kwa mujibu vile ambavyo tokeo au agizo limepuuzwa.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine naomba nitoe ufafanuzi katika Waheshimiwa Wajumbe ambao walizungumzia suala la ubomowaji ambao umefanyika katika maeneo ya Sharikia kule Kianga, maeneo ya Darajani na Michenzani. Naomba tu Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba hatua hizi ambazo zinafanyika huo ni utekelezaji wa kisheria. Naomba nichukue fursa hii kwamba nampongeza sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharib kwa kutii maagizo ambayo ni matakwa ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu inavyostahiki.

Suala la ubomoaji kuonekana kwamba limecheleweshwa kufanywa maamuzi na kusubiriwa wananchi mpaka pale wameshaendelea kujengwa ndio hatua zichukuliwe. Niseme kwamba jambo hilo halikuwa sahihi. Kwa sababu hatua mbali mbali na jambo hili halikuwa la siku moja na utaratibu ni uzoefu kwamba katika nchi yetu wananchi tumekuwa hatuna utamaduni ule wa kufuata sheria bila ya kushurutishwa. Hivyo suala hili halikuwa la siku moja, maangalizo mbali mbali yalitolewa, kuanzia mwaka 2015 kabla watu hawajajenga na suala hilo lilikuwa linaendelea na hatimaye ilipofika kipindi hichi cha mwaka 2017 Mhe. Mkuu wa Mkoa na watendaji sasa hatua nyengine zikachukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, hivyo basi naomba niwambie Waheshimiwa Wajumbe kwamba hatua hizo ambazo zimechukuliwa zimekwenda hatua kwa hatua. Kulikuwa na hatua ya kuonya, kuna hatua ya kuweka X na hadi hapo wengine wameshawahi kuhamia. Kwa hivyo kuna hatua nyengine ambazo taarifa zilitolewa na hatimaye hakuna lolote ambalo lilizingatiwa na ndio maana sasa serikali ya Mkoa ikachukua hatua ya kuvunja au ya kubomoa katika maeneo yale ambayo kwa upande mmoja maeneo haya yana umuhimu wa kipekee, ni maeneo ambayo yana rutuba ya kutosha kwa shughuli za kilimo na tukiangalia kwamba tunategemea sana uchumi wetu kutokana na kilimo pia lakini vile vile ni maeneo ambayo yanayategemea sana ni vyanzo vya maji.

Mhe. Naibu Spika, hivyo sasa naomba niwambie tu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba Serikali haina dhamira ya kumkomoa mwananchi wake na badala yake ni hatua ambazo tunachukua ili tusijetukafika siku kama hivi ambavyo kuwa maeneo mengine yanajitokeza. Kwa mfano kama Mwanakwerekwe na kwengineko kwa kuziba mitaro na mambo mengine. Hivyo nawaomba Waheshimiwa walielewa hilo na watusaidie sana katika kuona kwamba tunachukua hatua kwa kuwaelimisha wananchi wetu ili haya mambo yasijirejee tena na tukaweza kulaumiana kwa kila siku.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la Michenzani pia sambamba na majibu yanafanana na hayo kwamba maeneo yale kama tulivyoona haikuwa ni maeneo ambayo yaliruhusiwa watu kujenga majengo ya kudumu. Mhe. Naibu Spika, ilipita sehemu ambayo kwa kuwa waliruhusiwa katika kufanya biashara katika maeneo kama ni *temporary*, lakini hatimaye wananchi walianza kuchukua utaratibu ule ule wa kujimilikisha kinyume na utaratibu. Lakini tunashukuru kwamba wananchi wa pale wakati walipotakiwa kuondoka waliondoka kwa hatua ambazo zipo nzuri bila ya kuvutana. Naomba nishukuru kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue fursa pia sitotaja majina moja kwa moja ya Waheshimiwa Wajumbe bali nitataja kwa jumla kama ambavyo nimeanza. Niseme suala la barabara. Suala hili takriban Waheshimiwa wengi ambao wamesimama walizungumzia sana katika kuona kwamba barabara za ndani zifanyiwe matengenezo. Umuhimu wa barabara kama wachangiaji wengine wameanza kusema kwamba zina imuhimu wa kipekee. Sio barabara zote ambazo zimetajwa kwamba zipo katika mamlaka yetu. Zipo barabara nyengine ambazo hazihusiki na huku lakini kuna barabara ambazo zinahusika.

Sambamba na hilo naomba niseme Mhe. Naibu Spika, katika kitabu chetu tumeorodhesha ni barabara zipi kwa mwaka huu wa bajeti ambao tunatarajia

kuzifanyia kazi. Sio kwamba tumetaka kufanya kwa baadhi. Cha msingi kutokana na uwezo wetu na mfuko wenyewe barabara ambazo tumeziainisha ndizo kwa mwaka huu bajeti ambazo ndizo tutakwenda nazo kama ambavyo labda tumeziainisha. Hizo barabara nyengine tutajaribu kutayarisha utaratibu maalum ambao Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutambua kwamba ni barabara zipi ambazo ni barabara za ndani na zile ambazo ni barabara ambazo *main road* zile ambazo hazihusiki na huku waweze kuzitambua zaidi.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo naomba nichukue fursa hii katika kumjibu Mhe. Mwakilishi aliyetaka kujua au aliyependekeza kuhusu ujenzi wa barabara ya Msingini Chake Chake. Barabara hii naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi tumekuwa tukijibu maswali yake katika kipindi cha maswali na majibu. Naomba kwa kutumia fursa hii nimwambie tena Mhe. Mwakilishi barabara hiyo ni kwamba katika mwaka huu wa fedha tumeipanga utekelezaji wake utaanza mara moja. Kwa sababu tayari tumeshapita hatua mbali mbali kufanya *design* kuangalia na kuithaminisha na hatua zitafuata na naomba nimpe matumaini hayo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, katika ujenzi wa soko la Kinyasini na Konde Mkwajuni na Gamba, nadhani Mhe. Mwakilishi nimwambie kuhusu masoko haya hayapo katika jukumu letu sisi. Sisi hatujui ni nani aliyepewa *tender* na ni thamani gani. Sisi tunachosubiri ni kukabidhiwa masoko pale ambapo kuwa yatakamilika. Nimuombe Mhe. Mwakilishi asubiri Wizara husika ya Kilimo kupitia mradi wa *MIRVAP*, nadhani watakuwa na majibu ambayo yatakuwa ni sahihi sana. Mimi kwa hili naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi masoko haya, sisi tunasubiri tu tukabidhiwe tuanze utekelezaji na ndiyo yataanza kuwa ya kwetu.

Mhe. Naibu Spika, kuna Waheshimiwa wengine wamezungumzia kuhusu masuala ya mahanga, maaskari na mambo ya sare nadhani haya majibu yameshatolewa na Mhe. Waziri wa Fedha, haya sina haja ya kuyajibu. Mhe. Ussi Yahya Haji kuhusu umiliki wa maeneo katika vikosi vyetu. Nadhani jambo hili tayari tumeshaanza kulichukulia hatua na takriban vikosi vingi sasa hivi tayari sasa hivi wameshapata hati miliki na yale maeneo ambayo yamebakia hatua nyengine za utaratibu zinaendelea katika kuona nalo tunakamilisha kazi hii. Ni imani yangu tutakamilisha muda sio mrefu sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa kuhusiana na ulipaji wa stahiki za likizo kwa Idara maalum. Nadhani jambo hili nalo nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli stahiki za likizo zilichelewa kulipwa lakini wafanyakazi kutokana na

kukabiliwa na ufinyu wa bajeti kwa fedha. Hata hivyo bajeti ya likizo tayari imeshaingizwa na katika maombi ya mwaka huu wa fedha nadhani hayo yote yatatatuka haraka hali itakavyoruhusu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu idadi ya watu wa Mkoa wa Kusini Pemba na asilimia yake. Mheshimiwa hili alilizungungumzia lakini kubwa zaidi alitaka kuonesha ni jinsi gani vile ambavyo hisia zake kutokana na kuvamiwa kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi, kuonesha kwamba *population* ni kubwa lakini. Lakini hata hivyo tumesema idadi ya watu katika Mikoa ipo kwa mujibu wa sensa na makaazi ya mwaka 2012. Mhe. Mwakilishi nikuombe kwamba tusubiri hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha itakapofika hapa nadhani Mtakwimu atakuwepo katika maeneo hayo nadhani tunaweza tukaipata kwa usahihi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Waheshimiwa waliotaka kujua Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhusiana na ukumbi uliojengwa wa mikutano. Naomba niwambie Waheshimiwa Wawakilishi ambao waliotaka kujua hali hii ni kwamba mradi huu ni mradi ambao unatekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Kuhusu namna ya Mkandarasi ambaye aliyepewa kazi hii, nadhani ni mkandarasi ni mzawa na mpaka sasa hivi ameshatumia kiasi cha shilingi milioni mia nne na arubaini na nne, laki tisa, tisini na tisa na thamanini na nane.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kambi ya KVZ Micheweni vile vile ambayo inajengwa na mkandarasi gani alitaka kujua. Lakini naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba ujenzi huo unajengwa huo na Kikosi cha KVZ na mpaka sasa hivi jumla ya shilingi milioni nne na laki nane ndizo ambazo zimeshatumiwa ambazo fedha hizi ni *OC* na si fedha kutoka sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza yeye alitaka kujua madeni tunayodaiwa Idara Maalum kwa wafanyabiashara na vile vile na sisi ambao tunawadai. Naomba nimjibu kwa muhtasari tu, nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba katika Kikosi cha JKU jumla ya shilingi mia tatu, tisini na nne, laki saba tisini na tatu elfu. Hizi JKU wanadai. Vile vile na wao pia katika Kikosi cha KVZ jumla ya shilingi mia sita thalathini na tisa milioni, laki tano hamsini na sita, mia moja na sitini na mbili, hili ni deni ambalo linadaiwa Chuo cha Mafunzo. Vile vile na wao wanadai shilingi tisini na saba milioni, laki mbili na elfu tisa na mia tano.

Mhe. Naibu Spika, kwa haraka haraka vile vile na madeni mengine ambayo ya JKU kama nilivyosema ni kwamba yamechanganuliwa katika utaratibu wa umeme na mambo mengine nayo pia tunadaiwa, lakini kwa muhtasari naomba

nimjibu hivyo na taarifa nyengine zinaweza zikapatikana muda ambao utakuwa ni muafaka kwani zinarekebishwa zaidi.

Mhe. Mussa Foum Mussa kuhusu madawa ya kulevya, alitaka kujua kwamba agizo hili au *operation* hii inafanyika kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi pekee na sio kwa Mikoa mengine. Natala nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba agizo hili ama *operation* hii inafanyika kwa Mikoa yote ya Zanzibar, yaani Unguja na Pemba na kwa kila mmoja anatekeleza agizo kwa mujibu wa jiografia na maeneo ambayo husika. Lakini tuamini tu kwamba Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wanafanya kazi nzuri na nadhani muda utakapofika basi tutaona kwa uwazi zaidi hatua ambazo zinachukuliwa. Kila mmoja anakuwa anastahili ambayo anaitumia katika kukabiliana na jambo hili kubwa na jambo ambalo linauzito wa pekee.

Mhe. Naibu Spika kuhusu Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mhe. Ame Haji, Mhe. Hamza Hassan Juma vile vile Mhe. Makame Rashid Shamsi kuhusu ugatuzi na namna ya kufanikisha majukumu yaliyogatuliwa. Nadhani Waheshimiwa hata Mhe. Naibu Waziri wa Elimu alisema kwamba suala hili ni la Kikatiba na pia matakwa ya Sera. Nadhani mwaka 2012 Sheria Na.7 Mheshimiwa kaielezea na sina haja ya kuielezea. Lakini kuhusu lini tutaanza nadhani shughuli imeanza na punde tu bajeti ikipitishwa nadhani utekelezaji wake ndio utaanza rasmi.

Mhe. Makame Rashid Shamsi na yeye pia alitaka kujua mamlaka za Serikali za Mitaa, kukabiliwa na uhaba wa wafanyakazi wenye taaluma stahiki na mabadiliko ya wafanyakazi kwa mkataba. Mheshimiwa niseme kwamba jambo hili ni kweli, mamlaka za Serikali za Mitaa zinakabiliwa na uhaba kweli na wafanyakazi wake. Lakini sambamba na hilo changamoto hii tayari imeshabainishwa na tumeshawasilisha maombi kupata kibali cha kuwaajiri wafanyakazi ambao katika nyanja tofauti tofauti, wakiwemo Wahasibu, wanasheria na maafisa wengine ambao watafanya kazi hizo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Mhe. Waziri wa Afya yeye aliunga mkono hoja na akasema kwamba ameunga lakini alitaka kuona tofuti kidogo kujua kwa nini kumekuwepo na bajeti tofauti kuonekana kwamba Mkoa wa Mjini/Magharibi umekuwa na bajeti ndogo kuliko Mkoa wa Kusini Pemba.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba hili lilitokana na shughuli za Mkoa husika na vipa umbele vyao na katika hili nadhani ufafanuzi zaidi uko hivyo. Mhe. Yussuf Hassan Iddi yeye kuhusu ni lini Masheha wapya, Shehia mpya zitapatiwa Masheha. Naomba nimwambie Mheshimiwa Mkoa wa

Mjini/Magharibi ni mkoa ambao ni nyeti kidogo na una mazingira nyeti kidogo. Vile vile naomba nimwambie Mheshimiwa taratibu Mhe. Mkuu wa Mkoa anaendelea kuzifanya na pale atakapokuwa tayari nadhani wakati wowote basi ataweza kutekeleza jambo hilo na kwa wakati na kwa uhakika zaidi na umakini zaidi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa nakupa muda wa dakika tano umalizieWwaziri pia naye pia atakuja kujumuisha. Kwa hivyo Waziri ana saa nzima na unachukua muda wa Waziri sasa.

Mhe.Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote na naomba niunge mkono hoja asilimia mia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha jioni ya leo kufika hapa na kuja kufanya kazi hii muhimu kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali ambazo zimeelezwa na Waheshimiwa Wajumbe. Kwa jumla ya wachangiaji ambao wamechangia Mhe. Naibu Spika, waliochangia kwa kusema moja kwa moja ni Waheshimiwa Wajumbe 37 na waliochangia kwa maandishi ni 23. Kwa hivyo jumla ya wachangiaji wote ni 60. *(Makofi)*

Tabaan Mhe. Naibu Spika, nikiamua kutoa ufafanuzi na kujibu hoja kwa Wajumbe wote, muda ambao umewekwa kwa mujibu wa Kanuni ya 95(5) nitaupita na sitoweza kumaliza hoja za Waheshimiwa Wajumbe. Lakini nataka niwathibitishe kwamba majibu yao yote yapo na mimi nitaomba baadae nikuombe Mhe. Naibu Spika, yake ambayo sitaweza kuyajibu yaingizwe kwenye *Hansard* ili iwe ni kumbukumbu ya yale ambayo Serikali itakuwa imeyatolea ufafanuzi wa hoja mbali mbali za Wajumbe.

Mhe. Simai pia ali- *raise* hoja ya kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 88 Mawaziri tunatakiwa tujibu kwa ufasaha na kwa uhakiki. Nathamini mchango wake huo na mimi leo nitajitahidi sana yale nitakayowahi kuyajibu, niyajibu kwa ufasaha wa kueleweka na wala hatutababaisha. Lakini kwa yake ambayo sitaweza kuyajibu Waheshimiwa wote niwaombe watumie utaratibu tuliojiwekea Barazani kwa mujibu wa Kanuni ya 95, haya tuyapeleke kwenye *Hansard* ili iwe ni kumbukumbu ya maelezo ya Serikali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba kwa heshima zote nianze kutoa ufafanuzi kwa Waheshimiwa Wajumbe au nianze kuwataja Wajumbe ambao wamechangia hotuba hii.

1. Mhe. Mwantatu Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum
2. Mhe. Simai Mohammed Said
3. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
4. Mhe. Ali Khamis Bakari
5. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
6. Mhe. Suleiman Makame Ali
7. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
8. Mhe. Ame Haji Ali
9. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
10. Mhe. Rashid Makame Shamsi
11. Mhe. Hamza Hassan Juma
12. Mhe. Ali Salum Haji
13. Mhe. Viwe Abdalla Khamis
14. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
15. Mhe. Ali Suleima Ali
16. Mhe. Ussi Yahya Haji
17. Mhe. Miraji Khamis Mussa
18. Mhe. Khadija Omar Kibano
19. Mhe. Mussa Foum Mussa
20. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
21. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
22. Mhe. Mohammed Said Mohamme
23. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
24. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
25. Mhe. Hidaya Ali Makame
26. Mhe. Mussa Ali Mussa
27. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
28. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
29. Mhe. Suleiman Sarhan Said
30. Mhe. Omar Seif Abeid
31. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
32. Mhe. Makame Said Juma
33. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
34. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
35. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

36. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango
37. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Mhe. Naibu Spika, hao walichangia kwa kusema moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi:-

1. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
2. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
3. Mhe. Hamida Abdalla Issa
4. Mhe. Bahati Khamis Kombo
5. Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji
6. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
7. Mhe. Nassor Salim Ali
8. Mhe. Juma Ali Khatib - Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum
9. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
10. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
11. Mhe. Waziri wa Afya
12. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
13. Mhe. Zaina Abdalla Salum
14. Mhe. Salma Mussa Bilal
15. Mhe. Shehe Hamad Mattar
16. Mhe. Shaib Said Ali
17. Mhe. Mgeni Hassan Juma
18. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
19. Mhe. Said Omar Said
20. Mhe. Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru wote wale ambao wamechangia na nina imani kwamba Wajumbe wengine wote kwa sababu ya muda wangepata nafasi na wao wangechangia, na kwa nini wangechangia hotuba hii kwa sababu kama walivyosema wenyewe katika michango yao kwamba hii ni Ofis ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, ni Ofisi inayowagusa wananchi moja kwa moja katika kuwashughulikia. Kwa hivyo niwashukuru sana kwa michango yao na mimi nitajitahidi kutoa ufafanuzi ili Waheshimiwa Wajumbe waone kwa wale ambao nitabatika na wale nitakaokuwa sikubahatika waelewe kwamba majibu yote yapo. Lakini niwaomba tuweze kukubaliana na majibu hayo ili kuendelea kuwatumikia wananchi wetu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimshukuru sana Makamo Mwenyekiti wa Kamati na ushauri wao ambao wametupa toka kwenye Kamati na ule ambao wametupa kwenye hotuba yao ya kuchangia katika hotuba yetu ya bajeti. Nataka niwambie kama tulivyokuwa tunachukua ushauri wao wakati wa kutupitia na kutukagua utekelezaji wa majukumu yetu, basi na huu ushauri ambao wametuletea na ambao wameuleta mbele ya Baraza lako Tukufu tutajitahidi sana tuufanyie kazi. Na yale mengine kama baadhi ya Mawaziri waliopata nafasi ya kuchangia wametoa ufafanuzi, naomba ufafanuzi ule uhesabiwe kama ni sehemu ya majumuisho haya ambayo nimeyatoa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo Mhe. Makamo Mwenyekiti naishukuru sana Kamati na maoni yao yote tunayachukua na tutayafanyia kazi. Lakini nikija kwa wachangiaji mmoja mmoja, nataka niseme kwamba hoja nyingi ambazo zimejitokeza na kuchangiwa na watu kuanzia mmoja na kuendelea. Kwa hivyo wale ambao mimi nitajaribu zaidi kutaja hoja kwa ujumla na kutoa ufafanuzi kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kutolea ufafanuzi lile suala la masoko ambayo wameyasema kama lilivyokuwa *raised* hapa, yale masoko ambayo yanashughuliwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi pale tutakapokabidhiwa, ndipo pale ambapo sisi tutaanza kuyaendesha. Kwa mujibu wa Sheria Mamlaka za Serikali za Mitaa ndizo zenye jukumu la kundesha masoko haya. Kwa hivyo niwaombe tu kwamba yale masoko ambayo bado Wizara ya Kilimo wenyewe wametwambia wayafanyie kazi, kwa mfano soko la Tumbe, basi niombe kwamba tuvute subra ili Wizara ya Kilimo wakamailishe kazi na waweze kutukabidhi.

Lakini kwa mfano soko la Tumbe Mhe. Mwakilishi nakuomba sana na wewe kwa sababu ni Mwakilishi wa wananchi wende ukawaelimishe wananchi. Kwa sababu kinachoonekana pale kunafanywa kwetu kule tunaita, "hayalizi". Maana yake mambo ambayo hayana msingi. Kwa hivyo wende ukawaelimishe wananchi uwaeleze kwamba Serikali nia yake ni kuwajengea masoko kwa ajili ya kutoa huduma kwao wao. Hivyo yale maelekezo yatakayotolewa na Serikali basi wakubaliane nayo ili tuweze kuwahudumia wananchi na lile lengo lililokusudiwa liweze kupatikana, si vizuri sana *World Bank* wakija wakiona wametupa msaada ule na halafu kile kitu hakitumiki. Tungeomba sana, nimesema Tumbe lakini yapo na maeneo mengine.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wawakilishi wenye masoko kama haya ambayo kuna utata kati ya wananchi na Serikali, nadhani tushirikiane na

Serikali za Wilaya na Mikoa tuwaelimishe wananchi hawa ili waweze kusaidia na zile soko ziweze kufanya kazi zake vizuri.

Mhe. Naibu Spika, lakini ombi la Mhe. Simai Mohammed Said kuhusu soko la Kaebona. Kama nilivyosema wengi hapa wamezungumzia suala la ugatuzi wa madaraka, wengine kila mmoja na maoni yake, wengine walikuwa wanaona Serikali inafanya haraka kuli-*address* hili jambo. Lakini mimi nadhani faida yake ni kwamba kwanza suala la ugatuzi wa madaraka nataka nilizungumzie hapa. Suala la ugatuzi wa madaraka limeelezwa ndani ya Katiba ya Zanzibar. Kwa hivyo ni jukumu letu sisi Serikali na wananchi kwa jumla kutafuta namna ya kuweza kulitekeleza. Suala hili limetungiwa Sera, suala hili limetungiwa Sheria na suala hili nimelitengenezea Kanuni na bahati nzuri Kanuni zake tayari nimezishazisaini kwa ajili ya kutaka kutumika.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo hatuna sababu ya hili jambo sasa kulichelewesha na madhumuni yake makubwa ni nini, kupeleka mamlaka ya nchi kwa wananchi wenyewe. Kwa maana mipango yote ya maendeleo iaanzie kule chini, iletwe huku juu. Kwa hivyo suala la mpango wa Soko la Kaebona, kwanza ni jambo kweli litakaloleta mwelekeo mzuri kwa Mkoa wa Kusini na wananchi wa Mkoa wa Kusini kwa jumla. Kwa hivyo Halmshauri ya Wilaya ya Kati lakini na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, kupitia Kamati ya Maendeleo ya Mkoa, jambo ambalo litaibuliwa na wananchi kutoka ngazi ya Shehia, kwenye Mabaraza ya Wadi na hatimaye sisi kama Wawakilishi wa wananchi na wajumbe kwenye hiyo Kamati ya Maendeleo ya Mkoa.

Kwa hivyo niombe Mkoa wa Kusini, jambo hili lianze kulipanga kwa kushirikiana na Halmashauri husika, sisi Serikali Kuu hatuna tatizo kabisa na jambo hili kwa sababu ni jambo ambao litaweza kutatua matatizo ya wananchi kupeleka bidhaa zao katika masoko ya mbali.

Kwa hivyo Mhe. Simai jambo hili ulilolileta ni zuri na sisi tunaliunga mkono na hatuna sababu ya kulizuia. Na katika suala zima la ugatuzi Mhe. Naibu Waziri wa Elimu kuhusu sekta ambazo tumezigatua, kwa sasa hivi sekta ambazo tumeamu tumezigatue ni sekta ya elimu, afya na kilimo. Elimu tumesema Elimu ya Msingi, Elimu ya Maandalizi na Msingi na yake mambo ya Kisera, Kisheria na Miradi Mikubwa ya Maendeleo bado inabakia katika Sekta hizi.

Afya ya msingi wengi, hapa baadhi ya Wajumbe samahani sitowataja mmoja mmoja wamezungumzia tatizo la hivi sasa la kila kitu wananchi kutegemea

kifanywe na Serikali, hata kusafisha taka mbele ya mlango wako unataka ije Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa utaratibu huu wale Wakaguzi wa Afya ambao tumeanza kufanya kazi nao ndio ambao watafanya kazi moja kwa moja kule kwa wananchi na kufanya kazi siku hadi siku, badala ya wakaguzi wale kuwepo Wizara ya Afya na huku hawajui nini kinachofanyika. Kwa hivyo lengo ni kuhakikisha kwamba huduma zilizo bora kwa wananchi zinapatikana badala ya kuwaweka watu Makao Makuu ya Wizara na halafu wakawa hawana usimamizi wa karibu kule kwa wananchi, ndilo lengo. *(Makofi)*

Sekta ya kilimo vile vile. Sekta ya kilimo hakina msingi wala nini. Maana yake kilimo ni kilimo tu nacho tumeona ni vizuri. Lakini ni kweli yako baadhi ya mambo ambayo tunayafanyia kazi hata kama hayagatuliwa. Kwa hivyo mimi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kwamba jambo hili ni jema na wengine wamezungumza kwa udogo wa nchi yetu, pengine kwa nini tumeamua kufanya hivi. Haja yetu sisi udogo huu tulionao, maendeleo yafike kwa wananchi kwa haraka zaidi na ule utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi uweze kutekelezeka na tuweze kufanya tathmini vizuri, na tutambaini nani sasa hawajibiki. Na suala la wataalamu ndio maana tumeunda vikundi vitano kwa ajili ya kubainisha na kutambua mahitaji na kuweza kuelimisha.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, tumeunda kikundi cha uwelewa "*awareness"* ambacho kinaongozwa na Katibu Mkuu Wizara ya Habari. Tumeunda kikundi cha fedha ambacho kinaongozwa na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Wajumbe wake, tumeunda kikundi kinachoshughulikia masuala ya sera na sheria ambacho kinaongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu, tumeunda kikundi cha raslimali watu ambacho kinaongozwa na Naibu Katibu Mkuu anayeshughukia masuala ya Utumishi, tumeunda kikundi cha miundo ya taasisi, kujua hizi mamlaka za Serikali za Mitaa ziweje na kwa miundo gani, kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa Umma.

Kwa hivyo Serikali hatujakurupuka hata kidogo kuweza kulianzisha jambo hili, tunaelewa ugumu wake na tunaelewa changamoto zake. Kwa hivyo hivi vikundi tulivyovibainisha tumevipa muda wa miezi miwili viweze kuleta *result* ya ripoti ni watumishi wa namna gani hao wanaohitajika.

Mhe. Naibu lakini hata katika Mikoa tumeamua kuunda sekreteriati za Mikoa ambazo zitakuwa ziko chini na Mhe. Mkuu wa Mkoa na Mwenyekiti wake ni Katibu Tawala wa Mikoa. Hawa wanaitwa Makatibu Tawala Wasaidizi ambao watakuwa wapo pale kwa mujibu wa sekta. Hivi sasa Maafisa walioko

Wilayani na Mikoani hawawajibiki kwa Wakuu wa Mikoa, wanawajibiki kwa Makatibu Wakuu wa Wizara zao. Lakini kazi zinazofanywa zinafanywa kule kwa wananchi. Kwa hivyo usimamizi wa siku hadi siku unakuwa haupo. Ndio maana Serikali imekuja na zile sheria mbili. Kwa hivyo tunachowaomba Waheshimiwa Wajumbe kwamba jambo hili tunalifanya kwa uangalifu mkubwa na tunalifanya kwa umakini mkubwa na hatutegemei kufeli.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu Tanzania Bara, tunatambua kwamba baadhi ya nchi jambo hili limefeli, lakini sio mifano mibaya inaweza ikaja ndani ya nchi yetu. Mimi nadhani sisi tushirikiane sote kwa pamoja kwa sababu sote tuliomo humu ndani, jambo hili ni wahusika wakuu, kwa lugha ile nyengine ambayo Maalim Haroun Ali Suleiman huwa hapendi tuiseme wadau, kwamba sote sisi ni wahusika katika jambo hili. Kwa hivyo si jambo la Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa peke yake, ni jambo la nchi nzima, ni jambo la serikali nzima, ni jambo la wananchi wote. Kwa hivyo hili tukifanikiwa tumefanikiwa sote na tukifeli itakuwa tumefeli sote. Lakini kwa mujibu wa serikali pamoja na wananchi tulivyojipanga hatutegemei jambo hili tufeli kwa sababu tumezingatia zile changamoto zilivyo.

Mhe. Naibu Spika, wengine wamezungumzia suala la ukusanyajai wa kodi. Ni kweli nikiri kwamba tuna changamoto kubwa ya ukusanyaji wa ada mbali mbali zinazotolewa na *local government,* yaani kwa maana ya Halmashauri na Mabaraza ya Manispaa. Ndio maana kwa mwaka ujao wa fedha tunataka kwenda kwenye mfumo wa elektroniki, kwa sababu utaratibu huu wa *manual* unatupa shida na ni dhahiri kwamba yako baadhi ya mapato yanavuja. Kwa hivyo niseme kuhusu suala hili la ugatuzi likishakuanza litatua changamoto nyingi ambazo sasa tunazo. Kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe waridhike na maelezo hayo kwamba ndivyo serikali ambavyo tumejipanga.

Mhe. Naibu Spika, mfumo wa fedha utabadilika, risiti zile ambazo Mhe. Ali Salum Haji umesema kwamba kila mmoja na risiti yake, mfumo huu utabadilika. Utaratibu tunaotaka kuuweka ni kwamba yule mkusanya kodi, kwanza zile ada zote zipo na kila Mkurugenzi atakuwa anazijua, Katibu Mkuu atazijua, hata mimi Waziri na Waziri wa Fedha utaunganishwa mfumo ambao yule mkusanyaji tutakuwa tunaona moja kwa moja kile anachokikusanya. Kwa hivyo tutajitahidi sana na serikali imejipanga kufanya hayo yote.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Simai Mohammed Said pia alizungumzia na Waheshimiwa wengine wamezungumzia suala la *fire hydrate* katika miji yetu. Ni kweli tunakubali kwamba Mji Mkongwe hili jambo lilifanywa vizuri wakati ule. Lakini katika maeneo mengi ambayo yanajengwa sasa jambo hili halipo na

ndio maana serikali yetu inakuja na mpango wa ile *master plan* ya kupanga miji upya, likiwemo na lile suala la Mhe. Suleiman Sarahan Said alilolizungumza. Ni kweli katika mji mpya wa Tunguu hakuna miundombinu, kila mmoja anachimba kisima chake cha maji. Njia zipo lakini hazikuwekwa vizuri katika miundombinu. Tunataka kuondoka huko na hili suala tukitaka tulifanye sisi tu kupitia Halmashauri litatushinda. Lakini hili ni jambo nchi nzima. Mpango huu utakapozinduliwa si muda mrefu Mhe. Rais atazindua mpango huu rasmi kwa ajili ya miji mipya iliyopangwa kwa mujibu wa *master plan*. Likifanyika hilo, ile changamoto uliyoizungumza Mhe. Simai itaondoka. Kwa hivyo itakuwepo miundombinu yote ambayo inastahiki kuwepo kwenye miji.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la kufunga njia ya Ikulu ni jambo la kiusalama na la kiulinzi. Lakini lile geti lilowekwa pale kwanza ni *automatic*, unaliendesha unavyotaka, inapotokezea haja ya kufanya hilo ulilolisema basi mara moja tunawasiliana na wahusika. Lengo la pale ni kuimarisha ulinzi wala si kuzuia huduma nyengine za jamii. Kwa hivyo itakapotokezea haja kwamba kuna moto tuseme Mwenyezi Mungu aepushe mbali, umetokezea pale Mahakamani, lile litafunguliwa ile gari ya Zimamoto ipite, ndio madhumuni yake. Kwa hivyo si kikwazo cha kuzuia shughuli nyengine za huduma za jamii zisiweze kuendelea. Lakini tumefanya vile kwa sababu ya unyeti na usalama wa ile nyumba, ile ndio nyumba Namba moja Zanzibar. Kwa hivyo lazima tuilinde na tuimarishe ulinzi wake na tuhakikishe vilivyomo mule ndani vinalindwa, waliokuwemo mule ndani wanalindwa. Kwa hivyo kile ndio kiwanja Namb moja na ndio nyumba Namba moja Zanzibar. Hivyo lazima tui-*protect* kwa nguvu zetu zote. Kwa hivyo geti lile liliopo pale, lipo kwa madhumuni ya kulinda usalama wa ile nyumba Namba moja, ile ndio nyumba yetu kuu. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nasikia watu wanaitafuta kwa kutaka wakaingie mule, lakini bado tunasema wakitaka kuingia mule wageuke kunguru wende wakatue juu ya paa halafu waondoke waende zao. Kwa hivyo, nilipenda niseme hilo.(*Makofi*).

Mhe. Ali Khamis Bakar kuhusu ufikishaji wa umeme kwenye bwawa la Zimamoto Uwanja wa Ndege. Nadhani hili tumeshawasiliana na wenzetu wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Jambo hili tunalitambua na wenzetu wamelipokea na karibu umeme utafikishwa ili lile bwawa liweze kufanya kazi na hatimae magari yetu ya Zimamoto yasiwe na tatizo la ujazo wa maji pale inapohitajika kufanya hivyo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kuhusu gari ya Zimamoto, nadhani ufafanuzi wake kwamba magari yale yaliyopo Uwanja wa Ndege yamenunuliwa kwa madhumuni ya kuweka viwango vya kimataifa kwa mujibu wa sheria za kikao *International Civil Aviation Organization* (*ICAO*) yapo pale. Na sisi sahihi kusema kwamba magari yaliyopo pale hayana kabila.

Mhe. Naibu Spika, magari yaliyotoka Afrika ya Kusini kabila lake ni *Scania* na magari yaliyotoka Dubai ni aina ya *Falcon VI*, yenye *engine* ya *caterpillar* na yamesibitishwa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa. Kwa hivyo namuomba Mheshimiwa aelewe hilo, yale yana kila kitu atakapotaka taarifa zake, taarifa tunazo basi hakuna tatizo lakini si hivyo ambavyo imesemwa. (*Makofi*).

Mhe. Ame Haji Ali ametoa ushauri mwingi tu na hasa katika vituo vyetu vya KMKM Kibweni, Kibwengo na kituo kile cha Zimamoto cha Kigunda. Mheshimiwa ushauri wake tunauchukua na baadhi ya maelezo ambayo ameyatoa Mhe. Waziri wa Fedha nadhani turidhike kwamba serikali inafanya juhudi ya kuyafanya hayo.

Mhe. Rashid Makame Shamsi kuhusu Kiwanda cha Nguo na Kiwanda cha Viatu. Mimi najua Mheshimiwa wewe ni muhusika mkuu na unauelewa mkubwa kuhusu hili lakini kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha kwamba serikali na Wajumbe wengi mmechangia hili, serikali imeona umuhimu wa kuwapa mavazi askari wetu ya kutosha. Kwa maana ya sare zinazojumuisha viatu na ndio maana serikali imechukua juhudi ya kuwapeleka wataalamu India kwa ajili ya kuangalia mashine ambazo zitafaa kufungwa kwenye Kiwanda kile cha Viatu cha KVZ na tunatarajia kuwa na mpango mkubwa wa viwanda vile kuvijenga pahala pamoja, ili tuepukane na hili tatizo la uchache wa sare lakini pia sare zetu tuzishone wenyewe, na viatu vyote tuvizalishe wenyewe. Kwa hivyo serikali imeamua na kama alivyosema Waziri wa Fedha serikali tayari na ilionekana kwenye kitabu changu kwamba ni asilimia 3.3 tu ndio fedha zilizoingia katika Kiwanda cha Viatu.

Mhe. Naibu Spika, lakini nataka niseme kwamba fedha zote zilizopangwa kwenye mradi wa maendeleo milioni 800,000,000 zimeingia lakini zimeingia baada ya mwezi wa Machi, na tayari sasa hivi tuko kwenye *process* ya kuangalia utaratibu wa kufungua *LC* ili hivyo vifaa vinavyohitajika viweze kuja na kile kiwanda kiweze kufanya kazi kwa *capacity* kubwa zaidi kuliko ya sasa hivi. Na pale kilipo kiwanda tutakiondosha tunajenga eneo jengine mule mule ndani ili kiwe na nafasi kubwa zaidi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Kiwanda cha Nguo vile vile tutakihamisha baadae Amani na kukileta katika maeneo yetu ya Idara Maalum ili tufanye kazi kwa uhuru zaidi na tufanye kazi kwa maeneo ambayo mazuri. Kwa hivyo Mheshimiwa nikushukuru na wale Waheshimiwa wote waliotoa maoni haya waone kwamba masuala yao nimeyatolea ufafanuzi kwa hili jibu la Mhe. Rashid Makame Shamsi.(*Makofi*).

Mhe. Mohammed Said Mohammed kuhusu kushindwa kufikia katika matukio 120 ya Zimamoto. Tathmini imefanyika na sababu ya kushindwa kufika katika matukio kwa wakati ni kutokupata taarifa mapema. Kuna mambo mawili. Kwanza taarifa kuchelewa kutufikia, bado wananchi na hili tutaongeza elimu ili wazijue zile namba zetu. Maana yake kwa mfano, tukio limetokea sehemu za Mombasa lakini mtu anapiga simu kwenye kituo cha Mjini, wakati akipiga simu kwenye kituo kile cha pale Mwanakwerekwe gari inafika haraka zaidi na kuwahi mapema. Kwa hiyo tutajitahidi tutoe taaluma ili wananchi wetu waelewe kwanza namba zetu za simu.

Mhe. Naibu Spika, lakini ukosefu wa miundombinu, ukosefu wa *fire hydrate* ni chanzo vile vile kinachosababisha baadhi ya matukio tusiweze kuyafanyia kazi. Mara nyingi tunapokwenda tunakuta wananchi wameshawahi kwa sababu sisi tunakwenda na gari, lakini maji yakimalizika kwenye gari lile hatuna sehemu nyengine ya kupata yale maji ili tukaweza kukabiliana na lile tukio. Na ndio maana nikasema haya tunayatafakari na tutaweza kuyafanyia kazi vizuri ili haya matukio yote, nia yetu tuweze kuyafanyia kazi na kuokoa wananchi na mali zao, ikiwezekana tuokoe kwa *hundred percent* badala ya kuokoa hivi ambavyo tumekuwa tunaokoa hivi sasa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nataka nitolee ufafanuzi vile vile kwamba gari nne zile walitoa kwamba askari hawana nguo, hawana mavazi yale ya Zimamoto. Katika gari mpya ambazo zimekuja kila gari ina *set 4.* Lakini tunatarajia hivi karibuni si muda mrefu pengine ndani ya wiki mbili tutapokea nguo maalum za kuzimia moto kutoka Ujerumani zipatazo *set 100*. Kwa hiyo jambo hili tutalifanyia kazi vizuri, hivyo askari wetu wale wanaokwenda kwenye matukio watakuwa na nguo ambazo wanafanyia kazi.(*Makofi*).

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf kuhusu magari yaliyonunuliwa kufuata taratibu ya manunuzi, taratibu na *tender* zilipitishwa kabla ya kufanya manunuzi. Mhe. Naibu Spika, taratibu zilifuatwa Waheshimiwa hasa hizi za magari ya Zimamoto.

Kuhusu kituo cha Wete kuwa kichakavu, ni kweli tunakubali kama walivyosema Wajumbe wengine kwamba maeneo yetu mengi, miundombinu yetu mingi wala hapa siwezi kujisifu nikasema kila kitu kiko sawa, hapana. Ndio maana serikali kama alivyosema Waziri wa Fedha tumeanza kutekeleza jambo hili awamu kwa awamu. Kwa hivyo tumeanza na hivi vikosi vyengine tutaangalia uwezekano wa kuweza kuviangalia na serikali inatafuta njia mbali mbali kutoka kwenye bajeti yake, lakini kutoka pia kwenye fedha za msamaha wa madeni ili tuweze kusaidia miundombinu ya vikosi vyetu vyote ikiwemo majengo ya kufanyia kazi pamoja na mahanga ya askari.

Kuhusu suala la kujenga uzio Mheshimiwa nadhani tunalipokea tutajaribu kulifanyia kazi, kama tunaweza kufanya kazi kwa pesa zetu za udhalishaji wa ndani, tutalifanyia kazi hilo. Kwa hivyo kuhusu hiki kituo cha Wete na vituo vyengine na wale wote waliochangia kuhusu vituo nakubaliana nao na serikali inalifanyia kazi jambo hili.

Kuhusu suala la sare nadhani nishalizungumza kwamba zile sare kutoka Ujerumani ni *set 200* sio 100 samahani. Kwa hivyo tutakuwa na sare za kutosha.(Makofi).

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa kuhusu kuchelewa kufika kwenye ajali, nadhani nishaieleza, ajali za moto nishaeleza vya kutosha lakini ajali za baharini. Kutokana na matukio mbali mbali ambayo yametokea katika nchi yetu ya kuzama kwa meli ya *MV. Spice Islander na Skagit.* Ni kweli tumepata maumivu makubwa. Kwa kuona hivyo serikali kupitia bajeti hii ya mwaka 2017/2018 tunanunua boti mbili za kisasa. Moja itakuwa Pemba na moja itakuwa Unguja. Nia ya serikali kila Wilaya tupate boti moja. Kama tutakavyojenga vile vituo vya uokozi kwa sababu ya ufinyu na ukomo wa bajeti, serikali tutanunua boti mbili kwa kuanzia na hizi boti zina uwezo wa kuwa na *crews* 17 ndani yake. Lakini zitakuwa na uwezo wa vifaa vya uokozi pale tukio linapotokea kuokoa watu 600 kwa wakati mmoja, pia hizi boti zitakuwa zina uwezo wa kwenda *nautical mile 60* kwa saa. Kwa hivyo tunahisi katika masafa ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba ikiwa kila boti ina vifaa vya uokozi vya watu 600, kwa hivyo tutakuwa na 1,200. Kwa hivyo unawahi kufika kwenye tukio na kurudi katika kituo cha uokozi bila ya matatizo yoyote. Hivyo tuvute subra serikali ina nia njema na tumejifunza kutokana na matukio haya ambayo yalitokea kwa kuzama kwa meli.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile tutakuwa na vifaa vya kisasa tukishapata taarifa kwamba pahala fulani uso wa membe imezama meli, tunarusha vifaa

hivyo, vinakwenda vinachukua picha ya *satellite* ili kuwaongoza *divers* wanapokwenda pale kuwa na uhakika wa kitu wanachokifanya.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Uwanja wa Ndege wa Pemba kutumia chumba kimoja. Hili jambo tutalichukulia hatua ya dharura *(fast track)* ili kuzungumza na wenzetu wa Mamlaka tuone tunakabiliana na tatizo hili ili liweze kupatiwa ufumbuzi.(Makofi).

Mhe. Abdalla Maulid Diwani vipi wizara imejipanga katika kutatua changamoto za upatikanaji wa vyeti, vizazi, vifo, talaka na kadhalika. Hivi jana waraka wa mfumo wa usajili umekwenda kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu, kikao kijacho cha serikali utakwenda kwenye kikao cha serikali. Tunatarajia tuweke mfumo kwa Zanzibar nzima, Wilaya zote, tuwe na mfumo mmoja wa vyeti na namna ya upatikanaji wake. Mfumo huo ulianza kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi, tunataka tuupeleke mote kwenye Wilaya zote na kama nia ya serikali ya kuunganisha Idara ya Vizazi na Vifo na Vitambulisho, tayari miundombinu kupitia Idara hii ya Vitambulisho ipo katika Wilaya zote na mfumo huu utaunganishwa tuwe na *database* moja.

Mhe. Naibu Spika, wamesema baadhi ya Wajumbe hofu ya kwamba fedha zilizotengwa zile bilioni 2 nazo ni kidogo, ndio maana tumetenga kwenye mradi. Gharama zote za mradi wa mfumo huu ulikuwa ni shilingi milioni mia tisa na zaidi. Ndani ya bajeti yetu, ya ndani tumekata baadhi ya vifungu tumeweka mradi katika mwaka huu wa fedha wa shilingi milioni mia tano ili mfumo huu uweze kuanza kazi mara moja. Kwa hivyo niwaondoshe wasi wasi na jibu hili liende pia kwa vile vyeti vinavyochelewa kutolewa.

Vyeti vinachelewa kutolewa tu kwa sababu ya ule mfumo tulionao wa kizamani, lakini tunakwenda kubadilisha mfumo na tunabadilisha pia na Sheria ili tuweze kulifanya jambo hili kwa ufanisi zaidi. Kwa hivyo machungu aliyoyapata Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa kupata cheti cha mzee wetu, babu yangu nadhani tunataka mwaka ujao wa fedha tulimalize jambo hili ili wananchi wetu tuwaondoshee usumbufu.(*Makofi*).

Muda rasmi wa kupatikana vyeti. Ni kweli muda rasmi uliopo sasa hivi una changamoto zake lakini huo mfumo utakuja kuondosha, bila ya huo mfumo changamoto zitaendelea kuwepo. Kwa hivyo naomba tuvute subra ili hili jambo tuweze kulifanya kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, bei rasmi ya vyeti vya ndoa. Bei rasmi ya cheti cha kufungisha ndoa ni shilingi 5,000 ambavyo vile vinatolewa na Mapadri,

Makadhi na Masheha. Maana kuna Dini tofauti na kila mmoja anafungishwa ndoa kwa mujibu wa Dini yake. Kwa hivyo kile ni shilingi 5,000 na cheti sasa *certificate* ile ambayo unaweza ukaiweka ukutani kama kumbukumbu yako na tunahimizwa tufanye hivyo ile ni shilingi 5,000 na cheti rasmi kile ni shilingi 25,000. Na hivi hatutoi kwa faida kwa sababu bado sisi tunatakiwa tutoe huduma kwa wananchi. Kwa hivyo huu ni kama mchango tu na mpaka sasa hivi huu ndio utaratibu uliowekwa na fedha hizi zinakwenda serikalini, nyinyi wenyewe mtaona kwamba fedha tunazopeleka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka uliopita ni kama shilingi milioni mia mbili na zaidi, lakini bajeti yetu ni zaidi ya shilingi bilioni mbili. Kwa hivyo sio biashara ni suala la kutoa huduma kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spka, ubora wa mfumo mpya wa usajili. Mfumo ni bora lakini huu ulifanywa kama ni *pilot* katika Mkoa wa Mjini/Magharibi, na ndio maana sasa kwa sababu tunauona ni mzuri, ndio maana tunataka kuufanya kwa nchi nzima. Kwa hivyo mfumo ni bora.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Zulfa Mmaka Omar kuhusu vyeti vya kuzaliwa nadhani jibu langu nishalieleza kwa sababu ya muda naomba majibu yawe yametosha. Ubadilishaji wa muonekano nao unakuja kwenye mfumo mpya naomba aridhike na hayo.

Mhe. Sima Mohammed Said bajeti ya mfumo mpya usajili ni ndogo nimeshasema, ile bajeti ya *OC* ya kawaida sio bajeti ambayo itatengenezea mfumo. Mfumo tumeupangia mradi ambao una jumla ya shilingi milioni 500 mkiangalia kwenye vitabu vyetu hivyo mtaona.

Mhe. Hamza Hassan Juma usajili wa matukio ya kijamii kuangaliwa tena kwa vile ni bajeti ndogo. Nakubaliana na yeye kama nilivyosema bajeti ni ndogo lakini kwa mwaka huu angalau tumeweka shilingi milioni 500. Mhe. Naibu Spika, na nimuombe Mhe. Hamza Hassan Juma Mjumbe wa UWAWAZA akubaliane na kile ambacho serikali tumekipanga kwa sababu lazima tukubaliane kwamba mahitaji ni mengi lakini fedha ni pungufu.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma idadi ya maafisa waliopandishwa vyeo. Mheshimiwa naomba niseme kwa ujumla, wale wote waliostahiki kupandishwa vyeo wamepandishwa vyeo na katika kupandisha vyeo kwenye uaskari hakuna mwanamke wala mwanamme wote ni askari tu. Kwa hivyo anapandishwa vyeo kwa mujibu wa namna anavyoonekana. Kwanza muda, lakini pili mafunzo aliyoyapata. Kwa sababu cheo sio kupanda cheo tu, cheo unatakiwa ukifanyie kazi. Kwa hivyo tunapandisha vyeo kwa mujibu wa taratibu zetu. Naomba

Mhe. Mwanaasha Khamis hili la wanawake na wanaume tuliache kwa hapa, na hili la idadi ya wangapi wamepanda vyeo pia namuomba tuliache. Lakini wale wote ambao wamestahiki kupandishwa vyeo wamepandishwa vyeo.(*Makofi*).

Idadi ya Watumishi waliopatiwa mafunzo kati ya hao wangapi ni wanawake, ndio vile nilivyosema mafunzo yametolewa kwa vikosi vyote lakini wangapi wanawake, wangapi wanaume naomba nisilijibu. Kwa heshima zote Mhe. Naibu Spika, nakuomba hili nisiliseme.

Kuhusu barabara za ndani. Wajumbe wengi wamezungumzia suala la barabara za ndani na tunathamini mchango wao. Barabara zote ambazo sisi kama Serikali za Wilaya, Serikali za *local government*, Mabaraza ya Miji, Halmashauri, tumefanya uchambuzi yakinifu kwa barabara zenye ukubwa wa kilomita 50.8 Unguja na Pemba. Sasa barabara hizi Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji anaweza akanisaidia. Gharama za ujenzi wa barabara kilomita moja ni kubwa na tabaan mpaka sasa chanzo tulichonacho cha ujenzi wa barabara ni kimoja kutoka Mfuko wa Barabara ambacho ni asilimia 15 tu, asilimia 85 inakwenda kwenye Idara ya Ujenzi wa Barabara. Kwa hivyo tungetamani barabara zote za ndani tuzijenge lakini uwezo huo sisi kama *local government* hatuna, ndio maana tunakwenda kwenye hizi *portion* ndogo ndogo.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo Ofisi yangu imetengeneza andiko la mradi kwa barabara zote za vijijini kupeleka Wizara ya Fedha kupitia Tume ya Mipango, ili barabara hizi nazo ziingizwe ndani ya zile barabara ambazo zinapata mikopo, zinapata ufadhili kutoka nchi wahisani na mashirika ya kifedha ya kimataifa, badala ya kusubiri tupate fedha kutoka kwenye Mfuko wa Barabara peke yake. Wazo kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha la kuongeza tozo lililotolewa na Mhe. Hamza Hassan Juma, serikali tumelipokea. Kama alivyosema Waziri wa Fedha kwa bajeti hii kwa sababu serikali ilishaweka msimamo wa kutokuongeza kodi na wadau wote wa kodi walishajua kwamba hakuna kodi iliyoongezwa, tunaomba jambo hili serikali tulifanyie kazi kama alivyosema Waziri wa Fedha kwa bajeti ijayo kuona kwamba tunaweza tukaweka. Lakini ni zuri sana wazo lako Mhe. Hamza Hassan na serikali kama alivyoahidi Mhe. Waziri wa Fedha tutalifanyia kazi.

Mhe. Hamza nataka nimjibu kabisa Mjumbe wa UWAWAZA na suala hili limezungumzwa na Waheshimiwa wengi hasa wanawake la tukio lililotokea la kuwaondosha kazini wafanyakazi tisa wa KMKM. Kwanza nataka nizungumze kitu kimoja hapa Waheshimiwa tuelewane. Sheria inapokuwa na makosa, ufumbuzi wake ni kurekebisha Sheria si kufanya vyenginevyo. Kwa hivyo

jambo hili limetokea, wanaohusika wamelichukua kwa mujibu wa sheria limefanyika. Lakini nataka niombe niwaambie Waheshimiwa vyombo hivi vyote vilivyotajwa vimo ndani ya Ofisi hii. Ssisi wenyewe tuliitana tukaona wapi tumekosea, ilitajwa hapa Tume ya Utumishi nini, lakini kuna ngazi zilikuwa zifanye kazi kabla ya Tume ya Utumishi, kwa sababu kuna *court-martial* wale kwanza walitakiwa wawajibike kwenda kutoa malalamiko yao kama wanataka rufaa kwenye hizo taasisi halikufanyika, limekwenda moja kwa moja kwenye Tume. Kwa bahati mbaya ndio hayo mambo yametokea.

Hata hivyo wahusika wamekiri mbele ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwamba wamefanya kosa, lakini pia wamekiri kwa maandishi kwamba wamefanya kosa. Sasa jambo hili nimeletewa Waziri niachieni nitumie busara za Uwaziri. Tusiliamue hapa Barazani kwa sababu jambo hili linakwenda kwa mujibu wa Sheria, niachieni. Mimi ni Waziri nina busara, nina hekma, ninafuata sheria, kwa hivyo niachieni nione jambo hili nitalishughulikia vipi. *(Makofi)*

Suala la mpango wa barabara kuzifanyia matengenezo nadhani nimeshalisema, lakini katika kuzungumza jambo hili kuna barabara Wajumbe wamechanganya zile *feeder roads* na *main roads.* Hili nalo serikali kupitia Wizara hizi mbili tutakaa sasa tuje na mpango tuainishe zipi barabara ambazo zinashughulikiwa na Wizara ya Ujenzi na zipi barabara ambazo zinashughulikiwa na Tawala za Mikoa.

Nadhani hapa hatujawa *very clear* ni zipi barabara za Tawala za Mikoa na zipi barabara za Wizara ya Ujenzi. Sasa kwa sababu sote ni serikali tutakaa tuje na mpango na mpango huu tutauleta mbele ya Baraza la Wawakilishi kuwaarifu rasmi Waheshimiwa Wawakilishi kwamba zipi barabara za ndani. Lakini kwa jumla nia ya kujenga barabara zote za ndani hasa kwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na kutekeleza ahadi za Mhe. Rais, tuna nia safi ya kuona kwamba ifikapo mwaka 2020 barabara zote tumeweza kuzijenga kwa kiwango cha lami na zile nyengine kwa kiwango cha kifusi. Kwa hivyo hili sina jibu la mkato kwamba lini tutajenga wapi, isipokuwa tuendelee kutupa muda.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani barabara ya Mpendae na Jang'ombe, ile barabara kweli Mhe. Mbunge wa Jimbo la Mpendae alitoa mchango wa shilingi milioni mia moja na zilikwenda Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Sasa namna gani serikali itatekeleza nadhani tuachiwe ili tukae na Wizara ya Ujenzi tuone tutafanya nini. Lakini barabara ya Kidongo Chekundu-Urusi, nayo ni katika zile barabara tulizozifanyia upembuzi yakinifu ambazo ziko kwenye Halmashauri na utaratibu wake ni ule niliouleza mwanzo. Sambamba na

barabara ya Mboriborini-Shaurimoyo-Kwamtipura ya kule wanakokaa Watumbatu wengi, nayo vile vile iko katika mpango huu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla barabara zote Waheshimiwa Wajumbe kila mmoja kataja jimbo lake na niseme kwamba barabara hizo ni zile kilomita 50.8, ambazo tumezifanyia upembuzi na tunataka kutafuta namna ya kuweza kuzitekeleza kwake kupitia fedha hizi za Mfuko wa Barabara, lakini kupitia fedha za nchi wahisani na mashirika ya kimataifa. Kwa hivyo suala la barabara nimelijibu kwa watu wote.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri una dakika kumi za kumalizia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika ahsante kama nilivyosema.

Naomba nizungumzie jambo moja ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa kuhusu suala la uzuiaji wa *disco.* Namshukuru sana Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo amelitolea ufafanuzi vizuri, lakini serikali haijapatapo kuzuia *disco*. Serikali iliweka muda wa kupiga *disco* na muda huu unakwenda hatua kwa hatua. Kwanza imezuia upigaji wa ngoma ndani ya mitaa isiyostahiki na serikali imeruhusu upigaji wa *disco* kwenye mahoteli huko ya kitalii. Na kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi imeruhusu Hoteli ya Bwawani na Ngalawa, lakini imeruhusu vipi. Kwanza iliweka muda mpaka saa sita ya usiku kwa sababu kulikuwa na sababu nyengine ambazo serikali iliona hebu ijaribu kuzuia baadhi ya maeneo ili kujua kama ndio chanzo au kuna kitu chengine. likiwemo hili suala la udhalilishaji, suala la madawa ya kulevya na suala la usalama pia. Kwa hivyo tukaanza na muda wa saa sita, lakini baada ya serikali kufanya uchunguzi wake, ikagundua kwamba baadhi ya mambo hayapo, ikapandisha muda mpaka saa nane ya usiku na ndio ruhusa iliyopo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Sika, sasa mimi nadhani tujenge tabia ya kufuata maelekezo ya serikali. Sisi tunathamini sana vijana wetu wote na ile ndio sehemu yao ya kukonga moyo. Lakini serikali inapoona kuna hitilafu lazima ichukue hatua kwa maslahi ya wananchi wenyewe wala sio kwa maslahi ya mtu binafsi. Kwa hivyo hili jambo linazungumzika lakini katu hatutaruhusu kupiga ngoma ovyo, anayepiga *disco* lazima afuate utaratibu. Sasa tumekuja mpaka saa nane.

Mhe. Naibu Spika, mimi najua kiu ya vijana wanataka mpaka riamba au sio. Sasa tutaendelea kufungua taratibu pale hali itakapotengemaa basi hakuna tatizo. Lakini tutakuwa umejihakikishia kwamba yale mambo maovu ambayo

yalikuwa yanatia hofu serikali na lawama nyingi ambazo serikali tulikuwa tunapewa yameondoka na watu wa umri gani waende kwenye nyumba hizo za starehe. Lazima tukubali baadhi ya mambo yaliyokuwa yanafanyika katika maeneo hayo hayakuwa mazuri, tuwe wakweli, *clips* nyengine tumeziona sisi wenyewe, vyooni watu walikuwa wakifanya nini, sina haja ya kusema. Kwa hivyo mimi nadhani tukubaliane kwamba jambo hili linazungumzika. Serikali haijazuia isipokuwa iliweka muda kwa sehemu maalum Hoteli ya Bwawani na Ngalawa mpaka saa sita na hatimaye sasa hivi imetoa ruhusa mpaka saa nane. Lile suala la askari wetu kwenda wakafanya *harassment*, nafikiri hilo nalo pia tunaweza tukali-*control*, tutaangalia ni kwa jinsi gani hilo limeenda.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini limejitokeza jambo hapa lililotokea siku ya *Swahili Festival.* Limetokea jambo Mhe. Ibrahim Hussein Makungu amelizungumza dhidi ya Mkuu wa Mkoa. Naomba sana sisi hili jambo tumelisikia na Mheshimiwa alikwenda kweli lakini alikwenda kwa sababu lile jambo lilikuwa limekusanya watu kutoka sehemu mbali mbali. Kama lilivyokuwa la *Full Moon Party*.

Serikali ya Mkoa wa Kaskazini ilipiga marufuku au sio, mnajua wadau? Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo unajua? Mjumbe wa UWAWAZA ulikwenda siku moja ukawa mgeni rasmi kule, lakini ilipiga marufuku kutokana na yale mambo ambayo tunayaona hayafuati silka na utamaduni wa Wazanzibari. Lakini Serikali ya Mkoa wa Kaskazini ilipojiridhisha na utaratibu wa *full moon party* serikali iliruhusu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo na hili serikali nafikiri itafikia pahala ikiona zile shaka zote, mana kila taarifa unatakiwa uifanyie kazi.,Ssi jambo la busara kusikia taarifa za mambo maovu serikali ikanyamaza lazima izifanyie kazi. Kwa hivyo mimi niombe tu kwamba hili jambo ni la muda na niishie kusema linazungumzika.

Hili suala la *Swahili Festival* Mhe. Hussein Ibrahim Makungu limekuja na shutuma dhidi ya Mhe. Mkuu wa Mkoa. Mhe. Mkuu wa Mkoa anapokwenda anakwenda na vyombo vya ulinzi na usalama. Taarifa inaonekana ulizozipokea wewe, inaonekana hazikuwa na usahihi mzuri. Lakini sisi tunasema tutaendelea kuzifanyia kazi. Lakini namna ulivyoli-*address* Mheshimiwa unajua litakuwa limemuumiza kidogo Mhe. Mkuu wa Mkoa. Kwa hivyo basi tutumie busara ni busara gani tutatumia ili kwanza yale ambayo tumemtwika nayo, wananchi huko nje waone kwamba sivyo yalivyo. Maana inasadikiwa Mkuu wa Mkoa alikwenda pale na akatoa *speech* ya kukataza hayo ambayo

wamelezwa humu na halafu akaondoka. Hayo ambayo yamezungumzwa hapa kama yalifanyika Mkuu wa Mkoa hakuwepo.

Kwa hivyo mimi sisemi uombe radhi, lakini busara gani utatumia ili hili jambo wananchi wasilielewe kama hivyo ambavyo umelieleza. Tumefanya *research*, tulikuwa na vyombo pale havitupi taarifa hizo. Waziri wa Habari yule pale sidhani kwamba alikataa kwenda kwa sababu ya mambo, maana lile jambo *Swahili Festival* na *Swahili Festival* linazingatia silka na utamaduni wa Afrika na Waswahili na Wazanzibari.

Niombe tu Waheshimiwa Wajumbe tunapo-*address* au tunapoweka vitu vyetu hapa, tuhakikishe tumevifanyia utafiti wa kutosha. Kwa hilo naweza kusema hivyo.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda umekwisha.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Ahsante sana, Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema majibu ya hoja zote yapo, lakini kwa sababu ya Kanuni na muda na wizara hii kubwa na wachangiaji wengi wamechangia, nisingeweza kusema yote. Kwa hivyo kwa heshima na taadhima nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waridhike na maelezo ambayo nimeyatoa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ametoa hoja. Sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza kabisa nikushukuru na nikupongeze sana Mhe. Waziri pamoja na Mawaziri wengine ambao walitoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wawakilishi. Niwapongeze na niwashukuru sana kwa kuweka mambo sawa.(*Makofi*).

Vile vile nikushukurini na nyinyi Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yenu pamoja na utulivu wenu na kwa kuwa muda haututoshi tena, tulijipanga tumalize leo lakini kwa kuwa muda haututoshi shughuli nyengine ya kuingia katika Kamati tutaifanya kesho asubuhi. (*Makofi*)

Kwa maana hiyo, nichukue fursa hii kuahirisha kikao chetu hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 2.46 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 18/05/2017 saa 3:00 asubuhi)